

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Tisa – Tarehe 17 Novemba, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae, Katibu.

NDG.RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:**

Maelezo kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa mwaka 2017 yaani *The Drugs Control and Enforcement Amendments Bill 2017.*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya masuala ya UKIMWI.

MHE. DANIEL E. MTUKA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya UKIMWI kuhusu maoni ya Kamati juu ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Sura Namba 95 wa mwaka 2017 yaani *The Drugs Control and Enforcement Amendments Act of 2017*.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Masuala ya marekebisho ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya kwa mwaka 2017 (*The Drugs Control and Enforcement Amendments Bill 2017*).

MASWALI NA MAJIBU

Na. 107

Ujenzi wa Barabara za Vijijini - Igunga

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU aliuliza:-

Zaidi ya asilimia 70 ya eneo la Jimbo la Igunga lilikuwa limefunikwa na maji ya Ziwa Victoria lakini baada ya Ziwa hilo kukauka, eneo hilo limebaki kuwa ni mbuga inayojaa maji wakati wa masika hivyo kufanya ujenzi wa barabara za vijiji kuwa wa gharama kubwa sana na Halmashauri ya Wilaya ya Igunga haina uwezo wa kifedha kujenga barabara hizo.

Je, kwa nini Serikali isiandae mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara za vijijini katika Wilaya ya Igunga na Wilaya nyingine nchini zenye tatizo kama hili?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Jimbo la Igunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua tatizo la udongo, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini yaani *TARURA* imepanga kufanya utafiti wa udongo huo ili kuona kama unafaa baada ya kuongezewa kemikali (*additive*) badala ya kuondoa na kuleta udongo mwingine na hivyo kupunguza gharama za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Halmashauri ili ziweze kupitika kwa kipindi chote. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Igunga shilingi milioni 336.8 ambazo zilitumika kufanya matengenezo ya barabara kilometa 119.3, madaraja 8 na kalvati 10. Vilevile katika mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri hiyo imetengewa shilingi bilioni 1.26 ambapo hadi tarehe 30 Septemba, 2017 fedha zilizopokelewa ni shilingi milioni 241.9. Taratibu na kumpata mkandarasi zinaendelea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu swali la nyongeza

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo yametoa matumaini kwamba watafanyia *research* udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi, Jimbo la Igunga ni Jimbo ambalo udongo wake hauwezi kujengwa kwa kukwangua barabara lazima uweke tuta kwahiyo hela zinazotengwa kwa Halmashauri hizi hazitoshi kabisa kujenga hizi barabara.

Swali la kwanza, je, kwa nini Serikali isilete upendeleo kwenye Jimbo hili la Igunga ikasaidia kujenga barabara za vijijini?

Swa li la pili, kwa azma ya Serikali ya kuunganisha Mikoa Tanzania, kwanini Serikali isijenge kwa kiwango cha lami barabara inayotoka Kolandoto kupitia Igurubi kwenda Igunga, Mbutu na kwenda mpaka Loya kwenye Jimbo la Igalula na mpaka Tura kwenye barabara ya lami itokayo Tabora kwenda Dodoma?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo swali lake la msingi linaeleleza jinsi ambavyo eneo lile linahitaji kutazamwa kwa umakini kwani udongo ule ni tofauti na maeneo mengine.

Kwanza naomba nikubaliane naye kwamba siyo kama suala la upendeleo lakini ni vizuri tutakatazama kulingana na hali ya barabara zile na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, *essence* ya kuanzia *TARURA*, Waheshimiwa Wabunge wengi tumekuwa ni mashahidi hapa tumekuwa tukiomba barabara zetu zipandishwe hadhi zichukuliwe na *TANROADS* kwasababu tukiamini *TANROADS* inafanya kazi vizuri zaidi. Naamini kwa kuanzishwa kwa chombo hiki cha *TARURA* hakika barabara zetu zitatengenezwa katika kiwango ambacho kitakuwa bora zaidi. Naamini na barabara hii ya Mheshimiwa Kafumu nayo kwa kupitia *TARURA* na kwa sababu inahitaji kiasi kingi che fedha, fedha ambayo itatengwa na Serikali itakuwa nyingi ili kuweza kukidhi hali ya barabara hiyo.

Kuhusiana na swali lake la pili la kuunganisha barabara kutoka Kolandoto mpaka Tura ambayo kimsingi jiografia yake inaonyesha ni kwamba itakuwa ni kiungo kikubwa sana mpaka kufika Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kama Serikali tulichukue, tulifanyie kazi halafu tuone namna itakayokuwa bora katika kulitekeleza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje swali la nyongeza

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mgao wa *Road Fund* Serikali Kuu wanachukua asilimia 70 na Serikali za Mitaa asilimia 30 na kwa kuwa Serikali imeunda chombo cha *TARURA* na kama mgao utakuwa asilimia 30 zile zile na barabara zetu ni mbaya sana vijijini kule hasa Wilaya ya Mpwapwa.

Je, sasa mgao utaongezeka iwe asilimia 50 kwa 50?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi asilimia 70 na asilimia 30 ni kwa mujibu wa Sheria na Sheria hii ilitungwa na Bunge lako Tukufu. Kama haja itakuwepo kwa wakati huo tutakubaliana kiasi gani ambacho kitafaa na lengo ni kuhakikisha kwamba chombo hiki ambacho tumekianzisha *TARURA* kinakuwa na uwezo ili kiweze kukidhi haja iliyoanzishwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche swali la nyongeza.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambazo ziko kwenye Mji mdogo wa Sirari na Mji mdogo wa Nyamongo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais akiwa pale na ziko *TARURA*.

Unasemaje kuhusu kutupa angalau kilometa mbili za lami ili kuondoa matatizo kwenye Mji ule ambao una watu wengi Miji miwili hii ambayo ni Sirari na Nyamongo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za Mheshimiwa Rais zimetolewa maeneno mengi na sisi sote ni mashuhuda kwamba tumeletewa taarifa kwamba uratibu utafanyika kuhusiana na ahadi zote ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Rais na kimsingi katika kutekeleza ahadi hizo tunahitaji miaka mitano, ndani ya miaka mitano tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba ahadi za Rais zinatekelezwa naamini katika kipindi hicho na eneo lake litatekelezwa kwa kujengewa hiyo barabara ya lami.

Na.108

Uhaba wa Watumishi Idara ya Afya Wilaya ya Urambo

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Tatizo la uhaba wa watumishi wa Idara ya Afya Urambo linaathiri utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura katika kuliondoa tatizo la uhaba wa watumishi wa Idara ya Afya Wilayani Urambo?

(b) Je, Serikali inaweza kuchukua vijana wa Urambo na kuwapeleka vyuoni kusoma kwa makubaliano ya kurudi kufanya kazi Urambo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ina upungufu wa watumishi wa kada ya afya. Tatizo hili linazikabili Halmashauri nyingi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwaajiri wataalam wa kada ya afya kipindi wanapohitimu mafunzo na kufaulu vizuri katika masomo yao. Aidha, kuanzia mwezi Novemba, 2015 Serikali ilisitisha zoezi la kuajiri ili kubaini watumishi wa umma walioajiriwa na hawakuwa na sifa stahiki na kuwatambua watumishi halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilisha zoezi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeendelea kutoa vibali vya watumishi wa kada za afya ambapo mwezi Aprili, 2017 tulipata kibali cha kuajiri madakrati 209. Katika kibali hicho, Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ilipata madaktari wawili. Vilevile mwezi Julai, 2017 tumepokea kibali cha watumsihi 2,152 ambao wamepangiwa katika Mikao na Halmashauri kwa uwiano ili kupunguza uhaba wa watumishi. Katika mgao huu Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ilipata watumishi 17. Serikali itaendelea kupanga watumishi kwa kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kuwasomesha vijana kwa makubaliano ya kurudi kufanyakazi umeshindwa kufanikiwa kwani uzoefu unaonesha vijana wengi wamesomesha na kuhitimu wanakuwa wamebadili mawazo na kuamua kufanyakazi sehemu nyingine na kuacha mgogoro kati ya wasomeshaji na aliyesomesha. Serikali inaendelea kuboresha mazingira kama vile upatikanaji wa nyumba pamoja na huduma za kijamii ili kuwafanya

watumishi wanaoajiriwa waweze kubakia katika maeneo waliyopangwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Margaret Sitta swali la nyongeza.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, lakini kabla ya hapo naomba uniruhusu kwa kifupi sana nimshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Kandege alifika Urambo na kujionea mwenyewe, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, karibu tena, ulifanya kazi nzuri na kusababisha tupate wafanyakazi 17 kama ulivyosema lakini sasa swali la nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Serikali imeona uhaba wa wafanyakazi uliopo na kutokana na wagonjwa wengi kutoka jirani zangu Kaliua ambako hawa Hospitali ya Wilaya wakiwemo kutoka Ulyankulu, Uyui, Uvinza. Naomba kuwauliza Serikali kama wako tayari kuongeza wafanyakazi ili tuendeleo kutoa huduma nzuri?

Swali la pili ni kwamba, kutokana na ongezeko la wagonjwa wengi kutoka Kaliua, Uyui, Uvinza ikiwemo Ulyankulu, je, Serikali iko tayari kutuongezea fedha ikiwemo fedha za *Busket Fund* ili tuweze kumudu ongezeko la wagonjwa ambao wanatoka jirani? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba wa dhati nipokee pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi tulifanya ziara kule na tukajionea kazi nzuri ambayo naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana jinsi ambavyo anahangaika na suala zima la afya za wananchi wa Urambo na tulipata fursa ya kutembelea Hospitali ya Wilaya na katika moja ya ombi ambalo Mheshimiwa Mbunge aliwasilishwa kwetu Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni pamoja na suala zima la kubadilishiwa matumizi kiasi cha shilingi milioni 150 ili ziweze kutumika katika kujenga wodi ambayo ni *Grade A* wazo ambalo tumelichukua na punde tutalifanyia kazi ataweza kupata majibu ili pesa ile iweze kutumika.

Kuhusiana na suala zima la uhitaji wa watumishi ili kukidhi haja ya wagonjwa ambao wanasafiri kutoka Wilaya nyingine kwenda Wilaya ya Urambo kwanza naendelea kumpongeza, ukiona wagonjwa wanakuja kwako maana yake huduma ambayo inatolewa na hospitali yako ni nzuri ukilinganisha na wengine.

Kwa nia hiyo hiyo njema na katika kuhakikisha kwamba tunakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Urambo, wewe ni shuhuda tulikubaliana, jitihada zinafanywa na Serikali hivi karibuni pesa zitakuja kwa ajili ya kulimalizia ile wodi ambayo ilikuwa imeanzishwa kutoka Wizara ya Afya.

Lakini kama hilo halitoshi, naomba niungane mkono kabisa na Mheshimiwa Magret Simwanza Sitta kwamba iko haja ya kutazama kwa kadri nafasi itakavyoruhusu watumishi wakipatikana ili kuweza kuongeza maana ukienda Kituo cha Afya Usoke pale tumeona kazi nzuri ambayo inafanyika na itakamilika hivi karibuni iko haja ya kuongeza watumishi pale watakapokuwa wamepatikana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri niwakmbushe maagizo ya Spika ya jana kuhusu maswali mafupi na majibu mafupi.

Na.109

Umuhimu wa Kujenga Nyumba za Walimu Vijijini

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO aliuliza:-

Ukosefu wa nyumba za walimu maeneo ya vijijini husababisha walimu kuhama maeneo hayo na hivyo kupelekea upungufu mkubwa wa walimu. Aidha, Halmashauri nyingi zikiwemo za Mkoa wa Ruvuma hazina uwezo wa kujenga nyumba za walimu kwa kutumia fedha za ndani.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga nyumba za walimu wa shule za msingi vijijini ili kuweka mazingira rafiki ya kufanya kazi kwa walimu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa upo upungufu wa nyumba za walimu nchini. Nyumba zilizopo kwa ajili ya walimu wa shule za msingi ni 41,321 wakati mahitaji halisi ni nyumba 222,115 hivyo kuna upungufu wa vyumba 179,794 sawa na asilimia 81. Mkoa wa Ruvuma una upungufu wa nyumba 5,470 za walimu wa shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Seriakli ina mikakati mbalimbali ya kuboresha utoaji wa elimu Nchini ikiwemo kutenga fedha za ujenzi wa nyumba za walimu. Kwa mwaka wa fedha 2017/18 Seriakli imetenga jumla ya shilingi bilioni 12.8 kwa ajili ya uejzi wa nyumba 1,669 za walimu wa shule za msingi nchini. Mkoa wa Ruvuma umetengewa shilingi milioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 30 za walimu wa shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuendelea kujenga nyumba za walimu kadri fedha zinavyopatikana kwa lengo la kuboresha mazingira na makazi kwa walimu. Ujenzi wa nyumba za walimu ni jukumu la wadau wote kuanzia Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, wananchi kwa ujumla, hivyo natoa wito kwa wadau wote walimu kuchangia ujenzi wa nyumba za walimu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sikudhani Chikambo swali la nyongeza

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:Mheshimiwa Naibu Spika, asante kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi kwamba ukosefu wa makazi bora ya walimu kunawakatisha tamaa walimu kuishi vijijini na mara kwa mara walimu wengi wamependa kuhama kutoka kwenye maeneo haya na kuhamia maeneo ya mijini ambako kuna makazi bora. Ukichukulia Halmashauri moja tu ya Tunduru mahitaji ni nyumba za walimu 1782; upungufu 1688 lakini Naibu waziri amesema ana mpango wa kujenga nyumba 30 katika mkoa mzima wa Ruvuma naona hii kasi ni ndogo nilipenda kujua Serikali ina mkakati gani katika kuhakikisha jambo hili tunalimaliza kwa haraka na ukizingitia sisi wote tumetokana na hao walimu? Ahsante.

NAIBU SPIKA:Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba ni wajibu wetu sisi Serikali Kuu Halmashauri pamoja na wananchi kwa ujumla tukizingatia kwamba upungufu huu ni mkubwa sana haitakuwa busara tukasema tunaiachia Serikali peke yake, tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba tunashirikishana ili tatizo hili tulimalizekwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii naomba nirejee kwa ruhusa yako jana wakati Mheshimiwa Gekul wakati anaomba Mwongozo kwa Mheshimiwa Spika alisema

kwamba kuna barua (Waraka ambao umetolewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI) ukiwataka wananchi kwamba kuanzia sasa hivi ni wajibu kushiriki kuanzia mwanzo kwa maana ya msingi hadi kwenda kumaliza. Kabla Serikali haijaleta taarifa yake rasmi naomba niseme kwamba hakuna waraka kama huo ambao umepelekwa ni wajibu wetu sisi wananchi pamoja na Serikali kushirikiana ili kumaliza matatizo yanayohusu watumishi wa Serikali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakoso swali la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa na vyumba na uhaba wa nyumba za walimu limekuwa tatizo kubwa sana na Jimbo langu ni miongoni mwa matatizo ambayo yanawakabili katika shule ya Busongola, Bulamata, Vikonge, Mchangani, Kapanga na Kafishe ambako kuna vyumba viwili tu vya madarasa lakini zipo darasa saba. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa na uhaba wa nyumba za walimu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Naibu wangu Mheshimiwa Kandege kwa *clarification* nzuri kwa maswali yote yaliotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna changamoto kubwa sana ya vyumba vya madarasa na ndio maana kwa Serikali kipindi hiki cha sasa tulifanya tulitumia takribani shilingi bilioni 21 kuhakikisha tunaongeza vyumba vya madarasa katika shule za sekondari 85 na shule za msingi 19. Lakini hata hivyo kipindi cha muda mfupi uliopita tumetumia takribani shilingi bilioni 16 kufanya uwezesaji mkubwa katika shule za sekondari 65 na shule za msingi 56 lakini hata hivyo naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge katika fedha tulizozitenga takribani shiling bilioni 246 kwa ajili ya kusaidia kwamba yale maboma yaliyojengwa kuhakikisha

tunayakamilisha naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tushirikiane vya kutosha na wizara ya fedha, fedha ziweze kutoka ziende katika halmashauri zetu kwa lengo la kumalizia viporo na kujenga maeneo mengine lengo kubwa wanafunzi wetu wapate mahali pa zuri pa kusomea.

NAIBU SPIKA:Mheshimiwa Zacharia Issaay swali la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi mimi ni kwa namna gani Serikali itoe utaratibu wa jamii, Halmashauri na Serikali Kuu kuweza kuweka nguvu pamoja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu hivi sasa maboma yaliyo mengi katika Halmashauri zetu yamechukua miaka mingi ningeomba basi Mheshimiwa Waziri atume wataalamu kwa baadhi ya maeneo machache ili kunyambulisha ni gharama gani zitakazotumika katika ujenzi wa nyumba hizi za walimu na tuwe na lengo kwa kila Halmashauri kwa zile nyumba ambazo ziko katika lenta ili tuweze kukamilisha kuungana na wananchi. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Issaay nadhani swali lake limejenga katika kujenga suala zima la ushauri na kiufupi kwamba ushauri huu tumeuchukua ndio maana tuliongeza bajeti katika mwaka huu wa fedha kutoka shilingi bilioni 150 npaka kufika shilingi bilioni 246 kwa lengo kubwa kuweza kuhakikisha eneo hilo tunalifanyia kazi. Lakini tunafanya kazi hilo katika maeneo yote sekta ya afya na sekta ya elimu ambapo Mheshimiwa Issaay ndio ulikuwa umejenga hoja ya msingi kipindi cha Bunge lililopita.

Kwa hiyo, naomba niseme tatalichukua hili naamini kwa pamoja tukishirikiana lakini hata hivyo nipende kuwapongeza Wabunge hasa wanaotumia Mfuko wa Jimbo na kwa kushirikiana na maeneo yao ambapo katika tembea

yangu nimekuta miradi mingi ambayo Wabunge kupitia Mfuko wa Jimbo wameingiza fedha kuhakikisha nyumba za walimu na madarasa yanafanyika hivyo, kwa hiyo nawapongeza sana kwa hali hiyo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendekea na Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mbunge wa Arusha mjini sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Heche kwa niaba ya Mheshimiwa Godbless Lema.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na mipango majibu.

Na. 110

Kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika Vifaa vya Ujenzi

MHE. JOHN W. HECHE (K.n.y. MHE. GODBLESS J. LEMA)
aliuliza:-

Kukosekana kwa mpango madhubuti wa Mipango Miji pamoja na gharama kubwa za ujenzi zinazosababishwa na kodi kubwa katika vifaa vya ujenzi kumefanya wananchi kujenga kiholela.

(a) Je, ni kwa nini Serikali isiondoe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vyote vya ujenzi?

(b) Shirika la Nyumba la Taifa linajenga nyumba bora za makazi na bashara; je, ni kwa nini Serikali isiondoe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyumba za Shirika hilo ili ziwe za bei nafuu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa fedha na mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa

Godbless Jonathan Lema, Mbunge wa Arusha Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vya ujenzi hutumika kwa ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo nyumba za makazi pamoja na nyumba za biashara. Kwa kuwa matumizi ya vifaa vya ujenzi ni mtambuka, ni vigumu kutambua kama mnunuzi atatumia kwa ujenzi wa makazi binafsi, biashara au miundombinu kama vile barabara, umeme na maji. Hivyo basi, kuondoa VAT kwenye vifaa vya ujenzi kwa lengo la kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba za makazi kunaweza kabisa kuwanufaisha zaidi wafanyabiashara wachache kuliko mwananchi wa kawaida na pia kusababisha kupungua kwa mapato ya Serikali na hivyo Serikali kuwa na uwezo mdogo wa kutoa huduma muhimu kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa bei ya bidhaa nyingine bei ya vifaa vya ujenzi haipangwi kwa kutumia kigezo cha kodi ya VAT pekee, bali hutokana na gharama mbalimbali zikiwemo za uzalishaji kama vile malighafi, umeme, maji, nguvu kazi, teknolojia pamoja na miundombinu ya usafirishaji na msukosuko wa nguvu ya soko. Hivyo basi, kuondoa VAT kwenye vifaa vya ujenzi si kigezo pekee kitakachopunguza gharama za ujenzi wa nyumba za makazi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kutoza kodi ni kuiwezesha Serikali kuwa na mapato ya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kutoa huduma muhimu za jamii kwa wananchi wote. Nyumba zinazojengwa na kuuzwa na Shirika la Nyumba la Taifa ni mradi wa kibiashara na si huduma.

Pili, ni vema ikaeleweka kwamba, wauzaji wa nyumba hapa nchini ni wengi, hivyo uamuzi wa kuondoa kodi ya VAT kwenye nyumba zinazouzwa na Shirika la Nyumba la Taifa pekee utakuwa na sura ya ubaguzi kwa wauzaji wengine wa nyumba, ikiwa ni pamoja na kuikosesha Serikali mapato kwa manufaa ya Taifa letu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche swali la nyongeza.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nasikitika kwa majibu ya Serikali kwasababu vifaa vya ujenzi hata vikijenga barabara, vikijenga kila kitu mwisho wa siku ina mahusiano ya moja kwa moja na maisha ya wananchi wa kawaida. Barabara hizi zimekuwa zikijengwa kwa gharama kubwa na wananchi ndio wanalipa kodi kwa hiyo Serikali hii haioni bado kuna sababu ya kuwapunguzia wananchi wake mzigo kwenye gharama ya vifaa vya ujenzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pilli katika zile *basic human needs* kuna nyumba, mavazi na kuna chakula na heshima ya binadamu yoyote ni mahali anapokaa kwa maana ya makazi. Na nchi nyingine zimeenda mbali kuwapatia wananchi wake makazi hata ya bure, Serikali yenu ya CCM inaona ni muhimu zaidi kutoza kodi kuliko maisha ya wananchi ambao wanaishi kwenye maisha duni na makazi duni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche inavyooneka CHADEMA mkiingia madarakani mtafuta kodi zote. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi na naomba ifahamike kwamba uhai wa Taifa lolote ni kodi hakuna maendeleo ya Taifa lolote bila kodi na kama nilivyosema wafanyabiashara wapo wengi wanafanya kazi hizi na kusema kwamba hapa tunasamehe kwa sababu wanakwenda kujenga nyumba ni watu wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, niulize tu swali na mimi labda hivi kabla ya kodi hii ya VAT mwaka 1998 wananchi walikuwa wakijenga tofauti na wanavyojenga leo baada ya kuwa tunakodi ya VAT? Hiyo si sahihi hata kidogo hali ya ujenzi ipo na sasa hivi tunaona Watanzania wengi wameinuka kimaendeleo na wanajenga nyumba za kudumu kwa asilimia kubwa kuanzia mijini mpaka vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makazi ya bure anayosema Mheshimiwa Heche, makusanyo ya kodi ndio yatakasababisha tutoe huduma kwa wananchi wetu, na sisi tunapoelekea ndio huko huko inawezekana kabisa tukafika sehemu baada ya kuimarisha makusanyo ya kodi ikiwepo kodi ya VAT tukaweza kutoa huduma nyingi kwa wananchi wetu bure lakini kwa kuzingatia kwamba uhai wa Taifa lolote ni kodi na hakuna maendeleo bila kodi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ali King swali la nyongeza.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwanza nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba uhai wa Taifa ni kodi. Lakini kuna kodi inakuwa-*charged* mara mbili ya VAT kwa bidhaa hizo za vifaa vya ujenzi ambavyo vinakwenda Zanzibar kwa wale ambao *non registered for VAT*. Je, Serikali ina maelezo gani juu ya kutatua kero hii ya *double VAT*?

NAIBU SPIKA: Wahehimiwa Wabunge kwa sababu nitawapa Wabunge zaidi wawili kwenye swali hili. Swali la msingi linahusu VAT kwenye vifaa vy ujenzi vya NHC, kwa hiyo tuzingatie hiyo mipaka hata hivyo Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa hayo maswali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza si sahihi kusema kodi inalipwa mara mbili kwa kutoka Tanzania Bara kwenda Tanzania Zanzibar si sahihi. Kodi ya VAT ni kodi ya mlaji inayolipwa na malaji wa mwisho na kodi hii inakuwa-*charged* mara moja tu, kodi ambayo najua ina changamoto ya kusema kwamba ina sura ya kulipwa mara mbili lakini kiuhalisia hailipwi mara mbili ni kodi ya *import duty* ambayo kwa wenzetu Wazanzibari wanapoingiza bidhaa kule Zanzibar mfumo wanaotumia haulingani na mfumo wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo na ile pia hatuwezi kusema ni *double taxation* ile ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na usawa katika soko wa bidhaa zinazolingizwa kutoka nje ya nchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti Majala Swali la nyongeza.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa Serikali inatoza VAT kwenye vifaa vya ujenzi lakini pili tena tuna suala zima la tozo kwenye majengo, je, Serikali haioni sasa kuna sababu ya kumtoza mwananchi huyu kodi moja tukaondoa ya majengo tukabaki na hiyo tozo ya vifaa vya ujenzi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mpiango majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kodi hizi mbili ni kodi tofauti kabisa huku tuna-charge kodi ya VAT kwa mlaji wa mwisho na hasa ambaye yuko *registerd* kwa VAT, ambaye anavuka mapato yake kwa shilingi milioni 100 na kodi ya majengo hii ni kodi tofauti kabisa wala hazina sababu ya kuunganishwa pamoja. Mheshimiwa *this is property tax* na hii ni kodi ya mlaji, ka hiyo, kodi hizi haziwezi kuunganishwa na ikawa kodi moja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jaku swali la nyongeza.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili Mheshimiwa Naibu Waziri mimi ningemuomba, kodi zinalipwa mara mbili Zanzibar na ushahidi upo upo tayari kupokea ushahidi. Wala sina nia ya kutaka kuomba ajiuzulu yuko tayari kumletea ushahidi kodi huku Tanzania Bara inakuwa-*charged* na Zanzibar inakuwa-*charged*. Suala hili bado ni kero.

Lakini la pili...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jaku naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge kodi mara mbili swali linalohusu kodi kulipwa mara mbili si sehemu ya swali la msingi, kwa hiyo, tutendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali Mbunge wa Mchinga Mzee wa Mjusi sasa uliza swali lako.

Na.111

Serikali Kusaidia Sekta ya Uvuvi Nchini

MHE. HAMIDU H. BOBALI aliuliza:-

Sekta ya uvuvi bado haijatumika kikamilifu kulipatia Taifa pato na kuwaondoa Watanzania hususani wavuvi katika dimbwi la umaskini.

(a) Je, ni lini Serikali itaweka jitihada za kusaidia wavuvi hasa wale wanaojihusisha na uvuvi wa Bahari Kuu?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wavuvi wadogo wadogo ili waweze kuvua katika Bahari Kuu?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa sekta ya Uvuvi nchini kwa kutekeleza mikakati yenye lengo la kuendeleza wavuvi nchini ili waweze kupata ajira, lishe, kipato na kuchangia katika Pato la Taifa. Kwa mwaka 2016 sekta ya Uvuvi imechangia asilimia 2.0 katika Pato la Taifa na imekua kwa asilimia 4.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuwasaidia wavuvi wadogo hususani wale wanaojihusisha na uvuvi wa Bahari Kuu Serikali imeanza kuweka vifaa maalum vya kuvutia samaki (*Fish Aggregating Devices - FADs*) ili kuwasaidia wavuvi kupata samaki wengi na kutumia muda mfupi katika uvuvi. Hadi sasa jumla ya *FADs* 77 za mfano zimewekwa katika

maeneo mbalimbali. Vilevile Serikali imetoa mafunzo kwa wavuvi wadogo ili waweze kuvua katika Bahari Kuu ambapo hadi sasa jumla ya wavuvi 150 wakiwemo 83 wa Ukanda wa Pwani ya Bahari wa Hindi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wakulima wakiwemo wavuvi na wafugaji ili waweze kununua zana bora za uvuvi. Aidha, Serikali imeanzisha Dirisha la Kilimo katika Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*). Mikopo hiyo inatolewa kupitia vyama vya ushirika ambayo pamoja na majukumu mengine inatoa pia mikopo ya masharti nafuu kwa watu wanaojishughulisha na sekta za kilimo, mifugo na uvuvi. Ili kuweza kukidhi masharti ya kupata mikopo hiyo, Serikali inaendelea kuwahamasisha wavuvi kujiunga katika Vyama vya Ushirika vya Msingi wa Wavuvi ili kuwa na nguvu ya pamoja na kuweza kukopesheka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bobali swali la nyongeza.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi wa bahari Kuu unahitaji uwekezaji wa fedha na mitaji na wavuvi wengi katika maeneo ya Ukanda wa Pwani walikuwa wanatumia uvuvi wa kupiga mabomu ili kupata samaki na Jimboni kwangu katika maeneo ya Mchinga, Ruvu, Mvuleni, Maloo na maeneo mengine wale watu wameacha sasa upigaji wa mabomu kwa kufuata na kutii sheria za nchi sasa.

Je, nauliza Serikali ina mpango gani ya kuwasaidia hawa wavuvi ambao walikuwa wanavua kwenye eneo la bahari kuu kwa kutumia mabomu na sasa wameacha kwa kutii sheria wana mpango gani wa ziada wa kuwasaidia ili waendelee kuvua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ukanda wetu wa bahari una takribani urefu wa kilometa 1,424 kutoka Tanga

mpaka Mtwara, lakini ukiacha maeneo ya Miji Mikuu kama Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, maeneo yote yaliyopo kwenye ukanda wa bahari watu wake ni maskini sana. Nataka kujua, Serikali inajifunza nini kwa watu wa Ukanda wa Pwani kuwa maskini kwa kiwango kile wakati wana rasilimali hii nzuri ya bahari? Nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo majibu.

NAIBU WAZIRI WA UVUVI NA MIFUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ametaka kujua mikakati zaidi ya namna ambavyo Serikali imejipanga kuwasaidia wavuvi ili waweze kuvua katika eneo la bahari kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi ya kwamba Serikali ina mipango kadha wa kadha na tayari tumekwisha anza nayo. La kwanza ni hili la kuwawezesha kupata ruzuku kupitia vikundi vyao ambapo wavuvi mbalimbali katika nchi yetu wamepata ruzuku hii ya mashine. Hata yeye Mheshimiwa Bobali wavuvi wake wa jimbo la Mchinga tuko tayari kuhakikisha kwamba wanapata mashine hizo za kuweza kwenda kuwasaidia kwenda kufika bahari kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama haitoshi, Serikali kupitia Taasisi mbalimbali na mifumo ya ushirikiano tunao mradi mkubwa wa **SEOFISH** ambao utakwenda kuhakikisha kwamba kama tulivyofanikiwa katika Mradi wa **MACEMP** hapo nyuma utakwenda kuwasaidia wavuvi hawa wa Ukanda wa Pwani kuweza kupata elimu za ujasiriamali, kuweza kuwasaidia kivyombo na kimifumo ili waweze kuwaondoa katika umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili linahusu kwa nini na Serikali ina mpango gani. Ni kweli jamii nyingi za wavuvi wakiwemo wavuvi wa Jimbo la Mkuranga katika eneo la Kisiju ni kweli wapo katika hali ya umaskini na wavuvi wengine wote nchini. Ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Tano ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kujua hilo tukadhamiria kuona

kwamba tuondoe tozo mbalimbali ambazo zinawagusa wavuvi na kuwarudisha nyuma na kupata unafuu wa maisha yao. Tutaendelea na jitihada hizo ili kuhakikisha wavuvi wetu wanapiga hatua ya maendeleo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Sambamba na swali la msingi la Mheshimiwa Bobali napenda niulize swali langu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tunafahamu kwamba kwenye ukanda wa Pwani wavuvi wake ni maskini sana hasa katika mikoa hiyo iliyotajwa na ninataka nizungumzie Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi hauna viwanda, rasilimali pekee iliyopo ni ya bahari na wavuvi wanategemea bahari hiyo ili kujipatia riziki zao. Wavuvi hao wote kule wanavua samaki wengi sana matokeo yake baada ya kuvua samaki wale kwa kuwa wanakosa soko kinachofanyika, samaki wale ni kuwakausha kwa mazingira ya kwetu tunaita ng'onda. Samaki wale wanafanywa kuwa ng'onda yaani samaki wakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaamini kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali ya viwanda. Je, Serikali ina mpango gani juu ya kutuletea au ya kuhakikisha kwamba wavuvi wale wanatengenezewa viwanda ili kuondokana na umaskini waliokuwa nao? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, Lindi sasa ni ya viwanda na ushahidi upo tayari wa kutosha kutokana na malighafi hiyo ya upatikanaji wa gesi. Lindi inanukia katika viwanda na tayari maeneo kama ya Kilwa yameonesha mfano, kuna kiwanda kikubwa sana

cha mbolea ambacho kinaenda kujengwa pale. Nina imani kwa uwepo wa malighafi hii ya samaki na nina imani kwa kuwa Serikali yetu ya Awamu ya Tano ni Serikali ya viwanda na kwa kuwa Mheshimiwa Mwijage na Wizara yake wanafanya kazi kubwa sana ya kuhamasisha viwanda viweze kujengwa na sekta binafsi, ninaamini wawekezaji watakutika na wataenda kuweka kiwanda cha uchakataji wa samaki katika eneo la Lindi na kuondoa kilio hiki cha kukosekana kwa kiwanda cha samaki katika mwambao wetu huu wa Pwani. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swali la nyongeza.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka kumi mfululizo ulimwenguni sekta inayokua kwa kasi katika sekta ya kilimo ni sekta ya samaki. Serikali ipo tayari sasa kuwasaidia wavuvi walioko Ukanda wa Pwani kuondokana na umaskini kwa sababu sekta hii imeonekana ni sekta inayokua kwa kasi? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari kuwasaidia wavuvi kusonga mbele.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Selasini, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kamati ya Mheshimiwa Chenge iliyokuwa inapendekeza kodi mbalimbali mpya ilitoa mapendekezo ya kutumia uvuvi wa bahari kwa ajili ya kuongeza mapato na mara zote ni kwamba Serikali inasema boti za kisasa

ambazo zinaweza zikadhibiti wavuvi wa kina kirefu hazipatikani.

Je, Serikali haioni kwamba kwa kutopatikana kwa boti hizo Serikali inakosa mapato makubwa sana kutokana na wavuvi haramu wa nchi mbalimbali duniani wanaokuja kuvua katika bahari yetu? Ni lini sasa boti hizo zitapatikana? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Selasini swali huwa ni moja tu. Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Selasini anaulizia juu ya uboreshaji wa sekta ya uvuvi na akihusisha na Kamati ya *Chenge One* ambapo mimi nilikuwa mjumbe wa Kamati hiyo tukiwa na Mheshimiwa Selasini. Nimwambie tu Mheshimiwa Selasini kwamba sasa kwa sababu mapendekezo yale tuliyapendekeza ili Waziri wa Uvuvi akayafanyie kazi na mimi ndiye Waziri wa Wizara hiyo sasa hivi aniachie ili tukamilishe mapendekezo hayo ambayo tulipendekeza kwa Waziri wa Uvuvi ambaye leo ni mimi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Majibu murua kabisa hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea. Mheshimiwa Hasana Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Zainab Katimba.

Na. 112

Kuwawezesha Wavuvi Waishio Ukanda wa Ziwa Tanganyika

MHE. ZAINAB A. KATIMBA (K.n.y MHE. HASNA S. K. MWILIMA) aliuliza:-

Shughuli kubwa za kiuchumi kwa wananchi wa Ukanda wa Ziwa Tanganyika ni uvuvi lakini nyavu zimekuwa zikikamatwa na kuchomwa moto.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia wavuvi hao nyenzo au vifaa vya kisasa vya uvuvi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati yenye lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya uvuvi ili kuwawezesha wavuvi wakiwemo wa Ukanda wa Ziwa Tanganyika kufanya uvuvi endelevu na wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeondoa kodi kwenye zana na malighafi za uvuvi zikiwemo *engine* za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu na vifungashio kupitia Sheria ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) ya mwaka 2007. Aidha, kupitia Umoja wa Ushuru wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Common External Tariff*) *engine* za uvuvi na malighafi zinazotumika kutengeneza zana mbalimbali za uvuvi na viambata vyake kwa maana ya *fishing gear accessories 10%* na *outboard engine 0%* zimepewa punguzo la kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi wakiwemo wavuvi ili waweze kununua zana bora za uvuvi. Hivyo wavuvi wahamasishwe kujiunga katika Vyama vya Ushirika ili kuwawezesha kupata mikopo hiyo.

Vilevile Serikali inatekeleza mpango wa kutoa ruzuku ya zana za uvuvi, ambapo wavuvi wenyewe huchangia 60% na 40% iliyobaki ya gharama huchangiawa na Serikali. Hadi sasa *engine* 73 zimenunuliwa kupitia mpango huu, nakati ya hizo *engine* 49 zimelipiwa na kuchukuliwa na vikundi vya wavuvi vilivyokidhi vigezo vikiwemo vitatu kutoka katika

Wilaya ya Kalambo na kimoja kutoka katika Wilaya ya Sumbawanga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zainab Katimba, swali la nyongeza.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninaswali moja la nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba ina hakikisha wavuvi hawa wanapata sokola uhakika baada ya kuhamasisha uzalishaji kwa kuhakikisha kwamba kuna jengwa kiwanda cha kuchakata minofu ya samaki katika ukanda wa *Lake Tanganyika* na hasa ukizingatia kwamba kuna *specie* ya kipekee katika Ziwa Tanganyika ya samaki anayeitwa migebuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali ina mkakati gani kuhakikisha viwanda vinajengwa katika ukanda ule? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa uvuvi katika Ziwa Victoria tumejenga mwalo wa kisasa pale Kibirizi ambapo mwalo ule tumeuwekea vifaa vyote muhimu ambavyo samaki akivuliwa anaweza kutunzwa hata kwa zaidi ya wiki mbili. Yote haya ni kuwafanya wavuvi wanapovua samaki kabla hawajafika sokoni wasiharibike yaani waweze kupata soko kabla hawajaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais tumejenga pale mradi mkubwa sana wa ziadi ya takriban shilingi bilioni mbili zimetumika kwa ajili ya kutengeneza mwalo ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili la pili linalokuja ni la kujenga viwanda sasa kwa sababu tayari tumeshapata mwalo mzuri ambapo samaki wanapokelewa na kutunzwa.

Kinachofuata sasa ni maandalizi ya kujenga kiwanda ili tuweze kuchakata samaki katika ukanda ule na tutafanya hivyo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zainab Matitu Vullu, swali la nyongeza.

MHE. ZAINAB M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya wavuvi wa Uvinza haina tofauti sana na hali ya wavuvi wa Ukanda wa Pwani ya Mkoa wa Pwani. Naomba nizungumzie hasa Kisiwa cha Mafia ambapo wanawake wengi wanajitahidi kulima kilimo cha mwani si kwa wao tu kwa mtazamo wa nje kwamba kinawapatia mapato lakini pia kilimo cha mwani kinasaidia kukuza samaki kuzaliana, kutunza mayai na hata kuhifadhi mazingira bora ya bahari. Kilimo hicho kinalimwa kwa shida sana,

Je, ni lini Serikali itahakikisha inawapatia nyenzo kama viatu, kamba na vifaa vingine vya kulimia mwani ili wananchi hao waweze kulima vizuri? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya vizuri sana Zanzibar katika kilimo cha mwani hasa kwa kuwatumia wataalam wetu hawa wa *COSTECH* pamoja na *IMS*. Tutapeleka wataalam wetu hawa katika eneo hili analolizungumza Mheshimiwa Mbunge ili waweze kwenda kuwafundisha wakulima wetu wanaolima zao la mwani ambalo tunalipendekeza sana sasa hivi kwa wakulima na kulipigania lifanyike kwa ajili ya kuongeza thamani za zao hilo na kujipatia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo eneo hilo ambalo wakulima wanalima kwa shida tunatahakikisha kwamba tunaelekeza nguvu huko kuhakikisha wafugaji wale

tunawapa mafunzo, tunawaonesha soko na vilevile tunawaunganisha kimtaji ili kuhakikisha kwamba zao hilo wanalilima vizuri zaidi kwa sababu lina soko la uhakika duniani. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaita maswali ya nyongeza, tulisome swali la msingi linauliza kuhusu nini ili Serikali iweze kutoa majibu ambayo ni mahsusi kwetu lakini pia yatusaidie kusonga kutoka pale tulipo. Tukiuliza maswali nje ya swali la nyongeza tusitarajie majibu kutokea hapa. Kwa hiyo, tuuliza maswali hivyo.

Mheshimiwa Maryam Msabaha, swali la nyongeza.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Na mimi naomba nimuulize Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Ziwa Tanganyika kulikuwa na uharamia, wale wavuvi walikuwa wakivamiwa na maharamia kutoka nchi za jirani na kuwapokonya nyavu zao na hata mitumbwi yao. Je, Serikali imedhibiti vipi maharamia hawa katika Ziwa Tanganyika? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wavuvi wetu wa Ziwa Tanganyika na hata wavuvi katika Ziwa Victoria wamekuwa wakivamiwa na maharamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie kwamba Serikali imepata taarifa hizi na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimejipanga ipasavyo kuhakikisha wavuvi wetu wanalindwa ili waweze kufanya shughuli zao za uvuvi kama kawaida bila ya hofu yoyote.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Alhaji Bulembo swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Mimi naomba kwanza kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri mlioteuliwa kwenye Wizara hiyo lakini nina swali moja kuhusiana na swali la uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoka Mtwara mpaka kufika Singida kuna *butchery* za samaki kama 60, lakini ndani ya *butchery* zile za kuuza samaki wauzaji wa kupima ni Wahindi, wapokea pesa ni Wahindi. Wizara inasema nini kuwasaidia Watanzania ambao wanayo haki ya kufanya kazi hizo kuliko watu wa nje?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bulembo, hilo swali naomba ulilite kama swali la msingi maana linahusu ajira ya watu kwenye hii sekta maana sasa nitakuwa nawaweka Mawaziri kwenye wakati mgumu kidogo kujibu maswali kwa namna ambavyo tunataka maswali hayo yawe yamekamilika.

Kwa hiyo swali la msingi hilo litakuja, Waheshimiwa Mawaziri hapa mjipange kulijibu sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 113

Kutumia Chanzo cha Maji cha Mto Rufiji

MHE. HAWA M. CHAKOMA aliuliza:-

Kwa muda mrefu chanzo cha maji cha Ruvu Chini na Ruvu Juu kimekuwa chanzo pekee cha maji katika Mkoa wa Pwani. Lakini kimsingi chanzo hicho hakitoshelezi mahitaji na hivyo kushindwa kumaliza tatizo la maji.

Je, ni lini Serikali itatumia chanzo cha maji cha Mto Rufiji kuwapatia maji safi na salama wananchi hususan wa Wilaya ya Rufiji, Kibiti, Mkuranga na Kisarawe?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Kuanzia mwaka 2005 hadi 2007 Serikali ilifanya uchunguzi wa vyanzo 26 vya maji kwa ajili ya matumizi ya Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo kwa miaka 2025 hadi 2032. Uchunguzi huo ulibaini kuwa wakati ule vyanzo vya maji vya mto Ruvu na visima vya Kimbiji na Mpera vilikuwa vinatosha kwa matumizi ya Jiji la Dar es Salaam na maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Pwani hadi mwaka 2032. Chanzo cha maji cha Mto Rufiji hakikuchaguliwa wakati huo kwa sababu ilionekana gharama za kusafisha na kusafirisha maji kutoka Mto Rufiji hadi Dar es Salaam zilikuwa kubwa ukilinganisha na vyanzo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati uchunguzi huo unafanyika, Serikali ilifanya uchunguzi wa vyanzo mbadala kwa ajili ya miji ya Utete, Ikwiriri, Mkuranga na Kisarawe. Uchunguzi ulibaini kuwa miji hiyo inaweza kupata maji ya visima. Miradi mikubwa ya visima ilitekelezwa katika miji hiyo na kunufaisha wakazi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi mahitaji ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam pamoja na maeneo ya Mkoa wa Pwani hususan Wilaya za Rufiji, Kibiti, Mkuranga na Kisarawe, Serikali imeanza taratibu za kumwajiri mtaalam mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na utayarishaji wa vitabu kwa kutumia chanzo cha Mto Rufiji. Kazi hiyo inatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2018/2019. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, swali la nyongeza.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Nabu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi kuvunwa kwa maji ya Mto Rufiji ni pasi moja ndefu mpaka golini, na ushindi huo unanufaisha akinamama kutua ndoo kichwani. Sasa ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi kuanza kuyavuna maji haya ili kupoza kiu ya Mheshimiwa Rais ya kuwatua akinamama ndoo kichwani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa mradi huu hauna dalili ya kuanza leo wala kesho. Na kwa kuwa, mradi wa maji ya visima uliopo haukidhi mahitaji ya Wana Rufiji. Ni nini sasa kauli ya Serikali juu ya upatikanaji wa maji safi na salama ndani ya mita 400 kama ilivyo kwenye sera? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, kwa namna ya kipekee anavyowapigania wananchi wake wa Mkoa a Pwani na wananchi wa Rufuji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa Serikali kuutumia Mto Rufiji, nikubalianenae, kutumia Mto Rufiji kutaweza kuondoa tatizo kabisa la maji katika mji wa Rufiji, lakini kikubwa katika lengo na nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, inawapatia wananchi wake maji. Si maji tu, ni maji safi, salama na yenye kuwatosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lengo na mkakati wa Rais wetu ni kuwatua ndoo akinamama kichwani na kwa kuwa hii ni Serikali ya Hapa Kazi Tu, kazi ya kuhakikisha kwamba mtaalamu mshauri kwa ajili mya kufanya upembuzi yakinifu wa/ya Mto Rufiji imeshaanza katika utaratibu. Kwa

hiyo, subira yavuta heri, namuomba tusbiri kuhakikisha kwamba, tunatekeleza mradi ule wa Mto Rufiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili kuhusu suala zima la kuondoa tatizo la majni katika Mji wa Rufiji; ikumbukwe katika Bunge lako Tukufu katika Mji wa Rufiji tumetenga kiasi cha shilingi milioni 630,977,000 kwa ajili ya kuondoa tatizo la maji kwa kipindi hiki wanasubiri katika suala zima la kutumia Mto Rufiji. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Tatizo la maji lililoko Mkoa wa Pwani linafanana kabisa na tatizo la maji lililopo Jimbo la Ngara ambapo tunapata maji kwa wiki mara moja au mara mbili. Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hili la maji katika Wilaya ya Ngara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Wizara yangu inatafuta mkandarasi mshauri ambaye ataanza kufanya *design* ya kutumia maji ya Mto Rubuvu kupeleka Ngara kwa sababu yale maji ni mengi kwa hiyo yatasambaa maeneo mengi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikwambie tu kwamba Serikali, Wizara yangu haijalala tayari inaangalia maeneo yote na kutumia vyanzo vilivyopo kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata maji safi na salama.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Willy Qambalo swali la nyongeza.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mradi wa maji wa Kijiji cha Getamog Wilayani Karatu, uliojengwa katika ule mpango wa Benki ya Dunia ambao uligharimu takribani shilingi milioni 600 haufanyi kazi

kwa sababu umejengwa chini ya kiwango. Nimshukuru Waziri wa Maji kwa kutuma wataalam wake ili kubaini tatizo hilo, ili mradi huo uweze kurekebishwa.

Je, ni lini Serikali sasa itapeleka fedha ili wananchi wa Kijiji cha Getambo waendeleo kupata huduma hiyo muhimu? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nilipata hiyo taarifa na nikamuagiza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Arusha, ambaye ameenda kule kuangalia uchunguzi namna gani mradi ulijengwa chini ya kiwango. Taarifa hiyo ikishapatikana, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba Serikali itafanya maandalizi ya kuweka mkandarasi wa kuboresha ule mradi na fedha itatolewa baada ya kuleta hati za malipo.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Hongoli swali la nyongeza.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe lina vyanzo vingi sana vya maji, lakini vijiji vyake vingi havina maji. Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Kata za Ikuna, Ninga, Kichiwa, Kidegembye, Lupembe, Matembwe, Mtwango na Igongolwa? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumpongeza. Waheshimiwa Wabunge katika Halmashauri ambazo zimetumia fedha vizuri kwa bajeti ya mwaka 2016/2017 ni pamoja na Halmashauri ya Lupembe,

ilitumia fedha zote ambazo zilikuwa zimetengwa na tukawaongezea nyingine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi hiyo tutahakikisha tunatenga fedha zaidi, ili vijiji vingine vyote vilivyobaki vipate maji.

Na. 114

Hitaji la Nyumba za Askari Polisi – Jiji la Tanga

MHE. NURU A. BAFADHILI aliuliza:-

Askari Polisi wengi katika Jiji la Tanga wanaishi uraiiani ambapo ni kinyume cha maadili kutokana na ukosefu wa nyumba za kuishi katika kambi zao.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga upya nyumba za askari hao?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwajengea nyumba za ghorofa askari wa Kambi za Chumbageni, Mabawa na Madina Msambweni, ili ziweze kuwaweka askari wengi katika eneo moja, kama ilivyo *Kilwa Road* Dar es Salaam?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, lenye kipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uchakavu wa nyumba za kuishi askari katika Jiji la Tanga na maeneo mengine hapa nchini. Katika kukabiliana na tatizo la uchakavu na upungufu wa nyumba za kuishi askari polisi, Serikali ina mpango wa kujenga nyumba mpya katika Jiji la Tanga na maeneo mengine kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu wa kujenga nyumba za ghorofa kwa ajili ya makazi ya askari,

kama ilivyojenga nyumba za *Kilwa Road* Jijini Dar es Salaam, Ziwani kwa upande wa Zanzibar pamoja na Buyekela Mwanza kwa kuwa zina uwezo wa kuchukua familia nyingi katika eneo dogo la ardhi. Aidha, taratibu za ujenzi wa nyumba za kuishi askari polisi Jijini Tanga zitakapoanza wataalam watazingatia ushauri wa Mheshimiwa Mbunge.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nuru Bafadhili, swali la nyongeza.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, miundombinu ya vyoo hususan katika Kambi ya Polisi wanaoishi katika eneo la Msambweni Madina ni mibaya sana kiasi ambacho wenyewe wanaita ni *SACCOS*.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatengenezea vyoo vyao wakati wanasubiri utaratibu wa kujengewa hizo nyumba?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa askari wale wanatumia maji ambayo Serikali ndio inawalipia, lakini maji hayo hayo utakuta wenyewe hawayatunzi vizuri, utakuta maji yanamwagika na wanayaachia.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawekea mita kama walivyoweza kuwawekea LUKU?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mawili madogo ya nyongeza. Nikianza na lile la uchakavu, la vyoo, niseme tu kwamba naelekeza wafanye tathmini na nitawaambia watu wangu Wizarani ili tuweze kuangalia namna ambavyo tunaweza kusaidia kwa sababu hilo ni jambo ambalo linahitaji uharaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili la kuhusu maji kumwagika ni suala la miundombinu na ni suala la umakini katika utumiaji wa maji. Tutayaangalia yote pamoja, lakini la msingi sana ambalo linafaa kwa askari wetu ni upatikanaji wa maji wa kila wakati. Tumejaribu kwenye LUKU, maeneo mengi sana tumepata shida sana kwa sababu ya wakati fulani fedha ambazo zinatakiwa zilipie kuchelewa na hivyo kuwafanya askari walipe kwa fedha zao na baadae kuanza kuhangaika kupata fedha za kufidia. Kwa hiyo, tutayaangalia yote kwa pamoja, ili tuweze kuhakikisha kwamba, tunatunza maji ili askari wapate maji kwa kila wakati. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Grace Kiwelu swali la nyongeza.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wanaoishi uraiani huwa wanapewa shilingi 40,000 kwa ajili ya pango. Shilingi 40,000 hii ni kwa ajili ya *room* moja, maji, umeme na familia hizi wana watoto.

Je, Serikali haioni umuhimu a kuongeza kiasi hiki cha fedha, ili askari wetu wanaporudi kupumzika nyumbani waweze kupumzika vizuri bila kelele za watoto?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Grace kwa swali alilolileta. Niseme tu jambo alilolisemea ni kilio cha askari na hata nilipozunguka maeneoe mengi nimekutanacho na Mheshimiwa Rais tayari alishatuelekeza tufanye upya uchambuzi wa masuala mengi yanayohusu stahiki za askari pamoja na sheria zinazo-*govern* utaratibu mzima wa taasisi hizi za majeshi yaliyoko ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani na hiyo ni moja ya kitu ambacho tutakiangalia yakiwepo na

mengine ambayo yanashusha morali ya kazi ya askari wetu.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, swali la nyongeza.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa pale kwenye Mji wetu wa Musoma tatizo la nyumba za polisi limekuwa ni tatizo kubwa na kwa muda mrefu. Na ninakumbuka kuanzia mwaka 2006 nimekuwa nikipiga kelele hapa Bungeni na bahati nzuri Serikali yetu sikivu ikakubali na ikaanza kujenga pale jengo na kufikia mwaka 2014 likawa limekamilika zaidi ya asilimia 85, lakini cha ajabu Serikali imeshindwa kutoa fedha za kulimalizia, matokeo yake wameanza kuiba milango, masinki na vitu vingine.

Je, Serikali sasa ni lini itatoa fedha ili ujenzi huu uweze kumalizika na wale askari waweze kuihsia vizuri?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru babu yangu Mheshimiwa Veda Mathayo kwa swali lake alilolileta. Nilishafika kwenye jengo hilo analoliongelea na kwa kweli limeshakamilika kwa kiwango kikubwa. Na sisi kama Wizara tunajipanga kuhakikisha kwamba, katika mwaka wa fedha huu fedha zitakazopatikana na ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo ambayo yameshafikia hatua nzuri, likiwepo hilo pamoja na maeneo mengine yanakamilishwa.

Kwa hiyo, punde fedha zitakapopatikana tutatoa kipaumbele kwa majengo haya ambayo yameshafikia hatua

nzuri, ili yaweze kukamilishwa na askari waweze kuhamia.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Munira swali la nyongeza.

MHE. MUNIRA MUSTAFA KHATIBU: Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri swali moja dogo tu. Mheshimiwa Waziri nyumba zilizopo ndani ya Mkoa wa Kusini Pemba, hasa Wilaya ya Mkoani ni chakavu sana. Je, Serikali ina mkakati gani kukarabati nyumba hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuleta swali hili. Ni kweli, hata mazingira ya kazi tu katika Mkoa wa Pemba ni magumu sana kufuatana na uchache wa nyumba za askari. Jambo hili Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilipigia sana akiwemo Balozi wa Askari, Mheshimiwa Faida Bakar.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, kama ambavyo nimesemea katika maeneo mengine ambayo yana hali tete za makazi ya askari, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ambaye nay eye amekuwa akifuatilia sana masuala ya askari, yakiwemo nyumba pamoja na haki zao nyingine yakiwemo madai kwamba, tutatoa kipaumbele kwa ajili ya nyumba hizo kwa sababu, mazingira ya kazi yanakuwa magumu pale askari wanapokosa makazi bora ya kukaa.

Na. 115

Kupeleka Umeme wa REA Katika Vijiji 47 Vilivyosalia Morogoro Kusini Mashariki

MHE. OMARY T. MGUMBA aliuliza:-

Vijiji 17 pekee kati ya vijiji 64 ndivyo vilivyopata umeme katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki na ni vijiji saba tu

vya Ludewa, Mtego wa Simba, Kidugaro, Lung'ala, Mangala na Kinonko vilivyo katika orodha ya kupatiwa umeme katika *REA III* awamu ya kwanza ya mwaka 2017/2018.

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vijiji 47 vilivyosalia?

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa vijiji 17 kati ya vijiji 64 ndio vilipatiwa umeme katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki. Vijiji vingine saba vitapatiwa umeme katika mzunguko wa kwanza wa mpango wa tatu wa *REA* ulioanza hivi karibuni. Kampuni ya *State Grid* ya Tanzania ambayo ndio mkandarasi wa eneo hilo tayari ameshaanza kazi katika vijiji hivyo saba ambavyo tumeviongeza. Katika eneo hilo kazi inajumuisha ujenzi wa njia ya kilometa 16.5 ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 pamoja na kilometa 16 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4. Kazi nyingine ni ufungaji wa *transformer* nane pamoja na kuunganisha wateja 256. Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 1.2 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vingine vilivyobaki vitapatiwa umeme katika mzunguko wa pili wa *REA* Awamu ya Tatu unaoendelea ambapo kwa pamoja utakamilika mwezi Julai, 2019 baada ya mzunguko kukamilika. Mradi huu utakamilika, kama nilivyosema mwaka 2020/2021.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Omary Mgumba swali la nyongeza.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kama Serikali ilivyosema katika jibu lake la msingi kwamba kuna vijiji saba ambavyo umeniongeza kwa hiyo, je, nataka kuvijua vijiji hivi saba ni vipi na ni lini vitaanza kupatiwa umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, katika Kata ya Mkulazi kuna miradi miwili nya kielelezo inayofanyiwa kazi sasahivi na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli, Kiwanda cha Mkulazi cha Sukari pia na ujenzi wa Bwawa la Kidunda, je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka umeme katika kata hii yenye vijiji vinne na Kijiji cha Kwaba, ambavyo ni vijiji vya Kwaba, Kidunda pamoja na Usungura?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Mgumba nakupongeza sana unavyoshughulikia masuala ya umeme katika Jimbo lako. Tulipokutana Morogoro ulituomba tukuongeze vijiji na tumekuongezea, lakini vijiji alivyotaka tumuogezee Mheshimiwa Mbunge pamoja na kwamba tumeshapeleka umeme katika vijiji vingine vikiwemo vijiji vya Mtego wa Simba pamoja na Kinonko, tunampelekea kwenye vijiji vingine ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, na vijiji ambavyo ameomba tumpelekee ni pamoja na Kibuko, Luhorole, Kizinga, Pangawe pamoja na Usungura. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikupe, kama vijiji ambavyo tumepeleka na vijiji vingine 40 tutakupeleka Mheshimiwa Mbunge, wala hakuna wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la pili kwamba ipo miradi ya vielelezo katika maeneo ya Usungura, ni kweli kabisa. Maeneo yale kutajengwa viwana vya sukari, lakini kadhalika kuna bwawa la maj. Kwa hiyo, tumemuongezea mbali na vijiji vingine vile 11 nilivyotaja na wala sio saba, tunaviongezea vijiji vingine vitatu vikijumlisha na Bwawa la Kidunda, ili tupeleke umeme Kidunda, Usungura

pamoja na Kwaba. Kwa hiyo, nimpe imani Mheshimiwa Mbunge kwamba vijiji vyote vya Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki vitapatwiwa umeme kupitia mradi wa tatu wa *REA*. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, hebu angalia hawa watu waliosimama hapo, halafu upate picha ya maswali ya kuhusu umeme, maana sasa wamesimama wengi hapa, hata sielewi nani aitwe nani asilitwe.

Mheshimiwa Lusinde, swali la nyongeza.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kupata fursa hii. Kama alivyouliza Mheshimiwa Mgumba, majimbo ya vijijini yana matatizo makubwa sana ya umeme hasa katika *center* za Kata ya Mpwayungu, Kata ya N'ninyi, Manzase na Makao Makuu ya Kata ya Muungano ambako hakuna umeme kabisa. Sasa je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika maeneo haya hususan katika Kata ya Muungano? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, ukiweza kuwajibu na wengine ili maeneo yao uwe umeyataja kabisa.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika Jimbo la Mtera tunapeleka umeme katika vijiji 21. Katika maeneo aliyoyataja kimsingi nimhakikishie Mheshimiwa Lusinde kwamba katika maeneo ya Manzese, Muungano, Mpwayungu pamoja na eneo ambalo hujalitaja linaitwa N'ninyi wanaanza Ijumaa inayokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumueleza Mheshimiwa Mbunge. Nichukue nafasi hii kwa sababu Waheshimiwa wengi wamesimama, kuwaeleza rasmi Waheshimiwa Wabunge kwamba kuanzia tarehe 20 mwezi huu wakandarasi wote katika mikoa 21 tuliyosaini mikataba wanaanza kazi rasmi ya ujenzi wa mradi wa *REA* Awamu ya Tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa miwili ya Katavi pamoja na Kigoma, taratibu tunazikalimisha wiki ijayo na mwanzoni mwa mwezi Desemba wanaanza ujenzi katika mikoa hiyo miwili. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge pamoja na kuwaambia *REA* namba tatu inanza kila mahali bado mmesimama? Mheshimiwa Hawa Bananga.

MHE. HAWA S. MWAIFUGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Tatizo lililopo Morogoro Kusini Mashariki ni tatizo ambalo linafanana na Jimbo la Tabora Manispaa katika Kata 11 za vijijini ambapo mpaka sasa hazijaanza kupelekewa umeme wa *REA III*. Je, ni lini Serikali itaanza utaratibu huo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwanza mkandarasi yupo Tabora na ameshakamilisha kazi ya *survey* na wiki iliyopita amekamilisha Igunga. Kwa hiyo, nimuambie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyosema tarehe 20 na bahati nzuri tunaanza kuwakagua ujenzi wa wakandarasi kuanzia Tabora na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mkandarasi atakuwa *site* kuanzia tarehe 20 baada ya kumaliza Igunga na ataendelea na ujenzi wa vijiji vyote 16 katika Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maftaha swali la nyongeza.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo hili la Morogoro Kusini linafanana kabisa na Jimbo la Mtwara Mjini ambako umeme unatoka pale lakini bado kuna vijiji vingi kwa

mfano Naulongo, Mkunjunguo, Namayanga na Mawala Chini kule kote mtandao wa umeme haujafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nimemweleza Mheshimiwa Waziri mara nyingi sana, je, yupo tayari hivi sasa kutoa kauli ya mwisho kwamba ni lini mtandao wa umeme utapita kwenye vijiji hivi nilivyovitaja? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati kuna Kijiji cha Mlala Chini nadhani hicho wakishapata umeme wataanza kulala vitandani hao. *(Kicheko)*

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama alivyosema, wiki mbili zilizopita nilikuwa Mtwara kushughulikia tatizo la umeme kukatika katika. Nilipita katika vijiji 16 na bahati nzuri vijiji vingine alivyosema Mheshimiwa Maftaha hivi leo mkandarasi yupo kule. Kwa hiyo, wakandarasi wameshaanza kazi Mheshimiwa Mbunge, asante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Wahehsimiwa Wabunge, natamani ningewataja wote hapo wenye maswali, namuona Mbunge wa Nyang'hwale kasimama mara nyingi, wa Hanang sasa hapa tafadhali Mheshimiwa Waziri majibu ya hawa watu waliosimama.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, maswali yetu kikanuni tumemaliza kwa Mheshimiwa Waziri kwa leo. Tunaendea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo sasa aulize swali lake.

Na. 116

Ubia wa Kiwanda cha Nguo cha Urafiki

MHE. SAED A. KUBENEA aliuliza:-

Serikali iliingia ubia na kampuni kutoka Jamhuri ya Watu wa China ya kumiliki na kuendesha Kiwanda cha Nguo

cha Urafiki kilichoko Ubungo Jijini Dar es Salaam lakini mbia huyo ameshindwa kutoa mtaji wa kuendesha kiwanda hicho.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kuwa mbia huyo anaweka mtaji wa kutosha wa kukiendesha kiwanda hicho?

(b) Je, kwa nini Serikali inafikia maamuzi ya kukibinafsisha kiwanda cha umma kwa mtu ambaye hana mtaji?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sued Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya Serikali ni kukiendeleza Kiwanda cha Urafiki ili kizalisje nguo na mavazi ya aina mbalimbali. Kutokana na mwekezaji aliyepo kutozalisha kwa ufanisi, mazungumzo ya wanahisa yalifanyika mwezi Machi, 2017 ambapo mbia mwenza, Kampuni ya *Changzhou State Owned Textile Assets Operations Limited* imeonesha kuwa tayari kumiliki kiwanda kwa kupunguza hisa zake kutoka 51 za sasa na kuipatia Tanzania hisa nyingi zaidi. Katika mpangilio huo mpya, tutakuwa na uwezo mkubwa wa maamuzi ikiwemo kusimamia kampuni kimkakati na kuweka mtaji wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Nguo cha Urafiki ni kiwanda cha kihistoria kilichoanzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa ushirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China mwaka 1966. Kutokana na historia ya kiwanda hicho wakati wa ubinafsishaji, Serikali ya Tanzania iliitaka Serikali ya China iliyotusaidia kujenga kiwanda hicho kutupa mbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya China ilikasimu ombi hilo kwa Jimbo la Liangsu ambalo ni bingwa katika sekta ya nguo. Serikali ikateua Kampuni ya *Dieqiu Textile Dyeng*

(DTD)na *Printing Group Company* ambayo haikufanya vizuri na ikaletwa Kampuni ya *Changzhou State Owned Textile Limited* tuliyonayo sasa. Kampuni hii nayo haifanyi vizuri hali iliyopelekea kushinikiza ongezeko la hisa za Serikali na mamlaka katika uendeshaji wa kiwanda kama nilivyoeleza hapo awali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Saed Kubenea swali la nyongeza.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwanza jina langu ni Saed Kubenea tofauti na Mheshimiwa Waziri alivyolitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kiwanda cha Urafiki kinaendeshwa kwa hasara kuanzia mwaka 1998 na kusababisha malimbikizo ya hasara yanayofikia shilingi bilioni 18.04 hadi tarehe 30 Juni, 2011. Na kwa kuwa mwekezaji aliyepita kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Hodhi la Taifa alichukua mkopo kwenye Benki ya Exim ya China unaofikia shilingi bilioni 56.1 na riba ya shilingi bilioni 4.04; na kwa kuwa Serikali imeamua kuwanyang'anya wafanyabiashara wazawa viwanda ambavyo walivinunua kutoka Serikalini kwa kushindwa kuviendesha. Je, Serikali iko tayari kumnyang'anya mbia huyu Kiwanda cha Nguo cha Urafiki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya Tanzania ilituma ujumbe China ambao uliongozwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Viwanda na Biashara, Shirika la Hodhi la Taifa na *FTC* kati ya tarehe 17 na 23 Desemba, 2011; na kwa kuwa ujumbe huu ndio uliopendekeza mwekezaji mpya kupewa kiwanda na kuhamisha hisa za Serikali kutoka asilimia 49 ambazo ilikuwa inamiliki. Je, Serikali iko tayari kuwawajibisha wafanyakazi hao wa umma waliotuletea mwekezaji *fake*? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Naibu Spika, hatunyang'anyi watu viwanda, hakuna mtu aliyebinafsishwa kiwanda atanyang'anywa, ila kama kiwanda kikikushinda nakushauri na nakuambia umpe jirani yako. Nimekuwa nikilisema ni kama tulivyolelewa sisi na nyanya zetu, ukiwa na nguo ikikubana usiichane, mpe mwenzio avae na viwanda hivi vitafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanda cha Urafiki nimesema ni kiwanda cha kihistoria, tulipobinafsisha viwanda, viwanda viwili vilikuwa na maneno na Mwalimu alivisemea, Mwalimu alipinga kubinafsisha Kiwanda cha Bora akasema gharama ya kubinafsisha Bora inazidiwa hata na bei ya *plot* pale *Pugu Road* wakampa majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, alipokuja kwa Urafiki akasema mwende kwa Wachina na katika jibu langu nimeeleza mlolongo tunaoufuata kupata *partner* mpya. *Partner* mpya sitaki kuendelea zaidi kwa sababu sasa tuna-*negotiate* na chini ya uongozi wa Kamati yangu ya Biashara unakwenda kupata *deal* nzuri, Kamati ya Viwanda na Biashara tumiliki zaidi na Mchina amekubali kutupa *percent* kubwa karibu *75 percent*. Kwa hiyo, tutakuwa na umiliki tutaweza kuamua kiwanda kiwanda kiende vipi, tutakujengea Urafiki nzuri Mheshimiwa Kubenea, nataka kuona watu 8,000 wanafanya kazi pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala la waliokwenda, hili suala limetolewa maamuzi na *CAG*. *CAG* aliyoyaona ukiyaona utalia Kubenea. Kwa hiyo, kila mtu ambaye alihusika katika kutuingiza kwenye dhahama hii rungu litamshukia kama mwewe. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khadija Nassir swali la nyongeza.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kumekuwa na malalamiko mengi juu ya mlolongo mrefu ambao hauna ulazima kwenye mchakato mzima wa uwekezaji ambao huwakatisha tamaa wawekezaji

wengi nchini. Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza kero hii kwa wawekezaji wetu? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anasema yalikuwepo malalamiko; yalikuwepo malalamiko wakati ule sasa hayapo. Yeyote anayetaka kuwekeza anione mimi, kama upo mkoani muone Mkuu wa Mkoa, kama uko Dar es Salaam nenda Ofisi yangu ya Dar es Salaam. Mkuu wa Mkoa amepewa mamlaka ya kukaribisha wawekezaji na Mheshimiwa Rais amesema mwekezaji atakayekwamishwa mkuu wa mamlaka awe Wilaya au Mkoa ajione hayupo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema Mheshimiwa Mbunge yalikuwepo, sasa yamekwisha. *(Makofi)*

Na. 117

Kupanda kwa Gharama za Pango Nyumba NHC

MHE. HALIMA A. BULEMBO aliuliza:-

Kumekuwa na upandaji holela wa gharama za pango kwa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kudhibiti upandaji holela wa pango ambao unaathiri wananchi wengi kutokana na kipato chao?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa linaendeshwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na miongozo ya Serikali. Aidha, masuala ya upingaji wa kodi huongozwa na Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 na sheria iliyoanzisha Shirika la Nyumba la Taifa Na. 2 ya mwaka 1990 kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2005. Sheria zote mbili zimeweka viwango ambavyo mmiliki wa nyumba ikiwemo Shirika la Nyumba la Taifa anapaswa kuzingatia katika ukadiraji wa kodi za pango. Miongoni mwa vigezo hivyo ni ukubwa wa nyumba, mahali nyumba ilipo, hali ya nyumba na kodi za Serikali zinazolipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kurekebisha viwango vya kodi ya nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa husimamiwa na bodi ya wakurugenzi ambayo imepewa mamlaka ya kisheria ya kusimamia kodi ya pango pamoja na kuidhinisha viwango vya kodi vitanavyotozwa kwa wapangaji wa nyumba za Shirika la Nyumba. Tangu mwaka 1990 shirika limefanya marekebisho ya kodi kwa miaka 6; 1994, 1999, 2001, 2005, 2007, 2008 na 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na marekebisho hayo, bado viwango vya kodi ya pango kwa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa ni kati ya asilimia 42 hadi 80 ya viwango vya soko. Kwa mfano, eneo la Masaki Shirika la Nyumba la Taifa hutoza kodi ya shilingi 1,700 kwa kila mita ya mraba wakati bei ya soko katika eneo hilo ni kati ya shilingi 12,000 hadi 30,000 kwa mita mraba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya mwisho Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Nyumba la Taifa iliidhinisha viwango vipya kwa kutoza kodi kwenye nyumba za shirika mwaka 2011 ambavyo ndivyo vinatumika mpaka sasa. Utaratibu wa kupandisha kodi kwa sasa hufanyika pale mkataba wa mpangaji unapomalizika na mpangaji kuomba kuhuisha mkataba wake. leleweke kuwa kodi zinapanda kwa mujibu wa sheria na pale mkataba wa mpangaji unapomaliza muda wake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima Bulembo swali la nyongeza.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya asilimia 56 mpaka 60 ya watanzania ni vijana lakini vijana wanashindwa kutimiza malengo yao ama ndoto zao kutokana na gharama kubwa ya upangaji wa nyumba za makazi hasa mijini kuwa kubwa na wamiliki kutaka kupewa kodi za mwaka au miezi sita.

Je, ni lini sasa Serikali itafuta utaratibu huu na sisi kama Bunge tutunge sheria itakayowalazimisha wamiliki wote kupokea kodi ya kila mwezi badala ya mwaka ama miezi sita kama ilivyo sasa? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze kwa kuona kwamba ipo haja ya kuona kwamba wapangaji wa nyumba wanakuwa na sheria ambayo inasimamia katika suala zima la upangaji. Naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge kwamba Wizara tayari imekwishaliona hilo na tayari tupo kwenye mchakato wa kuanzisha mamlaka itakayosimamia masuala yote ya nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sheria hiyo ambayo italetwa hapa Bungeni, tumeangalia suala zima la ukomo wa kutoa kodi za nyumba, hiyo ya miezi sita na mwaka mmoja haitakuwepo kwa sababu tumeona inaumiza watu wengi. Kwa hiyo, kodi itakuwa inalipwa kwa mwezi mmoja mmoja na wakati huo huo utatakiwa kuweka kama amana ya miezi mitatu kwa ajili ya shughuli ambazo zinaweza kuwa, kwa hiyo nimesikia na tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 118

Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi

MHE. KEMIREMBE J. LWOTA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Daraja la Kigongo Busisi utaanza?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kemirembe Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mradi wa ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi pamoja na barabara unganishi unatekelezwa katika hatua mbili. Hatua ya kwanza, ambayo tayari upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni. Upembuzi yakinifu ulikamilika tarehe 11 Julai, 2017. Aidha, kwa sasa Mhandisi Mshauri ambaye ni Kampuni ya *Cheil Engineering Ltd* kutoka Korea Kusini akishirikiana na *AFRISA Consultant* pamoja na Apex za Tanzania anaendelea na kazi ya usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni. Kazi ya usanifu wa kina zimepangwa kukamilika mwezi Julai, 2018 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni gharama halisi za ujenzi wa daraja zitafahamika. Baada ya gharama kufahamika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kemirembe Lwota swali la nyongeza.

MHE. KEMIREMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa daraja hili na kuagiza lijengwe haraka iwezekanavyo. Pamoja na hayo, kumekuwa na tatizo kubwa sana ambalo linatengeneza usumbufu mkubwa sana kwa wananchi kutokana na ubovu wa meli zilizopo. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kurekebisha vyombo hivi wakati tunasubiri ujenzi huo wa daraja? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mara nyingi tumezungumza juu ya changamoto mbalimbali ambazo zinawapata wananchi ambao wanavuka kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu tunafuatilia sana matatizo ambayo yapo hapa kutokana na hivi vivuko vipo, najua vipo vivuko vikubwa vitatu lakini iko changamoto ambayo vikiharibika vinasababisha usumbufu mkubwa sana kwa wananchi wa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu matatizo haya pia yanachangiwa na wananchi wenyewe. Nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge tushirikiane kuwaomba sana wananchi katika maeneo haya hasa wavuvi, wanavua katika maeneo haya ya kivuko, matokeo yake zile nyavu zinaswa na vivuko hivi na mara nyingi inasababisha uharibifu wa vivuko hivi ambavyo vinafanya kazi pale. Kwa hiyo, niombe tu wananchi tushirikiane na tusimamie jambo hili ili wananchi wasije wakaendelea kuvua maeneo haya ya karibu ili vyombo hivi vifanye kazi kwa *efficiency*. Kwa hiyo, nasisitiza tu kwa upande wa wenzetu wa *TEMESA*, wasimamie vizuri wakati harakati za ujenzi wa kivuko zinaendelea. Baada ya ujenzi naamini kwamba usumbufu utakuwa umeisha lakini pia itachangia sana katika ukuaji wa uchumi wa maeneo hayo na Tanzania kwa ujumla.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tutamalizia maswali yaliyobaki, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, swali litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Cosato Chumi.

Na. 119

**Huduma ya Mawasiliano ya Simu za
Mkononi katika Kata za Jimbo la Same Magharibi**

MHE. COSATO D. CHUMI (K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. DAVID) aliliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu za mkononi katika kata za Jimbo la Same Magharibi hususani Kata za Msindo, Mshewa, Mhuzi, Vumari, Vuudee, Tae, Suji, Gavao, Saweni na Ruvu Jiungeni?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Kata za Vumari, Suji na Ruvu Jiungeni vitafikishiwa huduma ya mawasiliano kupitia utekelezaji wa mradi wa Kampuni ya Simu ya Viettel. Utekelezaji wa mradi chini ya Kampuni ya *Viettel* unapaswa kukamilika mwezi huu wa Novemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Vijiji vya Kata za Mhezi, Msindo, Mshewa, Vuudee, Tae, Gavao na Saweni vinafanyiwa tathmini na Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na vitaingizwa katika orodha ya miradi ya mfuko itakayotekelezwa kulingana na upatikanaji wa pesa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyongeza.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kwa kuwa Serikali imesema kwamba inafanya tathmini kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili kuingiza Vijiji vya Mhezi, Msindo, Mshewa, Vuudee, Tae, Gavao na Saweni lakini mara nyingi imejitokeza kwamba mfuko huu hauna fedha za kutosha kutekeleza miradi. Je, Serikali iko tayari kutafuta namna nyingine ili kuwezesha vijiji hivi vipate mawasiliano? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa tatizo la Same Magharibi linafanana kwa kiasi fulani na maeneo kadhaa ya Jimbo la Mafinga Mjini hasa katika Vijiji vya Kisada, Uolele, Bumilayinga na Maduma. Je, Serikali iko tayari kutia msisitizo ili Kampuni ya Viettel ambayo wanaendesha mtandao wa Halotel wakafunge mitambo ili kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kupata mawasiliano ya uhakika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vijiji vingi sana bado vinahitaji huduma ya mawasiliano. Takwimu zilizopo ni kwamba tuna jumla ya kata 3,381 na kati ya hizo ni kata 443 ambazo tayari zimekwishafikiwa na mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaofanywa kupitia Mfuko wa Mawasiliano ni kuangalia asilimia ngapi eneo husika halina huduma ya mawasiliano kwa kutumia *prediction map* kutoka makampuni ya simu ambayo yanatoa huduma za mawasiliano. Nimepokea maombi mengi sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao wamepita pale ofisini kwa ajili ya kutaka huduma za mawasiliano zifike kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitambue kupokea maombi kutoka kwa Mheshimiwa Cosato Chumi ambaye

alifika sana ofisini kwangu, Mheshimiwa Edwin Sannda, Mheshimiwa Venance Mwamoto wa Kilolo, Mheshimiwa Deo Ngalawa na Mheshimiwa Mwakibete wa Busokelo. Serikali inaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kwamba huduma ya mawasiliano inafika kwenye sehemu zote ambazo zinahitaji huduma ya mawasiliano kwa sababu sasa hivi mawasiliano ni nyenzo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia swali letu la mwisho, Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 120

Hitaji la Uwanja wa Ndege – Mkoa wa Singida

MHE. JESCA D. KISHOA aliuliza:-

Mkoa wa Singida kwa sasa ni mkoa wa kimkakati, hasa kufuatia kazi ya kuleta Makao Makuu Dodoma.

Je, ni lini Serikali itahakikisha mkoa huo unapata uwanja wa ndege hasa kutokana na umuhimu wake?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha uwanja wa ndege wa Singida. Kutokana na umuhimu huo, Serikali ya Awamu ya Tano tayari imechukua hatua za kuwezesha kuimarisha uwanja wa ndege wa Singida ambapo hadi kufikia mwezi Mei, 2017 imekamilisha upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kufanya ukarabati na

upanuzi wa uwanja huo kwa kiwango cha lami. Uwanja wa ndege wa Singida ni miongoni mwa viwanja 11 vya ndege vilivyopata ufadhili wa Benki ya Dunia katika hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa uboreshaji wa viwanja hivyo. Viwanja vingine ni *Lake Manyara*, Musoma, Iringa, Tanga, Songea, Kilwa Masoko, Lindi, Moshi, Njombe na Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina nilourejea hapo juu, Serikali imeanza kutafuta fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa viwanja hivyo ukiwemo uwanja wa ndege wa Singida. Mradi huo ukikamilika utawezesha kuruka na kutua ndege kubwa zenye uwezo wa kubeba takribani abiria 70. Aidha, kazi ya ukarabati na upanuzi zitahusisha ujenzi wa jengo la abiria, jengo la mawasiliano na kuongozea ndege, kituo cha hali ya hewa pamoja na miundombinu mingine. Utekelezaji wa mradi huu utaanza mara tu fedha za mradi huu zitakapopatikana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jesca Kishoa swali la nyongeza.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashindwa kuelewa wananchi wa Mkoa wa Singida tumeikosea nini Serikali hii. Toka miaka ya 1970 uwanja huu ulipojengwa, haujawahi kufanyiwa *maintenance* ya aina yoyote, uwanja ni pori, hauna *fence*, imefikia hatua wananchi wameanza kupima viwanja na kujenga nyumba zao. Nataka *commitment* ya Serikali *very seriously*, ni lini mnakwenda kujenga uwanja wa ndege Mkoa wa Singida? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa umeme wa upepo Singida umewashinda, treni inayokwenda Singida kwa sasa hivi imeshakufa, ujenzi wa vyuo vikuu Singida umeshawashinda, *airport* Singida imeshawashinda. Je, hii ndiyo fadhila mnayowalipa wananchi wa Mkoa wa Singida pamoja na wao kuwa *champions* kutoa kura kwa Chama cha Mapinduzi? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, utakubaliana na mimi kwamba kwa *commitment* hii Serikali iliyoifanya kwa ajili ya ujenzi wa viwanja mbalimbali kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kuonesha namna Serikali hii ilivyo *serious* kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa viwanja mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii tu kuwaonya wananchi ambao wanakwenda kujichukulia maeneo hayo na kujipimia viwanja, kwa sababu sio sahihi, wanavunja sheria na sheria itachukua nafasi yake. Kwa hiyo, waache uwanja huu wazi ili taratibu zikamilike tujenge uwanja huu, wananchi wa Singida na Watanzania kwa ujumla waweze kupata huduma kupitia uwanja huu.

Swali lake la pili, Serikali haijashindwa, kwa fedha ambazo ziko *committed* kwa viwanja vyote ambavyo tunaendelea kufanya matengenezo ni kuonesha Serikali ya Awamu ya Tano iko *serious*. Kuna fedha karibu shilingi trilioni moja imetumika kwa ajili ya marekebicho ya viwanja vikubwa na niwaalike Waheshimiwa Wabunge wanavyopita maeneo kama ya *KIA* waone matengenezo yanayoendelea, wanavyopita Dar es Salaam waone namna tunavyouboresha uwanja ule na maeneo mengine, wakienda Shinyanga waone shughuli zinavyoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba Serikali iko *serious*, hatujashindwa, tunaenda kutengeneza viwanja, tunakwenda kuwahudumia wananchi na Mheshimiwa Kishoa asiwe na wasiwasi.

Suala hili nimuombe tu awe mvumilivu kwa sababu wapo Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa Kingu, wamekuwa wakija kuulizia juu ya uwanja huu kuonesha namna Serikali ya Chama cha Mapinduzi imejipanga kisawasawa. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu. Nitaleta matangazo tuliyonayo, kama ifuatavyo:-

Tangazo la kwanza ni la wageni waliotufikia Bungeni leo. Tunaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, ni Mgeni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), aliyekuja kushuhudia uendeshaji wa shughuli za Bunge, huyu ni Ndugu Nelson Mbunde, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 132 wa Mheshimiwa Stella Ikupa, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Watu Wenye Ulemavu ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya ziara ya mafunzo. Kundi la kwanza ni viongozi kumi kutoka Taasisi ya Kijamii ya *Hope Delivery Foundation* inayojishughulisha na utetezi na utoaji elimu kwa jamii ya watu wenye ulemavu, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Ndugu Michael Silas, karibuni sana. Pia wapo wanafunzi 104 wa kidato cha tano na walimu sita wa shule ya sekondari ya Chamwino ya Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Hassan Masala ambao ni wachungaji kutoka Nachingwea, Mkoa wa Lind, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ambao ni wapigakura wake kutoka Ilemela, Mkoani Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 56 wa Mheshimiwa Antony Mavunde ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira) ambao ni wanafunzi wa chuo kikuu kutoka Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. Tunao pia wageni 15 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambaye ni Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni wanafunzi wanaosomea madini katika Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambao wamekuja kushuhudia uendeshaji wa shughuli za Bunge kutoka Kaliua, Mkoani Tabora, karibuni sana. Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni viongozi wa Kampuni ya Chai ya Kisigo iliyopo Mufindi, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. Tunao wageni pia waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi nane wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambao ni viongozi wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM), Tawi la UDOM kutoka Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Lucas Nkende ambaye ni Diwani wa Kata ya Mwamashele (CCM) kutoka Wilaya ya Kishapu, Mkoa wa Shinyanga, amekuja kushuhudia uendeshaji wa shughuli za Bunge, karibu sana Mheshimiwa Diwani. *(Makofi)*

Tunao pia wageni sita kutoka Mkoa wa Tanga ambao ni viongozi wa wanawake Kanisa la Anglikana, Dayosisi ya Tanga wakiongozwa na Ndugu Mary Kajembe, karibuni sana. Pia tunao pia wakazi wawili wa Mkoani Dodoma ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndiyo wageni waliotufikia asubuhi ya leo. Kabla hatujaendelea na ratiba, Mheshimiwa Alhaji Abdallah Bulembo alikuwa ameuliza swali kuhusu ajira katika maeneo ya kuuzia samaki. Kwa sababu jambo hili ni la Wizara mbili na limetokea wakati wa maswali hapa na niliagiza lipelekwe swali la msingi ili lije lijibiwe, baada ya kutafakari, jambo hili limeshawahi kuja tena hapa Bungeni. Nadhani ni fursa sasa kwa Wizara hizi mbili (Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara inayoshughulika na Ajira), kwa maana ya Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Antony Mavunde, mkae pamoja Wizara hizi mbili, mojawapo ije itoe taarifa hapa Bungeni kuhusu jambo hili.

Kwa hiyo, mkae na Mheshimiwa Mbunge na hayo ambayo ameshawahi kuyazungumza huko nyuma na

nadhani pengine hayajapatiwa ufumbuzi ndiyo maana hili jambo linarudia kila wakati. Kwa hiyo, Wizara hizi mbili zikae, mtakapokuwa tayari, nafikiri katika Bunge lijalo, Wizara mojawapo itaweza kutoa taarifa hapa Bungeni kuhusu jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa ujumbe hapa kwamba tunao wageni wengine ambao hawakuwekwa kwenye orodha ya wageni na hawa wako kwenye Jukwaa la Spika, huyu ni Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya na viongozi wengine aliambatana nao. Karibuni sana viongozi wetu ambao mnatusaidia kwenye hili eneo ambalo linatusumbua hapa nchini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tutaendelea. Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments) No. 5) Bill, 2017)*

Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2017 *(The Public Service Social Security Fund Bill, 2017)*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori wa Mwaka 2017 *(The Wildlife Conservation Bill, 2017)*

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Miswada hii imesomwa kwa Mara ya Kwanza, itapelekwa kwenye Kamati zinazohusika ili na sisi tuweze kushiriki katika utungaji wa sheria kwa maana ya kuisoma Miswada hii lakini pia kuweza kushiriki vikao vya Kamati kikamilifu. Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa Mwaka 2017 (*The Drug Control and Enforcement (Amendment) Bill, 2017*)

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

NAIBU SPIKA: Sasa nimuite Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa mwaka 2017 yaani (*The Drug Control and Enforcement (Amendment) Bill, 2017*) kama ulivyorekebisha kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho, sasa usomwe kwa Mara ya Pili na ya Tatu na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitisha Muswada huu kuwa sehemu ya sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu ndani ya Bunge hii. Nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kunitiua kuhudumu kwenye nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Walemavu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wa viwango ndani na nje

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ya Bunge letu na pia kwa maelekezo na miongozo anayotupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati nampongeza sana Naibu wangu, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri wanazozifanya na wamekuwa msaada mkubwa kwangu. Vilevile nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wengine wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais katika kushika nyadhifa mbalimbali, tunaamini tutatekeleza wajibu wetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze wewe binafsi na kwa dhati nimpongeze Mheshimiwa Spika na Wenyevitini wa Bunge kwa jinsi mnavyotekeleza majukumu ya Bunge kwa ufanisi na ushirikiano mkubwa na hasa katika Ofisi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwenyezi Mungu ambariki, aendelee kumpa hekima na busara katika kutusaidia kutekeleza majukumu ya Bunge. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Janeth Massaburi kwa kuteuliwa na Rais kushika wadhifa wa Ubunge na hatimaye kuapishwa. Namtakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndugu yangu George Masaju na Ndugu yangu Gerson Mdemu, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watumishi wote wa ofisi yao kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuhakikisha kwamba tunaweza kuleta Muswada huu mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini na watumishi wengine wote wa mamlaka hiyo. Wamekuwa wakifanya kazi nzuri na Watanzania wote wameiona. Kwa

nafasi ya pekee, niwashukuru wananchi wote kwa kuendelea kutupatia ushirikiano katika vita dhidi ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini. (*Makofi*)

Kwa namna ya pekee, naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI chini ya uongozi wa Kaimu Mwenyekiti, Ndugu yangu Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki lakini na Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa, Mbunge wa Viti Maalum na ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa mwaka 2017. Ushauri na maoni na mapendekezo ya Kamati hiyo vimetusaidia kuboresha Muswada huu na kama itakavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ambalo Serikali imelileta ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Marekebisho wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa Mwaka 2017, unapendekeza kufanya marekebisho ya baadhi ya vifungu vya sheria hiyo. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuboresha utekelezaji wa sheria na kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa kuitumia sheria hii na kuongeza masharti mapya kwa ajili ya kuiwezesha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, musuala muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na kuboresha tafsiri za baadhi ya maneno mbalimbali yanayotumika katika sheria; kubadilisha baadhi ya vifungu na kuvifuta na kuviandika upya; kuongeza vifungu vipya; kuweka vifungu vya kuharamisha baadhi ya vitendo; kuweka adhabu na adhabu za ukomo wa chini kwa baadhi ya vifungu; kuainisha vigezo vya kufuata wakati wa utoaji wa dhamana; kuweka vigezo vya uwezo wa Mahakama kusikiliza mashauri ya makosa mbalimbali chini ya sheria hii na kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria na kuingiza maneno mapya.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umeganyika katika Sehemu kuu mbili. Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaainisha masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la sheria inayopendekezwa na tamko la marekebisho ya sheria hii inayokusudiwa kufanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kupitia Muswada huu katika vifungu mbalimbali vya sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 1(3) kinarekebishwa kubainisha au kujumuisha njia nyingine za usafirishaji wa dawa za kulevya na kudhibiti raia au kampuni ya kigeni iliyo Zanzibar itakayotenda kosa Tanzania Bara. Lengo la marekebisho haya ni kupanua wigo wa udhibiti wa dawa za kulevya na kuzuia mianya kwa raia au kampuni ya kigeni iliyoko Zanzibar kutenda kosa chini ya sheria hii. Kifungu cha 2 kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri mpya za maneno na kufanya marekebisho ya baadhi ya tafsiri za maneno yaliyotumika kwenye sheria pamoja na kufuta maneno yanayojirudia katika baadhi ya tafsiri. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mkanganyiko uliojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hii. Aidha, marekebisho katika kifungu hiki yanalenga pia kuainisha mahakama zitakazoshughulikia makosa mbalimbali yanayotokana na kukiukwa kwa masharti yaliyomo katika sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 4(2) kinarekebishwa kuipa uwezo Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kushughulikia si tu makosa ya dawa za kulevya bali pia makosa mengine yenye uhusiano wa moja kwa moja na biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Pia kuipa Mamlaka uwezo wa kufanya uchunguzi wa sayansi jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, inapendekezwa pia kiongezwe kifungu kidogo kipya cha (5) ili kuiwezesha Mamlaka kuimarisha udhibiti, uchapishwaji na umiliki usio halali wa kemikali bashirifu ambazo huweza kutumika

kutengeneza dawa za kulevya. Marekebisho haya yanalenga kuweka mfumo mzuri wa mawasiliano kati ya Mamlaka na taasisi nyingine zinazojihusisha na usajili wa makampuni au utoaji wa vibali vya uingizaji wa kemikali bashirifu nchini. Pia kifungu kidogo cha (6) kinaongezwa kwa lengo la kuipa Mamlaka uwezo wa kutunga miongozo kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya kufungu cha (5).

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 7 kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) na kuipa Mamlaka nguvu au uwezo wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya kwa kupata taarifa muhimu kutoka vyanzo mbalimbali. Marekebisho haya pia yanaweka sharti kwamba itakuwa ni kosa kwa Mkuu wa Taasisi au mtu anayesimamia Taasisi au Ofisi ya Umma itakayoombwa taarifa na Mamlaka na kushindwa kutekeleza ombi hilo bila sababu ya msingi.

Kifungu cha 9 kinarekebishwa kwa lengo la kuweka utaratibu wa uteuzi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri inayomshauri Kamishna Jenerali katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, inapendekezwa kiongezwe kifungu kidogo kipya cha (6) ili kuonesha Kamati ya Ushauri itakaa mara ngapi kwa mwaka kwa vikao vyake vya kawaida na pia vya ziada pale itakapolazimu. Inapendekezwa pia kiongezwe kifungu kidogo cha (7) kwa lengo la kuweka utaratibu wa upatikanaji wa Katibu wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 14 kinatoa mamlaka kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini kutoa ruhusa au kibali kwa kampuni inayotaka kujihusisha au kudhibiti biashara ya dawa za kulevya ndani na nje ya nchi. Masharti haya yameonekana kuweka mwingiliano wa majukumu na taasisi nyingine zilizopo kisheria. Inapendekezwa kifungu cha 14 kifutwe na badala yake kiwekwe kifungu kipya kwa lengo la kuondoa mkanganyiko na muingiliano wa majukumu kati ya Mamlaka na taasisi nyingine zinazotoa vibali vya kuingiza kemikali na dawa nchini ambazo ni Mamlaka ya Chakula na Dawa nchini na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya kifungu kipyaa cha 14(1) yanalenga kuweka masharti yanayoainisha orodha ya dawa za kulevya na za saikrotopiki au kemikali bashirifu zilizoainishwa katika Jedwali la Kwanza na la Pili zilizo chini ya udhibiti wa sheria hii. Aidha, inapendekezwa katika kifungu kidogo cha (2) kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana kupitia Tangazo la Serikali kurekebisha Jedwali la Kwanza na la Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 15(1) kinarekebisha kwa kufuta kipengele (a) kwa kuwa tafsiri ya kosa la umiliki limejumuishwa kwenye tafsiri ya kosa la usafirishaji wa dawa za kulevya. Aidha, kipengele (b) na (c) kinabadilishwa na kusomeka kama vipengele (a) na (b). Pia kipengele (b) kama kilivyobadilishwa kinafutwa kuwekwa kipengele kipyaa kitakachotambua kuwa itakuwa ni kosa kusafirisha isivyo halali, kuchepusha na kujishughulisha isivyo halali na kemikali zinazotumika katika kutengeneza dawa za kulevya. Inapendekezwa pia kiongezwe kipengele kipyaa cha (c) kuweka katazo kwa kuwezesha au kusababisha mtu kusafirishwa nje ya nchi kwa minajili ya kuwekwa rehani ili kufanikisha biashara ya dawa za kulevya. Kipengele hiki pia kinaweka adhabu ya kifungu cha maisha kwa mtu atakayekiuka masharti ya kifungu hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kifungu kidogo cha (2) kinarekebisha kwa kuzuia mtu yeyote kujihusisha isivyo halali na kemikali zozote zinazotumika katika uzalishaji wa dawa za kulevya. Aidha, inapendekezwa kiongezwe kifungu kidogo cha cha (3) kuainisha makosa yatakayoshughulikiwa chini ya kifungu hiki kwa kigezo cha uzito au ujazo wa dawa za kulevya au kemikali husika atakazopatikana nazo mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kipyaa cha 15A kinaongezwa kwa lengo la kuzipatia mamlaka za chini ya Mamlaka ya kushughulikia makosa ya usafirishaji wa kiasi kidogo cha dawa za kulevya na kemikali bashirifu na hivyo kupunguza msongamano wa kesi katika Mahakama Kuu. Kwa sasa mashauri yote yanayohusiana na makosa ya dawa za kulevya yenye uzito unaozidi gramu mbili kwa dawa aina

ya *cocaine* na *heroin*; gramu 50 kwa bangi na kilo mbili kwa milungi hupelekwa Mahakama Kuu hali ambayo imefanya mashauri yenye uzito mdogo kurundikana Mahakama Kuu. Makosa chini ya kifungu cha 15 cha sheria hii yamefanywa kuwa makosa ya uhujumu uchumi baada ya marekebisho ya Sheria ya Uhujumu Uchumi inayolazimisha makosa ya dawa za kulevya yenye uzito mdogo kuwa sehemu ya makosa chini ya kifungu hicho na hivyo kupelekea mlundikano wa kesi Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 20(1) kinarekebisha kwa kufuta maneno ya kufunga kifungu yaani *closing phrase* na badala yake kuweka maneno mapya kwa lengo la kuweka adhabu ya ukomo wa chini na wa juu kwa faini na kifungu. Aidha, kifungu cha 20(2)(b) kinarekebisha kwa kuondoa utata uliopo ambao unaonyesha kifungu hicho kinatengeneza kosa badala ya kuainisha mazingira ya utendaji wa kosa katika aya za (a) na (b) kwa minajili ya utoaji wa adhabu kwa kutumia maneno *commits an offence* mwishoni mwa aya ya (b).

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 27 kinarekebisha kwa kuweka adhabu ya chini kama ilivyo kwenye vifungu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu cha 28(1) kinarekebisha kwa kufuta maneno; *"in accordance with"* ambayo hayaleti maana katika kifungu hicho. Pia inapendekezwa kufuta neno *"regulations"* na badala yake kuweka maneno ya *"any other written law"* kwa lengo la kukifanya kifungu hicho kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 29 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuongeza makosa yasiyostahili dhamana ambayo yatajumuisha makosa ya kumiliki mitambo ya kutengeneza dawa za kulevya; kufadhili biashara ya dawa za kulevya na kuwaingiza watoto kwenye biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Sambamba na marekebisho hayo, viwango vya

uzito vinavyostahili dhamana kwa aina na makosa mbalimbali ya dawa za kulevya vimependekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa mapendekezo haya ni kudhibiti ongezeko la wafanyabiashara wakubwa; kupunguza viwango vya utunzaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini mfano *cocaine* na *heroin* kwa kutohofia kuendelea kufanya biashara kwa sababu uwezekano wa kupata dhamana ni mkubwa kutokana na viwango vya uzito uliopo kwenye sheria kwa sasa kuwa ni vikubwa ambavyo ndivyo vigezo vya utoaji wa dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 31 kwa lengo la kuweka utaratibu utakaofuatwa na Mahakama katika kufikia maamuzi ya kumpeleka mraibu wa dawa za kulevya kupata tiba hospitali au kituo cha utoaji nafuu baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kutumia dawa za kulevya. Kwa sasa sheria inaitaka Mahakama yenyewe ifanye uchunguzi kuhusiana na umri, tabia, mwenendo na afya ya mwili na akili ya mraibu au mtuhumiwa badala ya kuweka hitaji la taarifa ya daktari na jinsi ya kuipata taarifa hiyo ili iweze kusaidia Mahakama kufikia uamuzi sahihi na wa haki.

Kifungu cha 32 kilivyo kwa sasa kinaonesha kuwa kinatumika tu kwa baadhi ya makosa lakini taratibu zilizowekwa kwenye kifungu hiki zinahusisha makosa yote yaliyoko kwenye sheria hii. Hivyo, inapendekezwa kifungu kidogo cha (1) kifanyiwe marekebisho ili kupanua wigo wa matumizi yake ambayo yatahusisha makosa mengine yanayohusiana na makosa ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, inapendekezwa kiongezwe kifungu kidogo cha (2) kinachoweka masharti kuwa Afisa Mamlaka anapotekeleza majukumu yake inapolazimu atashirikiana na taasisi nyingine ili kukamilisha uchunguzi wa makosa mengine yanayohusiana na makakosa ya dawa za kulevya. Inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu kidogo cha (6) kwa kufuta kipengele cha (c) na badala yake kukiandika upya kwa lengo

la kuwaongezea mamlaka maafisa wanaotekeleza majukumu yao chini ya sheria hii kuwa na uwezo wa kuzuia wakati wa upekuzi wa mali zinazodhanika kutumika katika kutenda kosa au kusaidia katika uchunguzi wa kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 34 kinarekebisha kwa kuhusisha adhabu inayotolewa chini ya sheria hii kwa kuweka kiwango cha chini cha adhabu kwa lengo la kuisaidia Mahakama kufikia maamuzi sahihi na ya haki wakati wa kutoa adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 36 kinarekebisha kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na badala yake kukiandika upya kwa lengo la kuongeza kemikali bashirifu katika taratibu za kuteketeza dawa za kulevya pamoja na kukiboresha ili kitekelezeke katika mazingira tofauti. Aidha, maneno ya ufunguzi yaani *opening phrase* katika kifungu kidogo cha (3) yanapendekezwa yafutwe na badala yake yaandikwe upya kwa lengo la kujumuisha kemikali bashirifu na kemikali zinazothibitishwa kuwa na madhara yatokanayo na dawa za kulevya kuwa ni miongoni mwa mali zitakoweza kukamatwa na kuzuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 38 kinapendekezwa kufanya marekebicho kwa kufuta kipengele cha (c) na badala yake kukiandika upya kwa lengo la kupanua wigo wa udhibiti wa vifaa vinavyotumika kutengeneza dawa za kulevya kwa kutambua kuwa ni kosa kuwa na mashine, vifaa na maabara zinazotumika kuzalisha dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kipya cha 40A kinaongezwa kwa lengo la kuweka masharti kwa maafisa wa Mamlaka kumiliki na kutumia silaha inapobidi. Msingi wa marekebicho haya unatokana na ukweli kwamba wafanyabiashara wa dawa za kulevya kutokana na guvu za kifedha walizonazo humiliki silaha na wakati mwingine silaha kubwa na kujiwekea kinga ya kiulinzi wakati wote, hivyo kufanya mazingira ya kiutendaji ya Mamlaka kuwa hatarishi wakati wa ukamataji. Mamlaka imekuwa ikitumia

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Jeshi la Polisi kwa ajili ya ulinzi wakati wa kufanya *operation* zake za ukamataji watuhumiwa. Wakati mwingine taarifa za upatikanaji hupatikana usiku na kuhitaji utekelezaji wa haraka hali ambayo hulazimu Maafisa wa Mamlaka ama kujitoa mhanga au kuhatarisha maisha yao kwa lengo la kuendelea kupambana na dawa za kulevya nchini.

Kifungu cha 45 kinapendekezwa kifutwe kutokana na sababu ya kuwa masharti ya kifungu hicho yamewekwa sehemu isiyohusiana na utaifishaji wa mali. Maudhui ya kifungu hiki yanahamishiwa katika kifungu kipya cha 49A katika Sehemu ya Tano ya sheria inahusiana na utaifishaji wa mali na mazalia ya uhalifu chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapendekezwa kifungu cha 48 kifanyiwe marekebisho kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kukiandika upya kwa lengo la kuweka utaratibu rafiki wakati wa kukamata, kupekua, kuzuia mali na vielelezo; kuchukua maelezo ya watuhumiwa na mashahidi na kupeleleza kesi za dawa za kulevya. Aidha, katika kuboresha utaratibu huo, inapendekezwa kifungu kidogo cha (2) kifanyiwe marekebisho kwa lengo la kuboresha na kurahisisha taratibu za ukusanyaji wa ushahidi kwa njia za kisasa ambazo ni pamoja na kurekodi maelezo kwa njia ya sauti na video kwa kutumia vifaa vingine vya kisasa vya kieletroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapendekezwa pia kuongeza kifungu kidogo cha (4) kinachoweka utaratibu wa utolewaji na upokeaji wa ushahidi uliokusanywa chini ya kifungu hiki mahakamani. Sambamba na marekebisho haya inapendekezwa kiongezwe kifungu kidogo cha (5) kinachoainisha aina mbalimbali za fomu kama zilivyotajwa katika Jedwali la Tatu la Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapendekezwa kiwekwe kifungu kipya cha 48A kinachoweka masharti katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuainisha utaratibu wa Mkemia wa Serikali kuandaa taarifa ya uchunguzi wa sampuli au vielelezo vya dawa za kulevya vilivyowasilishwa kwake kwa ajili ya uchunguzi na jinsi ya kurejesha taarifa za uchunguzi kwa

mwasilishaji wa sampuli/vielelezo mara baada ya uchunguzi kukamilika. Aidha, inapendekezwa kuweka kifungu kidogo cha (2) kinachoainisha utaratibu wa upokeaji Mahakamani taarifa za uchunguzi wa sampuli/vielelezo vya dawa za kulevya toka kwa Mkemia wa Serikali kama kielelezo na uzito utakaopewa taarifa hiyo kama ushahidi katika kesi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kichwa cha Sehemu ya Tano kinachoelezea utaifishaji wa mali zinazotokana au zilizotumika katika makosa ya usafirishaji haramu kinapendekezwa kufutwa na badala yake kuwekwa Kichwa Kipya kinachoelezea utaifishaji wa mali zinazotokana au zilizotumika katika kutenda kosa chini ya makosa yaliyoainishwa chini ya Sehemu ya Tatu. Lengo ni kutatua wigo wa kuhakikisha utaifishaji unafanyika kwa makosa yote yaliyoainishwa chini ya Sehemu ya Tatu badala ya makosa ya usafirishaji haramu peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 49(1) kinaongelea kuitafisha mali ya mshtakiwa pekee na ile ambayo ilipatikana kwa tarehe ya kutiwa hatiani au baada ya hapo. Athari yake ni kuwa kifungu hiki hakihusishi mali zilizopatikana kabla ya kutiwa hatiani kwa mtuhumiwa na zile za washirika wa mtuhumiwa katika biashara ya dawa za kulevya. Inapendekezwa kifungu kidogo cha (1) kifutwe na kuandikwa upya lengo likiwa ni kuhakikisha mali inayotaifishwa ni ile iliyopatikana kwa tarehe ambayo mtuhumiwa alishtakiwa na siyo tarehe ya kutiwa hatiani. Aidha, kifungu kidogo cha 3(a) kinaongelea tafsiri ya neno "*associate*" kujumisha mtu aliyehukumiwa chini ya kifungu hiki. Ukweli ni kwamba mtu hawezi kuhukumiwa chini ya kifungu hiki bali kwa makosa ya vifungu vilivyomo Sehemu ya Tatu. Inapendekezwa kifungu kidogo cha 3(a) kifutwe na kuandikwa upya kwa lengo la kuondoa mkanganyiko kwenye tafsiri ya neno "*associate*".

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 49(4) kinasema mali haitataifishwa endapo mali hiyo ilipatikana siyo zaidi ya miaka mitano tangu tarehe ya kushtakiwa kwa makosa ya msafirishaji haramu wa dawa za kulevya. Miaka MITANO

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

katika mazingira haya ni muda mfupi sana, inapendekezwa kufuta kifungu kidogo cha (4) na kukiandika upya kwa lengo la kuongeza muda wa kipindi cha kutaifisha mali kutoka miaka 5 - 10 nyuma tangu tarehe ya kushtakiwa. Sambamba na hayo, kifungu kidogo cha (5) kinachoongelea utaifishaji kwa uwezo wa Mamlaka kimewekwa kwenye kifungu ambacho kinahusisha utaifishaji kwa taratibu za Kimahakama (*Judicial Forfeiture*) na siyo kwa uwezo wa Mahakama (*Administrative Forfeiture*). Hivyo, inapendekezwa kifungu kidogo cha (5) kifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapendekezwa kuwekwa kifungu kipya cha 49A kwa lengo la kuweka masharti ya utaifishaji mali na mazalia ya uhalifu yatokanayo na makosa chini ya sheria hii kwa kutumia utaratibu wa kimahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 50 kinaweka zuio la kumiliki mali iliyopatikana isivyo halali. Hata hivyo, vifungu vidogo vya (2) na (3) vinarudia kuelezea utaratibu wa utaifishaji mali hizo utaratibu ambao umekwishaelezwa kwa ufasaha katika vifungu vya (1) na (4) vya kifungu cha 49 hivyo vifungu vidogo hivi viwili havina maana kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 51 kinaongelea utaratibu wa utaifishaji mali kwa njia ya kiutawala. Kifungu cha 51(2) kina makosa kwa kuongelea mtu aliyehukumiwa wakati kifungu hiki hakitatumika kwa utaifishaji wa kimahakama. Inapendekezwa kifungu kidogo cha (2) kifanyiwe marekebisho kwa kufuta baadhi ya maneno na kukiandika upya kwa lengo la kuondoa dhana ya utaifishaji wa mali kwa njia ya kimahakama na badala ya utaifishaji wa mali kwa njia ya kiutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, inapendekezwa kufutwa vifungu vya (4), (5) na (7) na kuviandika upya kwa lengo la kuainisha utaratibu utakaotumika wakati wa utaifishaji wa mali na mazalia ya uhalifu utokanao na bishara za dawa za kulevya. Inapendekezwa pia kuongeza kifungu kidogo cha (8) kwa lengo la kuweka utaratibu wa namna

ya kushughulikia mali na mazalia ya uhalifu kwa njia ya Kimahakama badala ya utaratibu wa njia ya kiutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 51A kinaongezwa kwa lengo la kumpa uwezo Kamishna Jenerali kudhikilia akaunti za watuhumiwa benki kwa muda ili kurahishisha, kuimarisha na kuboresha taratibu za uchunguzi na kuweka uhakiki wa fedha haramu kutoroshwa kwa urahisi au uchunguzi kutoharibiwa. Sheria ilivyo sasa haimpi uwezo Kamishna Jenerali kuweka zuio au kushikilia akaunti za benki za watuhumiwa wa dawa za kulevya. Hali hii huathiri utendaji wa Mamlaka kwa kuongeza mwanya wa watuhumiwa kutorosha au kuhamisha fedha kwa haraka wakati wa uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Utaifishaji Mali na Mazalia ya Uhalifu, Sura ya 256 kwa sasa inampa Inspekta Jenerali wa Polisi uwezo wa kuzuia akaunti ya mhalifu kwa siku saba katika kuchunguza mashauri ya mali na mazalia ya uhalifu. Kamishna Jenerali wa Mamlaka humtegemea Inspekta Jenerali wa Polisi au Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai kuweka zuio hilo. Utaratibu huu wa kumuomba Inspekta Jenerali wa Polisi au Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai kuweka zuio hilo kwa maandishi na hivyo mazingira hayo huweza kumsaidia mtuhumiwa kuhamisha fedha zake kwa haraka sana na hivyo kupoteza au kuvuruga ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 52 kinafutwa kwa kuwa maudhui ya kifungu hiki yameainishwa kwa kina katika Sheria ya Utaifishaji Mali, Sura ya 256 ambapo katika mazingira hayo sheria hiyo ndiyo itakayotumika katika utaifishaji mali zilizopatikana isivyo halali. Kifungu cha 53 kinafutwa na kuandikwa upya kwa lengo la kumpa mamlaka Kamishna Jenerali uwezo wa kutoa amri ya kutaifisha mali kwa njia ya kiutawala ili kuepusha uwezekano wa matumizi mabaya ya mamalaka hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki pia kinaainisha utaratibu utakaofuatwa wakati wa kukata rufaa kupinga maamuzi ya amri ya Kamishna Jenerali ya utaifishaji wa mali.

Sheria ilivyo sasa kifungu cha 53 kinaweka utaratibu mbadala wa utafishaji wa mali. Aidha, kifungu hicho kimeweka utaratibu wa kupinga maamuzi ya utafishaji mali (*Administrative Forfeiture*) kwa muathirika kukata rufaa ndani ya siku 30 Mahakama Kuu bila kuainisha utaratibu wa kufuatwa wakati wa kukata rufaa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spiak, kifungu cha 54 kinafanyiwa marekebisho kwa kufutwa na kuandikwa upya kifungu kidogo cha (1) kumpa mamlaka Kamishna Jenerali ya kutoa amri ya kusalimisha mali iliyotaifishwa badala ya kuacha mamlaka hiyo kwa Maafisa wa Mamlaka ili kuepusha uwezekano wa mamlaka hiyo kutumiwa vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 55 kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuandikwa upya kwa lengo la kuweka utaratibu mzuri wa kufanya makubaliano baina ya nchi yetu na nchi za nje chini ya sheria hii ya namna ya kusaidiana katika kutaifisha, kubaini au kukamata mali kwa minajili ya utafishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ilivyo kwa sasa kifungu cha 55 kinaweka utaratibu wa namna ya kufanya makubaliano baina ya nchi yetu na nchi za nje chini ya sheria katika kusaidiana katika kutaifisha, kubaini au kukamata mali kwa minajili ya utafishaji. Maudhui ya kifungu kidogo cha (1) yanaonekana kuwa na mkanganyiko kwani ukisoma kifungu kidogo cha (1)(a)(i) hakileti maana. Aidha, aya nyingine za (a)(ii) na (b)(ii) zinaongelea mali za watu wanaodhaniwa kufanya makosa chini ya sheria hii tu ikiwaacha watu ambao watakuwa wametenda makosa na kuhukumiwa chini ya sheria hii au sheria ya nchi nyingine. Aidha, aya ya (b)(i) inamuongelea mhalifu tu kuwa mali zake ndizo zinaweza kuhusishwa na utaratibu wa kukamatwa au kutaifishwa ikimuacha nje mshirika wake (*associate*). Upungufu huu unatoa mwanya kwa mhalifu kuhamishia mali zake zote kwa washirika wake ili kuziepusha na utaratibu wa utafishwaji na wao kuendelea kufurahia mali zilizopatikana kutokana na biashara ya dawa za kulevya bila mkono wa sheria kuwafikia.

Kifungu cha 65 kinafanyiwa marekebisho kwa kuipa Mamlaka uwezo wa kutoa mwelekeo (*directions*) kwa Taasisi za Serikali jinsi ya kutekeleza matakwa na masharti ya vifungu vya sheria hii tofauti na kusudio la kutoa uwezo wa kutoa maelekezo (*directives*) kwa Taasisi hizo ambao ulipaswa kuwa kwa Kamishna Jenerali. Kutokana na upungufu huu, kifungu hicho kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kumpa Kamishna Jenerali mamlaka ya kuweza kutoa maelekezo kwa taasisi mbalimbali wakati wa utekelezaji wa masharti ya vifungu vya sheria hii. Aidha, inapendekezwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) kitakachotambua kuwa ni kosa kwa mtu atakayeshindwa kutekeleza masharti ya kifungu hiki cha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yanapendekezwa kwenye Jedwali la Kwanza, la Pili na la Tatu kwa lengo la kuyaboresha majedwali hayo. Katika Jedwali la Kwanza na la Pili yanafutwa na kuandikwa upya kwa lengo la kuboresha orodha ya dawa za kulevya na kemikali bashirifu zitakazodhibitiwa chini ya sheria hii. Aidha, Jedwali la Tatu linafutwa na kuandikwa upya kwa lengo la kufanya masahihisho katika baadhi ya fomu, kuweka fomu mpya na kuweka tafsiri ya Kiswahili kwa baadhi ya fomu hizo zitakazotumika wakati wa utekelezaji wa sheria hii.

Baada ya maelezo hayo na kwa mara nyingine tena, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maelezo ya hoja kuhusu Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nchi wa mwaka 2017 (*The Drug Control and Enforcement (Amendment) Act 2017*) na naomba Bunge lako Tukufu liujadili na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na Mara ya Tatu ili hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi yetu ya Tanzania. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA
ZA KULEVYA, SURA YA 95 WA MWAKA 2017 (THE DRUG CONTROL AND
ENFORCEMENT (AMENDMENT) ACT 2017 - KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI**

ISSN O856 – 01001

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

SPECIAL BILL SUPPLEMENT

No. 9

31st October, 2017

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.9 Vol. 98
dated 31st October, 2017*

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

THE DRUG CONTROL AND ENFORCEMENT (AMENDMENT) ACT, 2017

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Section Title

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title

PART II
AMENDMENT OF VARIOUS PROVISIONS

2. Amendment of section 1
3. Amendment of section 2
4. Amendment of section 4
5. Amendment of section 7
6. Amendment of section 9
7. Repeal and replacement of section 14
8. Amendment of section 15
9. Addition of section 15A
10. Amendment of section 20
11. Amendment of section 27
12. Amendment of section 28
13. Amendment of section 29

14. Repeal and replacement of section 31
15. Amendment of section 32
16. Amendment of section 34
17. Amendment of section 36
18. Amendment of section 38
19. Addition of section 40A
20. Repeal of section 45
21. Amendment of section 47
22. Amendment of section 48
23. Addition of section 48A
24. Amendment of Part V
25. Amendment of section 49
26. Addition of section 49A
27. Repeal and replacement of section 50
28. Amendment of section 51
29. Addition of section 51A
30. Repeal of section 52
31. Repeal and replacement of section 53
32. Amendment of section 54
33. Amendment of section 55
34. Amendment of section 65
35. Amendment of the Schedules

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dodoma,
30th October, 2017

JOHN W. H. KIJAZI
Secretary to the Cabinet

A BILL
for

An Act to amend the Drug Control and Enforcement Act, 2017.

ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Short title **1.** This Act may be cited as the Drug Control and Enforcement (Amendment) Act 2017 and shall be read as one with the Drug Control and Enforcement Act herein after referred to as the "principal Act."
Cap.95

PART II
AMENDMENT OF VARIOUS PROVISIONS

Amendm
ent of
section 1 **2.** The principal Act is amended in section 1 (3):

 (a) by inserting the word "also" between the words "shall" and "apply" appearing in subsection (3);
 (b) by deleting the word " aircraft" appearing in paragraph (a) and substituting for it the words "any other conveyance";
 (c) in paragraph (b), by:
 (i) deleting subparagraph (i) and substituting for it the following:
 "(i) a citizen or a person who ordinarily resides in the United Republic;"

- (ii) deleting the word "ship" appearing in the first line of subparagraph (iv) and substituting for it the word "conveyance";
- (iii) deleting the word "ship" appearing in subparagraph (v) and substituting for it the word "conveyance".

Amendment of section 2

3. The principal Act is amended in section 2, by:

- (a) inserting in the appropriate alphabetical order the following new definitions:
 - "Convention State" means any state which is a signatory to the United Nations Convention Against Illicit Traffic in Narcotic Drugs and Psychotropic Substances, 1988, or any other related international conventions or protocol or other instrument amending it;
 - "khat plant" means a flowering green leaf plant of the family *celastraceae* which contains the alkaloid chemical compounds named cathinone and cathine;
 - "officer" means a person appointed or employed in accordance with section 8(1) or any other law enforcement officer under other laws of Tanzania enforcing or performing powers and duties under this Act;"
- (b) adding at the end of the definition of the term "cannabis plant" the words "containing tetrahydro-cannabinol";
- (c) deleting the definitions of the terms "chemical precursors" and "cannabis oil";
- (d) inserting the word "Control" between the words "Drugs" and "Council" appearing in the definition of the term "Council";
- (e) in the definition of the term "court"-
 - (i) by deleting paragraph (a) and substituting for it the following:
 - "(a) in respect of an offence for contravention of section 7, 11, 15A, 17, 18, 19, 20, 21, 22, 25, 34, 39, 42, 47, 51A, 54 and 65 means subordinate court";
 - (ii) by deleting paragraph (b) and renaming paragraph (c) as paragraph (b); and
 - (iii) in renamed paragraph (b), by inserting between the word "section" and figure "16", figure "15";
- (f) by deleting the definition of the term "precursor chemical" and substituting for it the following:
 - "precursor chemical" means a chemical used in the

process of manufacturing of narcotic drugs or psychotropic substance as defined in article 12 of the UN Convention Against illicit Trafficking of Narcotic Drugs and Psychotropic Substances, 1988 mentioned in table I and table II as set out in the Second Schedule to this Act;”.

- (g) in the definition of the term “trafficking”, by deleting the opening phrase and substituting for it the following:
“trafficking” means the importation, exportation, buying, sale, giving, supplying, storing, possession, production, manufacturing, conveyance, delivery or distribution, by any person of narcotic drug or psychotropic substance any substance represented or held out by that person to be a narcotic drug or psychotropic substance or making of any offer but shall not include-”

Amendment of section 4

4. The principal Act is amended in section 4(2), by:

- (a) deleting the words “on drug related matters” appearing in paragraph (f) and substituting for them the words “drug offences and other related offences”;
- (b) adding immediately after paragraph (m), the following:
“(n) conduct forensic investigation;”
- (c) adding immediately after subsection (4), the following:
“(5) For purposes of controlling drug, drug abuse and trafficking in drugs, diversion of precursor chemicals and controlled pharmaceuticals, any other authority vested with powers to issue permit or licence to deal or engage in drug, chemicals, precursor chemicals or substances with drug related effects, shall consult the Authority before issuing import or export permit, licence or certificate.
(6) The Authority may, by notice published in the *Gazette*, make rules prescribing procedures for implementation of subsection (5).”

Amendment of section 7

5. The principal Act is amended in section 7, by adding immediately after subsection (2) the following new subsection:

“(3) The Commissioner General may, in the course of performing duties under this Act and in accordance with other relevant laws, demand, access and obtain any information from public institutions including information collected or maintained by or on behalf of other

public institutions and such institution shall be obliged to provide information as may be required.

(4) Any institution which fails to comply with the requirements of this section commits an offence under this Act."

Amendment of section 9

6. The principal Act is amended in section 9, by:

(a) inserting immediately after the word "appoint" the words "the Chairman and such other" appearing in subsection (4);

(b) adding immediately after subsection (5) the following new subsections:

"(6) The Advisory Committee shall meet at least twice a year in regular sessions and whenever necessary, in special sessions.

(7) A representative from the Authority shall be the Secretary to the Committee."; and

(c) renumbering subsection (6) as subsection (8).

Repeal and replacement of section 14

7. The principal Act is amended by repealing section 14 and replacing for it the following:

"List of prohibited narcotic drugs, psychotropic substances or precursor chemicals shall be as set out in the First and Second Schedules to this Act.

(2) Subject to subsection (1), the Minister may, by notice published in the *Gazette*, amend the list set out in the First and Second Schedules."

psychotropic substances or precursor chemicals

Amendment of section

8. Section 15 of the principal Act is amended:

(a) in subsection (1), by:

15

- (i) deleting paragraph (a);
- (ii) renaming paragraphs (b) and (c) as paragraphs (a) and (b);
- (iii) deleting paragraph (b) as renamed and substituting for it the following:
 - “(b) traffics, diverts or illegally deals in any way with precursor chemicals, substances with drug related effects and substances used in the process of manufacturing of drugs;” and
- (b) by adding immediately after paragraph (b) the following new paragraph:
 - “(c) directly or indirectly facilitates or causes any other person to be used as bondage for the purposes of drug trafficking, commits an offence and upon conviction shall be sentenced to life imprisonment.”;
- (c) in subsection (2), by inserting the phrase “or substances used in the process of manufacturing of drugs” between the words “effects” and “commits”;
- (d) by adding immediately after subsection (2), the following:
 - “(3) For purposes of this section, a person commits an offence under subsection (1) if such person traffics-
 - (i) narcotic drugs, psychotropic substances weighing more than two hundred grams;
 - (ii) precursor chemicals or substance with drug related effect weighing more than 100 litres in liquid form or 100 kilogram in solid form, and
 - (iii) cannabis and or khat weighing more than fifty kilogram.”

Addition of section 15A

9. The principal Act is amended by adding immediately after section 15 the following new section:

15A.-(1) Any person who traffics in narcotic drugs, psychotropic substances or illegally deals or diverts precursor chemicals or substances with drug related effects or substances used in the process of manufacturing drugs of the quantity specified under this section, commits an offence and upon conviction shall be liable to imprisonment for a term of thirty years.

substances or
illegal dealing
or
diversion
of
precursor
chemicals
of less
amount

- (2) For purposes of this section, a person commits an offence under subsection (1) if such person traffics in –
- (a) narcotic drugs, psychotropic substances weighing two hundred grams or below;
 - (b) precursor chemicals or substance with drug related effect weighing 100 litres or below in liquid form, or 100 kilogram or below in solid form;
 - (c) cannabis or khat weighing not more than fifty kilogram."

Amendment of section 20

- 10.** Section 20 of the principal Act is amended-
- (a) by designating the contents of section 20 as subsection(1);
 - (b) in subsection (1), by deleting the closing phrase and substituting for it the following:
"commits an offence and upon conviction shall be sentenced to a fine of not less than fifty million shillings or to imprisonment of not less than thirty years or to both";
 - (c) in subsection (2), by deleting the phrase "commits an offence and upon conviction shall be liable" and substituting for it the following:
"upon conviction shall be sentenced";

Amendment of section 27

- 11.** The principal Act is amended is section 27 by deleting the phrase "not more than twenty million shillings or to imprisonment for a term of not more than thirty" and substituting for it the phrase "not less than five million shillings but not exceeding fifty million shillings or to imprisonment for a term of not less than five years and not exceeding thirty".

Amendment of section 28

- 12.** The principal Act is amended in section 28, by:
- (a) deleting the words "in accordance with" appearing in the seventh line; and
 - (b) deleting the word "Regulations" appearing in the eighth line and substituting for it the words "any other written law".

Amendment of section 29

- 13.** Section 29 of the principal Act is amended-
- (a) in subsection (1), by:
 - (i) deleting the words "two hundred" appearing in paragraph (a) and substituting for them the word "twenty";
 - (ii) deleting the words "one hundred" appearing in paragraph (b) and substituting for them the word "twenty";
 - (iii) deleting paragraph (c) and substituting for it the following:
 - "(c) that accused person is charged of an offence relating to precursor chemical, other substances proved to have drug related effect or substances used in the process of manufacturing drugs, thirty litres in liquid form and thirty kilograms in solid form or more" ;
 - (iv) adding immediately after paragraph (c) the following new paragraph:
 - "(d) a person is charged under the provisions of sections 16, 20 and 23."
 - (b) in subsection (2), by deleting the words "Government Chemist" and substituting for it the words "Government Analyst".

Repeal and replacement of section 31

- 14.** The principal Act is amended by repealing section 31 and substituting for it the following:

- "Release of certain addicts
- 31.**-(1) Where a person is convicted of an offence under section 18 and the court is satisfied that:
- (a) the person is a drug addict;
 - (b) the addiction resulted or caused or motivated him to commit the offence he is charged with;
 - (c) the addiction can be medically treated within a reasonable time; and

(d) it is in the interest of justice notwithstanding anything contained in this Act or any other written law,

the court may record the finding, and instead of sentencing that person immediately to imprisonment, or such other sentence as it could otherwise pass, upon his consent, direct that he be released for detoxification or deaddiction to the hospital or an institution maintained or recognized by the Government.

(2) The court shall not make any findings under subsection (1) without receiving a written report from a medical expert providing relevant information to the court which shall include:

- (a) examination of the convicted person;
- (b) medical assessment regarding the presence and level of any addiction;
- (c) the nature and availability of any treatment;
- (d) the likelihood of successful treatment and time scales; and
- (e) any other information that the medical expert or the court considers relevant.

(3) In making a determination under subsection (1), it shall not be in the interests of justice to provide for medical treatment any convicted person in which any of the following aggravating features are present:

- (a) violence was used or threats;
- (b) weapon was used;
- (c) part of a gang or otherwise organized crime;
- (d) volume of drugs was more than consistent with personal use for an addict;
- (e) the convicted person had a role in the planning, controlling or facilitating others to commit offences; and
- (f) any other condition which the court deems fit to consider.

(4) The court shall give satisfactory reasons of the basis upon which the findings has been made under subsection (1).

(5) When a court makes determination under subsection (1), the court shall postpone the sentence of that person who shall enter into a bond in the form prescribed by the Authority, with or without sureties, for him to undertake the recommended medical treatment.

(6) In determining the length of time under subsection (5), the court shall award time not exceeding twelve months for completion of the treatment during which period of sentence shall be postponed and the bond extended.

(7) The court may, as it deems fit, order a medical report progress be provided in a period not exceeding three month intervals, and such report

shall contain assessment of the health condition of the convicted person, levels of cooperation and likely outcome.

(8) Before the expiry of twelve months, the convicted person shall appear before the court for consideration of whether or not to be released without further sanction or if the convicted person has failed to cooperate or otherwise has shown bad faith that calls for imposition of sentence for the original offence.

Amendment of section 32

15. Section 32 of the principal Act is amended-

(a) in subsection (1), by adding at the end of that subsection the following:

“and other related offences.”

(b) by adding immediately after subsection (1) the following new subsection:

“(2) The officers of the Authority shall, in exercising the powers under subsection (1) and where circumstances requires, consult and cooperate with other relevant authorities.”.

(c) by renumbering subsection (2) to (8) as subsections (3) to (9);

(d) in subsection (7) as renumbered, by deleting paragraph (c) and substituting for it the following:

- (c) Uzito wa dawa/kemikali hizo katika ujazo wa kilogramu/gramu/lita au mililita
- (d) Athari za dawa/kemikali hiyo endapo itatumiwa na binadamu au kutengeneza dawa za kulevya

Maoni mengine (kama yapo)

- 1. Kiasi cha pakiti/sanduku/magunia/kilo/lita (kiasi) zikiwa/yakiwa zimefungwa kwa lakiri kila moja ikiwa na saini yangu, zimerudishwa baada ya uchunguzi kwa (afisa aliyechukua vielelezo) leo tarehe/...../20.....

Aliyefanya uchunguzi:

Jina:.....

Saini:.....

Cheo:.....

Afisa anayethibitisha

Jina:.....

Saini:.....

Cheo:.....

Tarehe:.....

Dodoma,
....., 2017

JJM
MS-PMO (PPALEY AND D)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono kwa hivyo tutaendelea na utaratibu wetu. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga.

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni ya Kamati. Kabla ya kusoma maoni ya Kamati, Wajumbe wa Kamati kwa niaba yao pamoja na mimi mwenyewe tunapenda kutoa hongera kwa Wajumbe wenzetu ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika Wizara mbalimbali kama Naibu Mawaziri akiwemo aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambaye amekuwa Naibu Waziri, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Mheshimiwa Juliana Shonza ambaye amekuwa Naibu Waziri, Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ambaye amekuwa Naibu Waziri, Wizara ya Madini. Mwenyezi Mungu awabariki katika kutenda majukumu yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 wa mwaka 2017 *(The Drug Control and Enforcement (Amendment) Act 2017)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 wa mwaka 2017 *(The Drug Control and Enforcement (Amendment) Act 2017)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana kwa mara ya kwanza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu katika ukumbi wa Zahanati ya zamani Ofisi ya Bunge Mjini Dodoma

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mnamo tarehe 10 Novemba, 2017 ili kupokea maelezo kuhusu Muswada husika. Aidha, baada ya hapo, Kamati iliendelea kukutana na Maafisa wa Sheria kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamishna Jenerali na Maafisa Waandamizi kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini katika vikao mbalimbali vya Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo yake, Waziri husika alieleza Kamati kuwa Muswada huu unapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 ya mwaka 2015 kwa lengo la kuondoa upungufu ambao umebainika katika utekelezaji wa sheria hiyo. Miongoni mwa masuala yanayozingatiwa na mapendekezo ya marekebisho hayo ni pamoja na:-

(a) Kuongeza nguvu za mamlaka ya Mahakama na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya katika kushughulikia makosa mengine yanayoweza kutokea katika kutekeleza majukumu yake. Baadhi ya makosa hayo ni pamoja na utakatishaji fedha, kughushi na usafirishaji haramu wa watu.

(b) Kupanua wigo wa kudhibiti na hivyo kuipa Mamlaka nguvu ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya ili kuendana na wakati pamoja na kuongeza ufanisi katika kushughulikia watuhimiwa wa dawa za kulevya wafikishwapo Mahakamani.

(c) Kuainisha makosa mapya ili kuziba mianya iliyoachwa wazi bila kushughulikiwa na sheria katika kuifanya sheria kutekelezwa kwa ufanisi.

(d) Kumpa mamlaka Kamishna Jenerali kutoa maelekezo badala ya miongozo na kuainisha kuwa ukiukwaji wowote wa maelekezo yake ni kosa.

(e) Kujumuisha njia nyingine za usafirishaji kwa lengo la kupanua wigo wa udhibiti wa dawa za kulevya. Aidha,

tafsiri za maneno mbalimbali yaliyotumika kwenye sheria zimeongezwa pamoja na kufuta maneno yanayojirudia.

(f) Kufanya marekebisho ya Majedwali kwa lengo la kuboresha orodha ya dawa za kulevya kulingana na viwango vya Kimataifa.

(g) Kufanya marekebisho ya fomu mbalimbali na kuziboresha baadhi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa masharti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea maelezo ya Serikali, Kamati ilitoa mwaliko na matangazo katika tovuti ya Bunge ili kuwaalika wadau mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za kudumu z Bunge, Toleo la Januari, 2016. Hii ni pamoja na kuandikia barua za mwaliko baadhi ya wadau, taasisi husika watoe maoni yao kuhusu vifungu mbalimbali vinavyokusudiwa kurekebisha kwenye sheria hii kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, orodha ya wadau ambao waliandikiwa barua za mwaliko huo moja kwa moja kwa lengo la kutoa maoni yao mbele ya Kamati ni pamoja na *Tanzania Network of People Who Use Drugs, Tanganyika Law Society, Sober House* na Mtandao wa Watoa Msaada wa Sheria Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wadau kutoka *Sober House* waliofika mbele ya Kamati kutoa maoni yao pamoja na *Tanganyika Law Society* ambao waliwasilisha maoni yao kwa maandishi kupitia Sekretarieti ya Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kugusia masuala ya awali katika utangulizi wa taarifa hii, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati ambayo yametokana na uchambuzi wa Wajumbe wa Kamati katika Ibara mbalimbali za Muswada na ambao kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Serikali.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu maneno ya utangulizi kwa kuainisha jina la Muswada na Sheria inayohusika ambayo ni pamoja na masharti kuwa marekebisho yanayopendekezwa yatakuwa sehemu ya sheria husika kama ifuatavyo: *This Act may be cited as the Drug Control and Enforcement (Amendment) Act 2017 and shall be read as one with the Drug Control and Enforcement Act herein after referred to as the "principal Act."* Sehemu hii haikuwa na marekebisho ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu vifungu mbalimbali vya sheria husika vinavyopendekezwa kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa Ibara mbalimbali za Muswada, Ibara ya 2 ya Muswada inarekebisha kifungu cha 1(3) ili kuweka masharti kuwa sheria hii itatumika kwa raia au mtu anayeishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika kwenye sheria yameongezwa pamoja na kufuta maneno yanayojirudia. Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali kwa kuwa lengo la marekebisho hayo ni kuongeza wigo wa kudhibiti na kuziba mianya kwa raia au kampuni ya kigeni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 3 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 2 ambapo kinarekebisha kwa kuongeza tafsiri mpya ya maneno '*Convention State*', '*Khat Plant*' na '*Officer*' ili kurahisisha utekelezaji bora wa sheria hiyo. Aidha, kunapendekezwa marekebisho ya tafsiri na maneno mbalimbali na kuianisha Mahakama zinazoshughulikia makosa yaliyomo kwenye sheria. Kamati imebaini makosa ya kiuandishi katika Ibara ya 3(d) hivyo inapendekeza kufuta neno "*control*" linalojirudia. Aidha, kufanya masahihisho ya makosa madogo ya kiuandishi yaliyojitokeza katika Ibara hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 4 cha sheria hiyo kwa kuipa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za

Kulevya uwezo wa kudhibiti dawa za kulevya ikiwemo mamlaka ya kutunga Kanuni hii ni pamoja na:-

(a) Kurekebisha kifungu kidogo cha (2) kwa kuweka masharti yatakayoiwezesha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, kushughulikia makosa ya dawa za kulevya pamoja na makosa mengine yenye kuhusiana moja kwa moja na biashara na matumizi ya dawa za kulevya na kufanya uchunguzi wa sayansi jinai.

(b) Kuongeza kifungu kodogo kipya cha (5) ili kuiwezesha Mamlaka hiyo kuimarisha udhibiti wa uchepushwaji na umiliki usio halali wa kemikali bashirifu ambazo zinazoweza kutumika kutengenezea dawa za kulevya. Lengo ni kuweka mfumo mzuri wa mawasiliano kati ya Mamlaka na Taasisi nyingine zinazojihusisha na usajili au utoaji vibali vya uingizaji wa kemikali bashirifu nchini.

(c) Kifungu kidogo cha (6) kinaongezwa kuiwezesha Mamlaka kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya kifungu cha 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na maudhui ya marekebisho hayo kwa kuwa yanalenga kuongeza uwezo wa mamlaka kwa Mamlaka husika katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini katika kuimarisha ufanisi wa Mamlaka hiyo. Hata hivyo, Kamati inapendekeza kufanyike masahihisho ya makosa ya kiuandishi katika Ibara ya 4(b) ambapo aya ya (m) inayotajwa katika Muswada haipo katika sheria husika. Kwa hiyo, yapo makosa ya kupanga namba vizuri katika kifungu cha 4(2) cha sheria husika pamoja na kujirudia kwa aya za (c), (d), (e) na (f).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 7 kwa kumpa mamlaka Kamishna Jenerali kupata taarifa kutoka vyanzo mbalimbali. Aidha, taasisi ambazo zitashindwa kutoa taarifa husika bila sababu ya msingi zitakuwa zimetenda kosa la jinai kwa mujibu wa sheria hii. Kamati inakubaliana na

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

maudhui ya marekebisho husika kwa kuwa yanalenga kuainisha wajibu kisheria kwa taasisi husika katika kutoa ushirikiano kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Wajibu huo haukuwa wazi kisheria kabla ya mapendekezo ya marekebisho haya na hivyo kuwepo kwa changamoto za kukosa ushirikiano wa pamoja baina ya taasisi za Serikali za Mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati inapendekeza kufanyiike marekebisho katika Ibara ya 5(4) chenye kutoa sharti kuwa; *Any "Institution" which fails to comply with the requirements of this section commits an offence under this Act.* Maoni ya Kamati ni kuwa, kifungu kidogo hiki kirekebishwe kwa kuondoa neno *"Institution"* ili watajwe (*specifically*) watendaji husika wa taasisi husika ili kuondoa utata wakati wa utekelezaji wa kifungu hiki, vinginevyo Watendaji husika wa taasisi hizo watakwepa uwajibikaji kwa mujibu wa kifungu hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 9 kwa kuainisha kuwa uteuzi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri (*Advisory Committee*) utafanywa na Waziri na Katibu wa Kamati atakuwa mwakilishi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwenye Kamati hiyo. Pamoja na kuainisha vikao vya Kamati ya Ushauri ambapo itakutana mara mbili kwa mwaka kwa vikao vyake vya kawaida na inaweza kufanya vikao vya ziada pale itakapoona umuhimu wa kufanya hivyo. Kamati inakubaliana na mapendezo haya kwa kuwa yanalenga kuongeza uwazi na uwajibikaji miongoni mwa watendaji husika katika kufanya maamuzi ya kiutendaji kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 7 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 14(1) kwa kukifuta na kukiandika upya, dhamira ikiwa ni kuondoa mkanganyiko na mwingiliano wa majukumu na wa mamlaka nyingine zinazotoa vibali vya kuingiza dawa nchini ambazo ni Mamlaka ya Chakula na Dawa Nchini (*TFDA*) na Wakala

wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA). Lengo ni kuweka masharti yanayoainisha orodha ya dawa za kulevya na za kisaikotropiki au kemikali bashirifu zilizoainishwa katika Jedwali la Kwanza na la Pili chini ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu kidogo cha (2) kinarekebishwa kwa kuweka masharti yanayompa mamlaka Waziri mwenye dhamana kurekebisha Jedwali la Kwanza na la Pili; kuorodhesha dawa na kemikali bashirifu mpya zinazojitokeza na kuhitaji kudhibitiwa na kuainisha orodha ya dawa na kemikali hizo kulingana na mahitaji yatakayojitokeza pasipo kulazimika kuleta Muswada Bungeni kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa sheria hiyo. Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali kwa kuwa imezingatia ongezeko la matumizi mapya ya kemikali na dawa mbalimbali ambazo hazikutambuliwa na sheria hiyo lakini zimekuwa na athari kubwa kwa jamii hasa vijana kwa kuwa zina sifa ya kuwa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 8 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 15(1) kwa kufuta aya ya (a) kwa kuwa tafsiri ya kukutwa na dawa za kulevya imejumuishwa kwenye tafsiri ya kosa la usafirishaji wa dawa za kulevya. Hii ni pamoja na kuongeza masharti mapya kuhusu kosa la kusafirisha isivyo halali; kuchepusha na kujishughulisha isivyo halali na kemikali zinazotumika katika kutengeneza dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aya mpya ya (c) inaongezwa kuhusu kosa la kuwezesha au kusababisha mtu kusafirishwa nje ya nchi kwa minajili ya kuwekwa rehani ili kufanikisha biashara ya dawa ya kulevya. Hii ni pamoja na kuweka adhabu ya kifungu cha maisha kwa mtu anayepatikana na hatia chini ya kifungu hicho. Aidha, kifungu kidogo cha (2) kinarekebishwa kwa lengo la kumzuia mtu yeyote kujihusisha isivyo halali na kemikali zozote zinazotumika katika uzalishaji wa dawa za kulevya. Kifungu kidogo kipya cha (3) kinaongezwa chenye kuainisha makosa yatakayoshughulikiwa chini ya kifungu hicho kwa kutumia kigezo cha uzito au ujazo wa dawa za kulevya au kemikali

ambazo mtu atakazokutwa nazo. Kamati inakubaliana na maudhuhi ya marekebisho hayo kwa kuwa yanalenga kuziba mianya mbalimbali ambayo imekuwa ikitumiwa katika kukwepa mkono wa sheria kwa watuhumiwa wa madawa ya kulevya nchini kutokana na upungufu wa kisheria uliokuwepo chini ya sheria husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza kuanzishwa kwa kifungu kipya cha 15A kinachoweka masharti kuhusu kosa la kusafirisha kiasi kidogo cha dawa za kulevya. Lengo ni kuzipatia Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya mamlaka ya kusikiliza makosa ya usafirishaji kwa kiasi kidogo cha dawa za kulevya na kemikali bashirifu na hivyo kupunguza msongamano wa kesi Mahakama Kuu. Kamati inakubaliana na maudhui ya marekebisho hayo kwa kuwa yanalenga kuongeza wigo wa utoaji haki kwa haraka na kwa wakati katika mahakama mbalimbali kulingana na ukubwa kosa badala ya kutegemea Mahakama Kuu hali ambayo imekuwa ikikwamisha utekelezaji. Aidha, maudhui ya masharti katika kifungu kipya cha 15A yamelenga kutoa onyo au funzo kali katika kukomesha biashara ya dawa za kulevya hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho yafuatayo:-

(a) Kifungu cha 20(1) kinarekebishwa kwa kuongeza adhabu ya kosa la kutumia dawa za kulevya kutoka faini ya shilingi milioni 20 au kifungu kisichopungua miaka ishirini au vyote badala yake adhabu ya kosa hilo iwe faini isiyopungua shilingi milioni 50 au kifungu kisichozidi miaka thelathini au vyote.

(b) Kifungu kidogo cha 20(2)(b) kinafanyiwa marekebisho ya kiuandishi kwa kufuta maneno ' *commits an offence* ' ili kuondoa utata uliopo ambao unaonyesha kuwa kifungu hicho kinaweka masharti kuhusu kutenda kosa wakati kinaainisha mazingira ya utendaji kosa katika aya ya (a) na (b).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanalenga kuongeza adhabu kwa mtuhumiwa atakayetiwa hatiani kwa makosa yanayoainishwa katika kifungu hiki ili kutoa fundisho kwa jamii kutojikusisha na vitendo vya matumizi ya dawa za kulevya kwa mujibu wa masharti ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 27 ambapo adhabu ya kosa ambalo adhabu yake haijatajwa katika sheria hii iwe faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi shilingi milioni 50 au kifungu kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka thelathini. Kamati inakubaliana na marekebisho hayo kwa kuwa yameainisha vizuri ukubwa au udogo wa adhabu kulingana na ukubwa au udogo wa kosa husika ili kuhakikisha haki inatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 28(1) kuhusu masharti ya *burden of proof* kina marekebisho ya kiuandishi kwa kufuta maneno *'in accordance with' appearing in the seventh line na kufuta neno 'Regulations', appearing in the eighth line and substituting for it the words "any other written law"* kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 29 kwa kuongeza makosa yasiyostahili dhamana kujumuisha makosa makubwa ya kumiliki mitambo ya kutengenezea dawa za kulevya; kufadhili biashara ya dawa za kulevya na kuwaingiza watoto kwenye biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Aidha, inapendekezwa marekebisho ya viwango vya uzito vinavyostahili dhamana kwa aina na makosa mbalimbali ya dawa za kulevya ili kupunguza viwango vya utunzaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini kwa *cocaine* na *heroin*. Kamati inkubaliana na mapendekezao ya Serikali kwa kuwa dhamira ni kudhibiti usafirishaji na

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

usambazaji wa dawa za kulevya nchini kwa kuangalia upya na kupunguza kiwango cha uzito kama kigezo cha dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 31 ambacho kinafutwa na kuandikwa upya kwa kuweka vigezo na utaratibu mzuri utakaofutwa na Mahakama katika kuamua ama kutoa adhabu ya kifungo au kumpeleka mraibu wa dawa za kulevya kupata tiba katika hospitali au kituo cha utoaji nafuu baada ya kumtia hatiani. Hii ni pamoja na Mahakama kupata taarifa ya daktari ambayo itasaidia Mahakama kufikia uamuzi sahihi na wa haki. Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo kwa kuwa yanalenga kuisaidia Mahakama kama chombo pekee cha utoaji haki kufikia maamuzi yake kwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu wenye uthibitisho kuhusu hali ya mtuhumiwa wa matumizi ya dawa za kulevya kutoka kwa daktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 15 ya Muswada inafanya marekebisho katika kifungu cha 32(1) kwa kuwezesha Maaafisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kupanua wigo wa matumizi yake katika kutekeleza majukumu ya kukamata, kupekua na kutaifisha mali chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kidogo kipyua cha (2) kinaanzishwa kwa kuainisha kuwa wakati wa kutekeleza majukumu yao, Maaafisa wa Mamlaka watashauriana na mamlaka nyingine pale itapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu kidogo cha 6(c) kinafutwa na kuandikwa upya kwa kuweka masharti ya kuwezesha Maaafisa wa Mamlaka wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kuzuia kitu chochote kilichotumika kutenda kosa husika; kitu kinachoweza kutumika kama ushahidi na kitu chochote kinachohisiwa kuwa kinaweza kutumika kutenda kosa. Kamati inapendekeza kufanyiwe marekebisho ya kiuandishi kama ifuatavyo:-

(a) Katika Ibara ya 15(b); kuandika vizuri neno *exercising* ili lisomeke; *“The officers of the Authority shall, in exercising the powers under subsection (1) and where circumstances requires, consult and cooperate with other relevant authorities.”*

(b) Katika Ibara ya 15(d); Aya ya (c) inayopendekezwa kufutwa katika kifungu cha 32(7) haipo, hivyo aya ndogo (i), (ii) and (iii) hazina pa kusimama kwa kuwa hakuna aya (c) na hivyo kukosekana kwa muunganiko wa maneno na maudhui ya kifungu hiki kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 16 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 34 kwa kuweka masharti ya adhabu kwa mmiliki, mkazi au msimamizi wa ardhi, nyumba au eneo anayepatikana na hatia kwa kosa la kushindwa kutoa taarifa kuhusiana na mimea ya dawa za kulevya katika eneo husika kuwa ni faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi shilingi milioni 50 au kifungo kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka 30 au vyote kwa pamoja. Lengo la mapendekezo haya ni kuondoa maneno yanayojirudia na kupotosha maana ya kifungu hicho na pia kuhuisha adhabu inayotolewa kulingana na ukubwa wa kosa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapendekeza kufanya marekebisho madogo ya kiuandishi katika Ibara ya 16(a) ambapo maneno ya *“commits an offence, and upon conviction shall be information”* yanayopendekezwa kufutwa hayapo katika kifungu cha sheria husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 17 ya Muswada inafanya marekebisho katika kifungu cha 36(1) kwa kuifuta na kuandikwa upya ili kuongeza kemikali bashirifu na kemikali zinazoweza kutumika kutengenezea dawa za kulevya kuwa miongoni mwa dawa zitakazoteketezwa chini ya kifungu hicho. Hii ni pamoja na kuondoa masharti ya kuchapisha utekelezaji katika Gazeti la Serikali kutokana na wingi wa kesi za dawa za kulevya katika Mahakama mbalimbali nchini na zenye uzito mdogo.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Aidha, marekebisho yanafuta na kuandika upya maneno ya ufunguzi (*opening phrase*) katika kifungu cha 36(3) ili kujumuisha kemikali bashirifu na kemikali zilizohibitishwa kuwa na madhara yatokanayo na dawa za kulevya kuwa ni miongoni mwa mali zinazoweza kukamatwa na kuzuliwa chini ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 18 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 38(c) kwa kukifuta na kuandikwa upya kwa kuongeza mashine, vifaa, maabara zinazotumika kuzalisha dawa za kulevya kwa lengo la kupanua wigo wa udhibiti wa vifaa vilivyotumika kutengeneza au kuzalisha dawa za kulevya kuwa miongoni mwa orodha ya vifaa ambavyo mtuhumiwa anaweza kuchukuliwa kuwa ametenda kosa iwapo atakutwa navyo. Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo kwa kuwa yanalenga kuongeza wigo wa udhibiti na kupambana na biashara ya dawa za kulevya kuanzia hatua ya uzalishaji wake kwa kudhibiti mitambo, mashine au dhana mbalimbali za kuzalishia dawa hizo ambazo hazikuwa zimeainishwa katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 19 ya Muswada inapendekezwa kuanzishwa kifungu kipya cha 40A ili kuwezesha Maafisa wa Mamlaka kumiliki na kutumia silaha katika kutekeleza majukumu yao pale inapobidi. Hii ni pamoja na kuainisha masharti ya matumizi ya silaha hizo ili zitumike kwa mujibu wa matakwa ya sheria hiyo. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwa kuwa maudhui ya mapendekezo haya yanalenga kuwajengea uwezo Mamlaka katika kukabiliana na watuhumiwa wa dawa za kulevya ambao baadhi yao hutumia au humiliki silaha kali na hata kuzitumia au wanaotumia nguvu za ziada kuzuia utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara 20 ya Muswada inapendekeza kufuta kifungu cha 45 kwa kuwa kiliwekwa sehemu isiyohusiana na utaifishaji wa mali na kuhamishiwa katika kifungu kipya cha 49A ambacho kitaainisha maudhui na kilichokuwa kifungu cha 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 21 ya Muswada inarekebisha kifungu cha 47 kwa kuainisha kosa la kukiuka masharti ya kifungu hicho kwa lengo la kuweka mtiririko mzuri kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 48 katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kifungu cha 48(1) kinafutwa na kuandikwa upya kwa lengo la kuweka utaratibu rafiki wakati wa kukamata, kupekua, kuzuia mali za vielelezo, kuchukua malezo ya watuhumiwa na mashahidi na kupeleleza kesi za dawa za kulevya.

(b) Kifungu kidogo cha (2) kinarekebishwa ili kuwezesha uchukuaji wa maelezo ya watuhumiwa au mashahidi kwa njia za kisasa kama *recoder*, video na vifaa vya kidijitali.

(c) Kifungu kidogo kipya cha (4) kinaanzishwa ili kuweka utaratibu wa utoaji na upokeaji wa ushahidi uliokusanywa chini ya kifungu hiki Mahakamani.

(d) Kifungu kidogo kipya cha (5) kinaanzishwa ili kuainisha aina mbalimbali za fomu kama zilivyotajwa katika Jedwali la Tatu la sheria hii.

Kamati inapendekeza marekebisho hayo ya kiuandishi katika Ibara ya 22(b) ambapo maneno yanayopendekezwa yasomeke kama ifuatavyo; *By deleting the words "appearing in" and substituting for them the words "at the end of" in paragraph (aa) which will read as follows;*

"(i) in paragraph (a)(aa) by adding the words "unless he submits himself" at the end of sub-paragraph (1);"

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuainisha sehemu ambayo hayo maneno yanayopendekezwa yataingia ili kuleta maudhuhi ya kisheria yaliyokusudiwa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 23 inapendekeza kuanzishwa kifungu kipya cha 48A ili kuweka bayana utaratibu wa Mkemia Mkuu wa Serikali kupokea vielelezo vya madawa ya kulevya na kutoa ripoti ya uchunguzi huo. Pamoja na kukubaliana na maudhuhi ya marekebisho hayo, Kamati inashauri kuwa mamlaka husika ihakikishe kuwa mianya ya kuharibu ripoti za uchunguzi unaoainishwa chini ya kifungu hiki inazibwa na kudhibitiwa ili kuondoa mazingira ya kuwabambikizia watuhumiwa kesi kwa kutumia ripoti zilizogushiwa au kuharibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 24 ya Muswada inapendekeza kufuta kichwa cha Sehemu ya Tano ya sheria kwa kukibadilisha na maneno yafuatayo: *Part V, Forfeiture of Property Derived From or Used in Commission of An Offence Under Part III*". Marekebisho haya yanalenga kuainisha kichwa husika ili kiendane na maudhui yaliyomo katika sehemu husika kwa kuzingatia marekebisho yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 25 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 49 kama ifuatavyo:-

(a) Kifungu cha 49(1) kinafutwa na kuandikwa upya kwa kuweka masharti kuwa mali itakayotaifishwa itajumuisha mali iliyopatikana kwa tarehe ambayo mshtakiwa alishtakiwa na siyo tarehe ya kutiwa hatiani pamoja na mali ya washirika wake na hivyo kuweka utaratibu mzuri wa kutaifisha mali na mazalia ya uhalifu.

(b) Kifungu cha 49(4) kinafutwa na kuandikwa upya na kuongeza muda wa mali ya mtuhumiwa iliyotokana biashara ya dawa ya kulevya kwa muda wa miaka kumi iliyopita itataifishwa badala ya miaka mitano.

(c) Kifungu kidogo cha (5) kinachoipa Mamlaka uwezo wa kutaifisha mali kwa njia ya kiutawa kinafutwa kwa kuwa masharti hayo yapo sehemu kuhusu utafishaji wa kimahakama (*Judicial Forfeiture*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa masharti ya sheria hii yazingatiwe wakati Mamlaka ikitekeleza utafishaji wa mali kwa njia ya kiutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ibara ya 26 ya Muswada inapendekeza kuanzishwa kwa kifungu kipya cha 49A ambacho kinaweka utaratibu utakaotumika kuitaifisha mali iliyozuiliwa au kukamatwa au mali iliyotumika kutenda uhalifu.

Kamati inapendekeza marekebisho ya kiandishi yafanyike katika Ibara ya 26(4) neno 'apperars' liandikwe vizuri (appears) ili kuleta maana iliyokusudia na hivyo aya isomeke: *"Where the article of property is susceptible to decay, or it appears the sale of such article or property would be necessary for its proper management the court may order the sale of that article or property."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 27 ya Muswada inapendekeza kufuta kifungu cha 50 na kukiandika upya ambapo kifungu kipya kinatao katazo kwa mtu kukutwa na mali haramu kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda ningependa maoni yote ya Kamati yaingie kwenye *Hansard*.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 31 ya Muswada inapendekeza kufuta kifungu cha 53 na kuandikwa upya kwa kumpa Kamishna Jenerali mamlaka ya kutaifisha mali zilizohibitika kuwa zinatokana na biashara ya dawa za kulevya pamoja na masharti ya kuzingatiwa kabla ya kufikiwa maamuzi hayo.

Aidha, marekebisho yanatoa fursa kwa mtu yeyote ambaye hataridhishwa na tamko la kutaifisha mali husika kuomba mapitio katika Mahakama Kuu ndani ya siku 30. Kamati inakubaliana na mapendekezo haya kwa kuwa yanalenga kuziba mianya iliyokuwepo ambapo mtu

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

angeweza kutiwa hatiani lakini Serikali ikakosa nguvu kisheria katika kufuatilia na kudhibiti mali zinazotokana na biashara ya dawa za kulevya kwa sababu ya upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unapendekeza kufanyia marekebisho majedwali kwa lengo la kuboresha orodha ya dawa za kulevya kulingana na viwango vya kimataifa. Aidha, inapendekeza kufanya marekebisho ya fomu mbalimbali na kuziboresha baadhi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa masharti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapendekeza kuwa makosa madogo madogo ya kiuandishi yaliyobainishwa katika upangaji wa majedwali ya fomu husika yasahihishwe na kuandikwa vizuri ili maudhui yake yaendane na vifungu vya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha maoni ya jumla ya Kamati yanayotokana na tathmini ya maudhui ya Muswada huu kwa ujumla wake kama ifuatavyo:-

(a) Bila kuathiri matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka husika ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar zikae na kutafuta mbinu ya kudhibiti mianya ya kupenyeshwa dawa za kulevya kwa upande wa Tanzania Zanzibar kutokana na sheria hii kutumika upande mmoja wa Muungano yaani Tanzania Bara.

(b) Wakati wa kutunga kanuni za utekelezaji wa sheria hii, Serikali ione umuhimu wa kuongeza pombe aina ya viroba na dawa nyingine za binadamu ambazo zinaweza kutumiwa kama dawa za kulevya ili ziwe sehemu ya orodha ya dawa za kulevya kwa lengo la kudhibiti mbinu mpya za kuzalisha dawa mpya za kulevya hapa nchini.

(c) Mamlaka Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya ihakikishe inadhibiti taarifa/ripoti za uchunguzi unaoainishwa chini ya sheria hii kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuondoa mazingira ya kuwabambikia kesi

watuhumiwa kwa kutumia ripoti zilizogushiwa au kuharibiwa kabla ya kufikiwa na mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kukushukuru kwa kutoa kibali ili Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi iweze kuufanya kazi Muswada huu.

Aidha, nawashukuru wataalam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamishna Jenerali na Wanasheria wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Idara ya Mshauri Mkuu wa Sheria wa Bunge kwa kutoa ufafanuzi kwa Kamati katika maeneo mbalimbali ya Muswada. Maafisa hao walifanya kazi hiyo kwa weledi na kujituma kwa lengo la kuhakikisha Muswada huu unachambuliwa vizuri kabla ya kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususani Katibu wa Bunge Ndugu Stephen N. Kagaigai kwa uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Dickson M. Bisile na Makatibu wa Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndugu Asia Msangi, Ndugu Happiness Ndalu, Ndugu Stanslaus Kagisa, Ndugu Victor Leonard Mhagama na Msaidizi wa Kamati Ndugu Grace Mwenye, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO
YA SHERIA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA
KULEVYA (SURA YA 95), WA MWAKA 2017 (THE DRUG
CONTROL AND ENFORCEMENT (AMENDMENT) ACT, 2017
KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Sura ya 95), wa Mwaka 2017 (*The Drug Control and Enforcement (Amendment) Act, 2017*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana kwa mara ya kwanza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, katika Ukumbi wa Zahanati ya Zamani (Ofisi ya Bunge) Mjini Dodoma, mnamo tarehe 10 Novemba, 2017 ili kupokea maelezo kuhusu Muswada husika. Aidha, baada ya hapo Kamati iliendelea kukutana na Maafisa wa Sheria kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamishna Jenerali na Maafisa Waandamizi kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nchini katika vikao mbalimbali vya Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu.

Katika maelezo yake, Waziri husika alieleza Kamati kuwa Muswada huu unapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95**, ya Mwaka 2015, kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamebainika katika utekelezaji wa Sheria hiyo. **Miongoni mwa masuala yanayozingatiwa na Mapendekezo ya Marekebisho hayo ni pamoja na:-**

(a) Kuongeza Nguvu za Mamlaka ya mahakama na Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

katika kushughulikia makosa mengine yanayoweza kutokea katika kutekeleza majukumu yake. Baadhi ya Makosa hayo ni pamoja na utakatishaji fedha, kughushi na usafirishaji haramu wa watu.

(b) Kupanua wigo wa udhibiti na hivyo kuipa Mamlaka nguvu ya kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevya ili kuendana na wakati pamoja na kuongeza ufanisi katika kushughulikia watuhumiwa wa dawa za kulevya wafikishwapo mahakamani.

(c) Kuainisha makosa mapya ili kuziba mianya iliyoachwa wazi bila kushughulikiwa na Sheria katika kuifanya Sheria kutekelezwa kwa ufanisi.

(d) Kumpa mamlaka Kamishna Jenerali kutoa maelekezo badala ya miongozo na kuainisha kuwa ukiukaji wowote wa maelekezo yake ni kosa.

(e) Kujumuisha njia nyingine za usafirishaji kwa lengo la kupanua wigo wa udhibiti wa dawa za kulevya. Aidha, tafsiri za maneno mbalimbali yaliyotumika kwenye Sheria zimeongezwa pamoja na kufuta maneno yanayojirudia.

(f) Kufanya marekebisho ya Majedwali kwa lengo la kuboresha orodha ya dawa za kulevya kulingana na viwango vya kimataifa, na

(g) Kufanya marekebisho ya fomu mbalimbali na kuziboresha baadhi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa masharti yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maelezo ya Serikali, Kamati ilitoa mwaliko na matangazo katika Tovuti ya Bunge ili kuwaalika Wadau mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Hii ni pamoja na kuwaandikia barua za mwaliko baadhi ya Wadau (Taasisi husika) watoe maoni yao kuhusu vifungu mbalimbali vinavyokusudiwa kurekebishwa kwenye

Sheria hii kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimwa Spika, Orodha ya Wadau ambao waliandikiwa barua za mwaliko wa moja kwa moja kwa lengo la kutoa maoni yao mbele ya Kamati ni pamoja na :-

(a) Tanzania Network Of People Who use Drugs (TANPUD),

(b) Tanganyika Law Society (TLS),

(c) Sobber House, na

(d) Mtandao wa Watoa Msaada wa Sheria Tanzania (TANLAP).

Napenda kuwashukuru Wadau kutoka **Sobber House** waliofika mbele ya Kamati kutoa maoni yao pamoja na **Tanganyika Law Society** (TLS) ambao waliwasilisha maoni yao kwa maandishi kupitia Sekretarieti ya Kamati hii.

2.0 MAONI YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kugusia masuala ya awali katika utangulizi wa Taarifa hii, naomba sasa kuwasilisha Maoni ya Kamati ambayo yametokana na uchambuzi wa Wajumbe wa Kamati katika Ibara mbalimbali za Muswada na ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Serikali.

2.1 SEHEMU YA KWANZA YA MUSWADA:

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inahusu Maneno ya Utangulizi kwa kuainisha Jina la Muswada na Sheria inayohusika ambalo ni pamoja na masharti kuwa marekebisho yanayopendekezwa yatakuwa sehemu ya Sheria husika kama ifuatavyo:- *This Act may be cited as the Drug Control and Enforcement (Amendment) Act 2017 and shall be read as one with the Drug Control and Enforcement*

Act herein after referred to as the "principal Act." Sehemu hii haikuwa na marekebisho ya Kamati.

2.2 SEHEMU YA PILI YA MUSWADA:-

Sehemu hii inahusu vifungu mbalimbali vya Sheria husika vinavyopendekezwa kufanyiwa marekebisho.

2.2.1 UCHAMBUZI WA IBARA MBALIMBALI ZA MUSWADA:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 2 ya Muswada inarekebisha Kifungu cha 1(3) ili kuweka masharti kuwa sheria hii itatumika kwa raia au mtu anayeishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, tafsiri za maneno mbalimbali yaliyotumika kwenye Sheria zimeongezwa pamoja na kufuta maneno yanayojirudia.

Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwakuwa Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza uwigo wa udhibiti na kuziba mianya kwa raia au Kampuni ya kigeni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 2 kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri mpya ya maneno 'Convention State', 'Khat Plant' na 'Officer' ili kurahisisha utekekelezaji Bora wa Sheria hiyo. Aidha, kunapendekezwa marekebisho ya tafsiri za maneno mbalimbali na kuainisha Mahakama zinazoshughulikia makosa yaliyomo kwenye Sheria.

Kamati imebaini makosa ya kiuandishi katika Ibara ya 3(d) hivyo inapendekeza kufuta neno "Control" linalojirudia. Aidha, kufanywe masahihisho ya makosa madogo ya kiuandishi yaliyojitokeza katika Ibara hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 4 cha Sheria hiyo kwa kuipa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kulevya uwezo wa kudhibiti dawa za kulevya ikiwemo mamlaka ya kutunga Kanuni. Hii ni pamoja na:

(a) Kurekebisha kifungu kidogo cha (2) kwa kuweka masharti yatakayo iwezesha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kushughulikia makosa ya dawa za kulevya pamoja na makosa mengine yenye kuhusiana moja kwa moja na biashara na matumizi ya dawa za kulevya, na kufanya uchunguzi wa sayansi jinai.

(b) Kuongeza kifungu kidogo kipya cha (5) ili kuiwezesha Mamlaka hiyo kuimarisha udhibiti wa uchepushwaji na umiliki usio halali wa kemikali bashirifu ambazo zinazoweza kutumika kutengenezea dawa za kulevya. Lengo ni kuweka mfumo mzuri wa mawasiliano kati ya Mamlaka na taasisi nyingine zinazojihusisha na usajili au utoaji vibali vya uingizaji wa Kemikali bashirifu nchini, na

(c) Kifungu kidogo cha (6) kinaongezwa kuiwezesha Mamlaka kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya kifungu cha 5.

Kamati inakubaliana na maudhui ya marekebisho hayo kwakuwa yanalenga kuongeza uwezo wa Mamlaka kwa Mamlaka husika katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini katika kuimarisha ufanisi wa Mamlaka hiyo.

Hata hivyo, Kamati inapendekeza kufanyike masahihisho ya makosa ya kiuandishi katika Ibara ya 4(b): ambapo aya ya (m) inayotajwa katika Muswada haipo katika Sheria husika. Kwahiyo, yapo makosa ya kupanga namba vizuri katika kifungu cha 4(2) cha Sheria husika pamoja na kujirudia kwa aya za (c) (d) (e) na (f).

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika 7 kwa kumpa Mamlaka Kamishna Generali kupata taarifa kutoka vyanzo mbalimbali. Aidha, Taasisi ambazo zitashindwa kutoa taarifa

husika bila sababu ya msingi zitakuwa zimetenda kosa la jinai kwa mujibu wa Sheria hii.

Kamati inakubaliana na maudhui ya marekebisho husika kwakuwa yanalenga kuainisha wajibu kisheria kwa Taasisi husika katika kutoa ushirikiano kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Wajibu huo haukuwa wazi kisheria kabla ya mapendekezo ya marekebisho haya na hivyo kuwepo kwa changamoto ya kukosa ushirikiano wa pamoja baina ya taasisi za Serikali na Mamlaka husika.

Hata hivyo, Kamati inapendekeza kufanyike marekebisho katika Ibara ya 5(4) chenye kutoa sharti kuwa Any *"Institution"* which fails to comply with the requirements of this section commits an offence under this Act." Maoni ya Kamati ni kuwa, Kifungu kidogo hiki kirekebishwe kwa kuondoa Neno *"Institution"* ili watajwe (*specifically*) Watendaji husika wa Taasisi husika ili kuondoa utata wakati wa utekelezaji wa Kifungu hiki, vinginevyo Watendaji husika wa Taasisi hizo watakwepa uwajibikaji kwa mujibu wa kifungu hiki.

Ibara ya 6 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 9 kwa kuainisha kuwa uteuzi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri (*Advisory Committee*) utafanywa na Waziri na Katibu wa Kamati atakuwa Mwakilishi wa Mamlaka ya Dawa za Kulevya kwenye Kamati hiyo, pamoja na kuainisha vikao vya Kamati ya Ushauri ambapo itakutana mara mbili kwa mwaka kwa vikao vyake vya kawaida, na inaweza kufanya vikao vya ziada pale itakapoona umuhimu wa kufanya hivyo.

Kamati inakubaliana na mapendekezo haya kwakuwa yanalenga kuongeza uwazi na uwajibikaji miongoni mwa Watendaji husika katika kufanya maamuzi ya kiutendaji kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 7 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 14 (1) kwa kukifuta na kuandikwa upya, dhamira ikiwa ni kuondoa mkanganyiko na muingiliano wa majukumu na mamlaka nyingine zinazotoa vibali vya kuingiza dawa nchini ambazo ni Mamlaka ya Chakula na Dawa nchini (TFDA) na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA). Lengo ni kuweka masharti yanayoainisha Orodha ya dawa za kulevya na za kisaikotropiki au kemikali bashirifu zilizoainishwa katika Jedwali la kwanza na la Pili chini ya Sheria hiyo.

Aidha, Kifungu kidogo cha (2) kinarekebishwa kwa kuweka Masharti yanayompa mamlaka Waziri mwenye dhamana kurekebisha Jedwali la Kwanza na la Pili (kuorodhesha dawa na kemikali bashirifu mpya zinazojitokeza na kuhitaji kudhibitiwa na kuainisha orodha ya dawa na kemikali hizo) kulingana na mahitaji yatayojitokeza pasipo kulazimika kuleta Muswada bungeni kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa Sheria hiyo.

Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali kwakuwa imezingatia ongezeko la matumizi mapya ya kemikali na dawa mbalimbali ambazo hazikutambuliwa na Sheria hiyo lakini zimekuwa na athari kubwa kwa Jamii hasa vijana kwakuwa zina sifa ya kuwa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 15 (1) kwa kufuta aya ya (a) kwakuwa tafsiri ya kukutwa na dawa zakulevya imejumuishwa kwenye tafsiri ya kosa la usafirishaji wa dawa za kulevya. Hii ni pamoja na kuongeza Masharti mapya kuhusu kosa la kusafirisha isivyo halali, kuchepusha na kujishughulisha isivyo halali na Kemikali zinazotumika katika kutengeneza dawa za kulevya.

Aya mpya ya (c) inaongezwa kuhusu kosa la kuwezesha au kusababisha mtu kusafirishwa nje ya nchi kwa minajili ya kuwekwa rehani ili kufanikisha biashara ya dawa za kulevya. Hii ni pamoja kuweka adhabu ya kifungo cha

Maisha kwa mtu anayepatikana na hatia chini ya kifungu hicho.

Aidha, Kifungu kidogo cha (2) kinarekebishwa kwa lengo la kumzuia mtu yeyote kujihusisha isivyo halali na kemikali zozote zinazotumika katika uzalishaji wa dawa za kulevya, Kifungu kidogo kipya cha (3) kinaongezwa chenye kuainisha makosa yatakatayoshughulikiwa chini ya kifungu hicho kwa kutumia kigezo cha uzito au ujazo wa dawa za kulevya au kemikali ambazo mtu atakazo kutwa nazo. Kamati inakubaliana na maudhui ya Marekebisha haya kwakuwa yanalenga kuziba mianya mbalimbali ambayo imekuwa ikitumiwa katika kukwepa mkono wa sheria kwa watuhumiwa wa biashara ya dawa za kulevya nchini, kutokana na upungufu wa kisheria uliokuwepo chini ya sheria husika.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza kuanzishwa kwa Kifungu kipya cha 15A kinachoweka masharti kuhusu kosa la kusafirisha kiasi kidogo cha dawa za kulevya. Lengo ni kuzipatia Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya mamlaka ya kusikiliza makosa ya usafirishaji wa kiasi kidogo cha dawa za kulevya na kemikali bashirifu na hivyo kupunguza msongamano wa kesi Mahakama Kuu.

Kamati inakubaliana na maudhui ya marekebisha haya kwakuwa yanalenga kuongeza uwigo wa utoaji haki kwa haraka na kwa wakati katika Mahakama mbalimbali, kulingana na ukubwa wa kosa badala ya kutegemea Mahakamu Kuu, hali ambayo imekuwa ikikwamisha utekelezaji. Aidha, maudhui ya Masharti katika kifungu kipya cha 15A yamelenga kutoa onyo au funzo kali katika kukomesha biashara ya dawa za kulevya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisha yafuatayo:-

(a) Kifungu ch 20 (1) kinarekebishwa kwa kuongeza adhabu ya kosa la kutumia dawa za kulevya kutoka faini ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Shilingi Milioni 20 au kifungo kisichopungua miaka 20 au vyote, badala yake adhabu ya kosa hilo iwe Faini isiyopungua Milioni Hamsini au Kifungo kisichozidi Miaka 30 au vyote, na

(b) Kifungu kidogo cha 20 (2) (b) kinafanyiwa marekebisho ya kiuandishi kwa kufuta maneno "*commits an offence*" ili kuondoa utata uliopo ambao unaonesha kuwa kifungu hicho kinaweka masharti kuhusu kutenda kosa wakati kinaainisha mazingira ya utendaji kosa katika aya ya (a) na (b).

Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwakuwa yanalenga kuongeza adhabu kwa mtuhumiwa atakayetiwa hatia kwa makosa yanoyoainishwa katika kifungu hiki ili kutoa fundisho kwa jamii kutojijhusisha na vitendo vya matumizi ya dawa za kulevya kwa mujibu wa masharti ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 27 ambapo adhabu ya kosa ambalo adhabu yake hajitajwa katika sheria hiyo iwe faini isiyopungua shilingi Milioni Tano lakini isiyozidi milioni hamsini au kifungo kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka 30. Kamati inakubaliana na marekebisho haya kwakuwa yameainisha vizuri ukubwa au udogo wa adhabu kulingana na ukubwa au udogo wa kosa husika ili kuhakikisha haki inatendeka.

Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 28(1) kuhusu masharti ya "*Burden of Proof*" kina marekebisho ya kiuandishi kwa kufuta maneno "*in accordance with*" appearing in the seventh line; na kufuta maneno "*Regulations*" appearing in the eighth line and substituting for it the words "any other written law" kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 29 kwa kuongeza makosa yasiyostahili dhamana kujumuisha makosa makubwa ya kumiliki mitambo ya kutengeneza

dawa za kulevya, kufadhili biashara ya dawa za kulevya na kuwaingiza watoto kwenye biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Aidha, inapendekezwa marekebisho ya viwango vya uzito vinavyostahili dhamana kwa aina na makosa mbalimbali ya dawa za kulevya ili kupunguza viwango vya utunzaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini kwa *cocaine* na *heroin*. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwakuwa dhamira ni kudhibiti usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini kwa kuangalia upya na kupunguza kiwango cha uzito kama kigezo cha dhamana.

Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 31 ambacho kinafutwa na kuandikwa upya kwa kuweka vigezo na utaratibu mzuri utakaofuatwa na Mahakama katika kuamua ama kutoa adhabu ya kifungo au kumpeleka Mraibu wa dawa za kulevya kupata tiba katika hospitali au kituo cha utoaji nafuu baada ya kumtia hatiani. Hii ni pamoja na Mahakama kupata taarifa ya daktari ambayo itasaidia Mahakama kufikia uamuzi sahihi na wa haki. Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo kwakuwa yanalenga kuisaidia mahakama kama chombo pekee cha utoaji haki, kufikia maamuzi yake kwa kuzingatia ushauri wa kitaalam yenye uthibitisho kuhusu hali ya mtuhumiwa wa matumizi ya dawa za kulevya kutoka kwa Daktari.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 ya Muswada inafanya marekebisho katika Kifungu cha 32(1) kwa kuwezesha Maafisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kupanua wigo wa matumizi yake katika kutekeleza majukumu ya kukamata, kupekua na kutaifisha mali chini ya Sheria hii. Kifungu kidogo kipyua cha (2) kinaanzishwa kwa kuainisha kuwa wakati wa kutekeleza majukumu yao, Maafisa wa Mamlaka watashauriana na Mamlaka nyingine pale itakapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Aidha, Kifungu kidogo cha (6) (c) kinafutwa na kuandikwa upya kwa kuweka masharti yakuwawezesha

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Maafisa wa Mamlaka wakati wa utekelezaji wa Majukumu yao, kuzuia kitu chochote kilichotumika kutenda kosa husika, kitu kinachoweza kutumika kama ushahidi na kitu chochote kinachohisiwa kuwa kinaweza kutumika kutenda kosa.

Kamati inapendekeza kufanyike marekebisho ya kiuandishi kama ifuatavyo:-

(a) Katika Ibara ya 15(b):-Kuandika vizuri neno exercising ili lisomeke:- "The officers of the Authority shall, in exercising the powers under subsection (1) and where circumstances requires, consult and cooperate with other relevant authorities."

(b) Katika Ibara ya 15(d): Aya ya (c). inayopendekezwa kufutwa katika kifungu cha 32 (7) haipo, hivyo aya ndogo za Romani (i), (ii) and (iii) hazina pakusimama kwakuwa hakuna aya (c) na hivyo kukosekana kwa muunganiko wa maneno na maudhui ya kifungu hiki kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 16 ya Muswada inapendekeza Marekebisho katika Kifungu cha 34 kwa kuweka masharti ya adhabu kwa mmiliki, mkazi au msimamizi wa ardhi, nyumba au eneo anayepatikana na hatia kwa kosa la kushindwa kutoa taarifa kuhusiana na mimea ya dawa za kulevya katika eneo husika kuwa ni faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi shilingi milioni hamsini au kifungu kisichopungua miaka mitano lakini kisichozi miaka 30 au vyote kwa pamoja.

Lengo la mapendekezo haya ni kuondoa maneno yanayojirudia na kupotosha maana ya kifungu hicho na pia kuhuisha adhabu inayotolewa kulingana na ukubwa wa kosa husika.

Kamati inapendekeza kufanya marekebisho madogo ya kiuandishi katika Ibara ya 16(a): ambapo maneno ya "commits an offence, and upon conviction shall be information" yanayopendekezwa kufutwa hayapo katika Kifungu cha Sheria husika.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17 ya Muswada inafanya Marekebisho katika Kifungu cha 36(1) kwa kuifuta na kuandikwa upya il kuongeza kemikali bashirifu na kemikali zinazoweza kutumika kutengenezea dawa za kulevywa kuwa miongoni mwa dawa zitakazoteketezwa chini ya kifungu hicho. Hii ni pamoja na Kuondoa masharti ya kuchapisha uteketezaji katika Gazeti la Serikali kutokana na uwingi wa kesi za dawa za kulevywa katika mahakama mbalimbali nchini na zenye uzito mdogo. Aidha, Marekebisho yanafuta na kuandika upya maneno ya ufunguzi (*opening phrase*) katika kifungu cha 36(3) ili kujumuisha kemikali bashirifu na kemikali zilizohibitishwa kuwa na madhara yatokanayo na dawa za kulevywa kuwa ni miongoni mwa mali zinazoweza kukamatwa na kuzuiliwa chini ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 38 (c) kwa kukifuta na kuandikwa upya kwa kuongeza mashine, vifaa, maabara zinazotumika kuzalisha dawa za kulevywa kwa lengo la kupanua wigo wa udhibiti wa vifaa vinavyotumika kutengeneza au kuzalisha dawa za kulevywa kuwa miongoni mwa orodha ya vifaa ambavyo mtuhumiwa naweza kuchukuliwa kuwa ametenda kosa iwapo atakutwa navyo.

Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo kwakuwa yanalenga kuongeza uwigo wa udhibiti na kupambana na biashara ya Dawa za kulevywa kuanzia hatua ya uzalishaji wake kwa kudhibiti mitambo/mashine au zana mbalimbali za kuzalishia dawa hizo ambazo hazikuwa zimeainishwa katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 ya Muswada inapendekeza kuanzishwa Kifungu kipya cha 40A ili kuwezesha maafisa wa Mamlaka kumiliki na kutumia silaha, katika kutekeleza majukumu yao pale inapobidi. Hii ni pamoja na kuainisha masharti ya matumizi ya Silaha hizo ili zitumike kwa mujibu wa matakwa ya Sheria hiyo. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwakuwa Maudhui ya mapendekezo haya yanalenga kuwajengea uwezo Mamlaka katika kukabiliana na Watuhumiwa wa dawa za kulevywa

ambao baadhi yao hutumia au humiliki silaha kali na hata kuzitumia, au wanaotumia nguvu za ziada kuzuia utekelezaji wa Sheria hiyo.

Ibara ya 20 ya Muswada inapendekezeza kufuta kifungu cha 45 kwa kuwa kiliwekwa sehemu isiyohusiana na utaifishaji wa mali na kuhamishiwa katika kifungu kipya cha 49A ambacho kitaainisha maudhui ya kilichokuwa kifungu cha 45. Ibara ya 21 ya Muswada inarekebisha Kifungu cha 47 kwa kuainisha kosa la kukiuka masharti ya kifungu hicho kwa lengo la kuweka mtiririko mzuri kisheria.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 48 katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kifungu cha 48 (1) kinafutwa na kuandikwa upya kwa lengo la kuweka utaratibu rafiki wakati wa kukamata, kupekua, kuzuia mali na vielelezo, kuchukua maelezo ya watuhumiwa na mashahidi na kupeleleza kesi za dawa za kulevya,

(b) Kifungu kidogo cha (2) kinarekebishwa ili kuwezesha uchukuaji wa maelezo ya watuhumiwa au mashahidi kwa njia za kisasa kama vile rekoda, video, vifaa vya kidijitali,

(c) Kifungu kidogo kipya cha (4) kinaanzishwa ili kuweka utaratibu wa utoaji na upokeaji wa ushahidi uliokusanywa chini ya kifungu hiki mahakamani, na

(d) Kifungu kidogo kipya cha (5) kinaanzishwa ili kuainisha aina mbalimbali za Fomu kama zilivyotajwa katika Jedwali la Tatu la Sheria hii.

Kamati inapendekeza marekebisho ya kiuandishi katika Ibara ya 22(b):-ambapo maneno yanayopendekezwa yasomeke kama ifuatavyo:- By deleting the words "appearing in" and substituting for them the words "at the end of" in paragraph (aa) which will read as follows;

“(i) in paragraph (a)

(aa) by adding the words “unless he submits himself” at the end of subparagraph (1);”

Lengo ni kuainisha sehemu ambayo hayo maneno yanayopendekezwa yataingia ili kuleta maudhui ya kisheria iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 23 inapendekeza kuanzishwa Kifungu kipya cha 48A ili kuweka bayana utaratibu wa Mkemia Mkuu wa Serikali kupokea vielelezo vya Madawa ya Kulevya na kutoa ripoti ya uchunguzi huo.

Pamoja na kukubaliana na maudhui ya marekebisho haya, Kamati inashauri kuwa Mamlaka husika ihakikishe kuwa mianya ya kuharibu ripoti za Uchunguzi unaoainishwa chini ya Kifungu hiki, inazibwa na kudhibitiwa ili kuondoa mazingira ya kuwabambikia watuhumiwa kesi kwa kutumia ripoti zilizogushiwa au kuaribiwa.

Ibara ya 24 ya Muswada inapendekeza kufuta Kichwa cha Sehemu ya Tano ya Sheria kwa kukibadilisha na maneno yafuatayo:- *“Part V*

Forfeiture of Property Derived From or Used in Commission of An Offence Under Part III” Marekebisho hayo yanalenga kuainisha kichwa husika ili kiendane na maudhui yaliyomo katika sehemu husika kwakuzingatia marekebisho yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 25 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 49 kama ifuatavyo:-

(a) Kifungu cha 49(1) kinafutwa na kuandikwa upya kwa kuweka masharti kuwa mali itakayotaifishwa itajumuisha mali iliyopatikana kwa tarehe ambayo mshtakiwa alishtakiwa nasio tarehe ya kutiwa hatiani, pamoja na mali ya washirika wake na hivyo kuweka utaratibu mzuri wa kutaifisha mali na mazalia ya uhalifu,

(b) Kifungu cha 49(4) kinafutwa na kuandikwa upya kwa kuongeza muda wa Mali ya Mtuhumiwa iliyotokana na biashara ya dawa za kulevya kwa muda wa miaka kumi iliyopita itataifishwa badala ya miaka mitano,na

(c) Kifungu kidogo cha (5) kinafutwa kianchoipa Mamlaka uwezo wa kutaifisha mali kwa njia ya kiutawala (Administrative Forfeiture) kinafutwa kwakuwa masharti hayo yapo sehemu yenye kuhusu utafishaji wa kimahakama (Judicial Forfeiture). Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa masharti ya Sheria hii yazingatiwe wakati Mamlaka ikitekeleza utafishaji Mali kwa njia ya kiutawala (*Administrative Forfeiture*). Aidha, Ibara ya 26 ya Muswada inapendekeza kuanzishwa kwa Kifungu kipya cha 49A ambacho kinaweka utaratibu utakaotumika kutaifisha mali iliyozuliwa au kukamatwa au mali iliyotumika kutenda uhalifu.

Kamati inapendekeza marekebisho ya kiuandishi yafanyike katika Ibara ya 26(4): Neno 'appearers' liandikwe vizuri (Appears) ili kuleta maana iliyokusudia na hivyo aya isomeke:- *Where the article of property is susceptible to decay, or it appears the sale of such article or property would be necessary for its proper management the court may order the sale of that article or property.*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 27 ya Muswada inapendekeza kufuta Kifungu cha 50 na kukiandika Upya ambapo kifungu kipya kinatoa katazo kwa Mtu kukutwa na Mali haramu kwa mujibu wa sheria hii (*tainted Property*).Kamati inapendekeza kuwa kifungu kiainishe hatua stahiki zitakazochukuliwa kwa mtu atakayekiuka masharti ya kifungu hicho.

Ibara ya 28 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 51 kama ifuatavyo:-

(a) Kifungu cha 51 kinafanyiwa marekebisho kwa kuainisha taratibu za utafishaji mali kwanjia ya kiutawala (*Administrative Forfeiture*);

(b) Kifungu kidogo cha (2) kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta baadhi ya maneno ili kuondoa dhana ya utaifishaji wa Mali kwa njia ya Kimahakama (*Judicial Forfeiture*) ambayo haihusiani na maudhui ya kifungu hiki;

(c) Kufuta na kuandika upya vifungu vidogo vya (4), (5) na (7) ili kuainisha utaratibu utakaotumika wakati wa utaifishaji wa mali na mazalia ya uhalifu utakano na biashara ya dawa za kulevya na kemikali bashirifu kwa njia ya kiutawala; na

(d) Kifungu kidogo kipya cha (8) kinaongezwa ili kuweka utaratibu wa namna ya kushughulikia mali au mazalia ua uhalifu kwa njia ya kimahakama baada ya utaratibu wa njia ya kiutawala kushindikana.

Maudhui ya jumla ya mapendekezo haya ni kuainisha taratibu stahiki za kufuata kutoka kutaifisha mali kwa njia ya Kiutawala (*Administrative Forfeiture*) kwenda kutaifisha mali kwa njia ya Kimahakama (*Judicial Forfeiture*), kwa lengo la kuhakikisha haki inatendeka.

Ibara ya 30 inapendekeza kufutwa kwa Kifungu cha 52 kwakuwa maudhui ya kifungu hicho kuhusu *Burden of Proof* kwa mashauri ya utaifishaji mali k yameainishwa kwakina katika sheria ya Utaifishaji Mali, Sura 256.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 31 ya Muswada inapendekeza kufuta kifungu cha 53 na kuandikwa upya kwa kumpa Kamishna Generali Mamlaka ya kutaifisha Mali zilizothibitika kuwa zinatokana na Biashara ya Dawa za Kulevya pamoja na masharti yakuzingatiwa kabla yakufikiwa maamuzi hayo. Adha, Marekebisho yanatoa fursa kwa mtu ambaye hataridhishwa na tamko la kutaifisha mali husika kuomba mapitio (*Review*) katika Mahakama Kuu ndani ya Siku 30 tangu tamko kutolewa.

Kamati inakubaliana na marekebisho haya kwakuwa pamoja na kuongeza mamlaka ya kisheria kwa Kamishna Generali, sheria imeainisha na kutoa haki kwa Mtuhumiwa

kuchukua hatua ya kutafuta haki yake katika kupinga maamuzi ya Kamishna Generali katika Mahakama Kuu ambayo ndicho chombo pekee chenye Mamlaka ya mwisho Kikatiba katika kufanya maamuzi ya kisheria nchini.

Ibara ya 32 ya Muswada inapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 54(1) na kuandikwa upya kwa kumpatia Kamishna Jenerali mamlaka ya kutoa amri ya kusalimisha mali iliyotaifishwa badala ya kuacha mamlaka hiyo kwa Maafisa wa Mamlaka wanaotajwa katika Sheria ya sasa.

Kamati inakubaliana na mapendekezo haya kwakuwa yanalenga kuepusha uwezekano wa mamlaka hayo kutumiwa vibaya na hivyo kuweka msingi mzuri wa uwajibikaji na usimamizi miongoni mwa Watendaji/Maafisa wa Mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 33 ya Muswada inafuta kifungu cha 55(1) kinafutwa na kuandikwa upya ambapo pamoja na kuainisha taratibu lakini pia Serikali itakuwa na mamlaka ya kutaifisha Mali zilizo nje ya nchi za Mtu aliyetiwa hatiani chini ya sheria hii, kwa mujibu wa taratibu za Kimataifa kati ya Serikali ya Tanzania na Nchi husika.

Kamati inakubaliana na mapendekezo haya kwakuwa yanalenga kuziba mianya iliyokuwepo ambapo Mtu angeweza kutiwa hatiani lakini Serikali ikakosa nguvu kisheria katika kufuatilia na kudhibiti mali zilizotokana na biashara ya dawa za kulevya kwasababu ya mapungufu ya kisheria.

Ibara ya 34 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 65 yanayompa mamlaka Kamishna Jenerali kutoa maelekezo kwa taasisi za Serikali badala ya miongozo na kuainisha kuwa ukiukaji wowote wa maelekezo yake ni kosa. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwakuwa yanalenga kuimarisha utekelezaji wa maelekezo ya Kamishna Jenerali na hivyo kuongeza ufanisi katika kusimamia utekelezaji wa masharti ya Sheria hiyo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kufanyia marekebisho Majedwali kwa lengo la kuboresha orodha ya dawa za kulevya kulingana na viwango vya kimataifa. Aidha, inapendekezwa kufanya marekebisho ya fomu mbalimbali na kuziboresha baadhi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa masharti yake. Kamati inapendekeza kuwa, makosa madogo ya kiuandishi yaliyobainika katika upangaji wa majedwali na Fomu husika yasahihishwe na kuandikwa vizuri ili maudhui yake yaendane na Vifungu vya Sheria hiyo vinavyo yaanzisha.

3.0 MAPENDEKEZO YA JUMLA:

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni ya jumla ya Kamati yanayotokana na tathmini ya Maudhui ya Muswada huu kwa ujumla wake kama ifuatavyo:-

(a) Bila kuathiri matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mamlaka husika za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar zikae na kutafuta mbinu ya kudhibiti mianya yakupenyeshwa Dawa za kulevya kwa Upande wa Tanzania Zanzibar, kutokana na Sheria hii kutumika upande mmoja wa Muungano (Tanzania Bara).

(b) Wakati wa kutunga Kanuni za utekelezaji wa Sheria hiyo, Serikali ione umuhimu wa kuongeza Pombe aina ya Viroba na dawa nyingine za binadamu ambazo zinaweza kutumiwa kama dawa za kulevya ili ziwe sehemu ya orodha ya Dawa za kulevya kwa lengo la kudhibiti mbinu mpya za kuzalisha dawa mpya za kulevya hapa nchini.

(c) Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya ihakikishe inadhhibiti taarifa/ripoti za Uchunguzi unaoainishwa chini ya sheria hii kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuondoa mazingira ya kuwabambikia watuhumiwa kesi kwa kutumia ripoti zilizogushiwa au kuaribiwa kabla yakuifikia Mamlaka husika.

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kukushukuru kwa kutoa kibali ili Kamati ya Bunge ya

Masuala ya UKIMWI iweze kuufanyia kazi Muswada huu. Aidha, nawashukuru Wataalamu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamishna Jenerali na Wanasheria wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Idara ya Mshauri Mkuu wa Sheria wa Bunge, kwa kutoa ufafanuzi kwa Kamati katika maeneo mbalimbali ya Muswada. Maaafisa hao walifanya kazi hiyo kwa weledi na kujituma kwa lengo la kuhakikisha Muswada huu unachambuliwa vizuri kabla ya kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. **Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu rasmi za Bunge (HANSARD).**

- 1.Mhe. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb – **M/Mwenyekiti**
- 2.Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb -Mjumbe
- 3.Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mb -Mjumbe
- 4.Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb-Mjumbe
- 5.Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb-Mjumbe
- 6.Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb -Mjumbe
- 7.Mhe. Kemirembe Julius Lwota , Mb- Mjumbe
- 8.Mhe. Lucia Ursula Michael Mlowe, Mb-Mjumbe
- 9.Mhe. Mary Deo Muro, Mb -Mjumbe
- 10.Mhe. Salma Rashid Kikwete , Mb- Mjumbe
- 11.Mhe. Martha Moses Mlata, Mb-Mjumbe
- 12.Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb-Mjumbe
- 13.Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb-Mjumbe
- 14.Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb-Mjumbe
- 15.Mhe. Zainab Matitu Vullu, Mb-Mjumbe
- 16.Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb -Mjumbe

Mheshimiwa Spika, nawashukuu Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge Ndg.Stephen. N. Kagaigai kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi

Ndg. Dickson M. Bisile na Makatibu wa Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndg. Asia Msangi, Ndg. Happiness Ndalu, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Victor Leonard Mhagama na Msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Mwenye, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb
M/MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI
17 NOVEMBA, 2017

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutamsikia Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Masoud, Mbunge wa Mtambile. *(Makoff)*

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - K.n.y. MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Marekebisho ya Muswada wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa mwaka 2017 *(The Drug Control and Enforcement (Amendment) Act, 2017)* ambapo yanatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeeleza kuwa madhumuni ya Muswada huu ni kuondoa upungufu ambao umebainishwa katika utekelezaji wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya ya mwaka 2015. Aidha, Serikali imeelekeza kuwa lengo la marekebisho ni kupanua wigo na kuipa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya nguvu ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya. Pamoja na malengo hayo Serikali imeeleza

kuwa marekebicho ya sheria hii yanalenga pia kushughulikia makosa mengine ya jinai kama vile utakatishaji fedha, kughushi na usafirishaji haramu wa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya ilipitishwa rasmi na Bunge tarehe 24 Machi, 2015 na kusainiwa na Mheshimiwa Rais tarehe 11 Mei, 2015. Malengo ya kutunga sheria hiyo ilikuwa ni kutokana na kwamba Sheria Na. 9 ya mwaka 1995 haikuleta tija inayostahili kudhibiti biashara haramu ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake marekebicho yaliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu ni ya kudhibiti kwa kuongeza adhabu na kuwa kali zaidi kuliko ilivyokuwa awali. Kuna usemi kwamba *“the higher the risk the higher the return.”* Hii maana yake ni kwamba adhabu kubwa zinazopendekezwa katika Muswada huu zinaweza kupandisha thamani dawa za kulevya na hivyo kuwa motisha kwa ambao wanaweza kujitoa kukabiliana na adhabu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona marekebicho haya yaliyoletwa na Serikali yanaweza yakawa njia ya kumtafuta mchawi badala ya kutibu tatizo la dawa za kulevya. Hii ni kwa sababu Serikali inaonekana kupunguza kasi ya utoaji wa elimu ya kudhibiti dawa za kulevya badala ya kutoa elimu kwa vijana na kutoa matibabu kwa walioathirika na matumizi ya dawa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona pia kuwa mapendekezo ya marekebicho mengi yanayopendekezwa katika Muswada huu yanalenga watumiaji wa kawaida wa dawa za kulevya badala ya kushughulikia wazalishaji na wasafirishaji wakubwa wa dawa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kutoa maoni kuhusu Ibara za Muswada huu ambazo kwa mtazamo wetu tunaona kuwa

zitaleta usumbufu mkubwa kwa jamii kama itapitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6 ya Muswada inayofanyia marekebisho kifungu cha 9 cha sheria kwa kuongeza kifungu kidogo cha (7) ambacho kinatoa mamlaka kwa mwakilishi wa Mamlaka kuwa Katibu wa Kamati. Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa kutokana na umuhimu wa Kamati hiyo iwekwe wazi katika sheria kuwa mwakilishi wa Mamlaka awe Afisa mwenye Wadhifa wa Juu katika uongozi na utawala wa Mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 8 ya Muswada inafanyia marekebisho kifungu cha 15 cha sheria kwa kuongeza kifungu kipya cha (3) ambacho kinaweka masharti ya aina na kiasi cha madawa ambayo mtu akikutwa na hatia ya kusafirisha madawa hayo atakuwa ametenda kosa la jinai. Aidha, Ibara ya 9 ya Muswada inaongeza kifungu kipya cha 15A cha sheria ambacho kinatoa adhabu ya kifungu cha miaka thelathini jela kama mhusika atapatikana na makosa yanayotajwa katika kifungu kidogo cha (2).

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa yaliyoainishwa katika Ibara ya 8 na 9 yataleta mkanganyiko katika jamii na vyombo vinavyosimamia haki kwa sababu ya kiwango na aina ya madawa ambacho atakutwa nacho mtuhumiwa. Hii ni kutokana na viwango vinavyotajwa katika kifungu kidogo kipya cha 15(3) kuwa mtu atafanya kosa ikiwa atakutwa na bangi au mirungi inayozidi kilo 50, wakati kifungu kipya cha 15A(2)(c) kinasema kama mtu atasafirisha bangi au mirungi chini ya kilo 50 atakuwa ametenda kosa na adhabu yake ni kifungu cha miaka 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 inafanyia marekebisho kifungu cha 27 cha sheria ambacho kinahusu adhabu kwa makosa ambayo adhabu zake hazikutajwa katika sheria. Vifungu vya sheria ambavyo vinapendekezwa kufutwa vilikuwa vinatoa ruhusa kwa Hakimu kupima kiwango kutokana na sheria kutowekewa kiwango cha chini. Mapendekezo ya Muswada huu yakiridhiwa na Bunge,

kiwango cha juu kimepandishwa na kiwango cha chini kimewekwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji msingi na sababu hasa za kupandisha kiwango cha adhabu toka shilingi milioni 20 hadi shilingi milioni 50 ili Waheshimiwa Wabunge na Bunge kwa ujumla waelewe malengo ya Serikali katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara 11 ikisomwa kwa pamoja na Ibara ya 13 ambayo inafanyia marekebisho kifungu cha 29 cha sheria kuhusu makosa yasiyo na dhamana ya polisi, itaonekana kuwa marekebisho yanayopendekezwa yanafuta gramu 200 za awali na kuzipunguza kuwa gramu 20. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa marekebisho ya masharti haya yanaweza kutumika kwa hila na bila kuwa na nia njema kwa sababu kama mtu anaweza kuchukua silaha nzito za kivita na kumshambulia mtu mchana kweupe atashindwaje kumuwekea mtu yeyote kiasi hicho cha madawa kwa lengo la kutaka kumkomoa akose dhamana ya polisi na pia ikiwezekana afungwe miaka 30? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa na mapendekezo ya Muswada huu ya kumwondoa Mkemia Mkuu wa Serikali (*Government Chemist*) katika sheria na kumweka mtu mwingine (*Government Analyst*) ambaye hata hivyo haijaelezwa ni mtu wa namna gani katika kifungu cha ufafanuzi. Ibara ya 13 ya Muswada inafanya marekebisho katika kifungu 29 cha sheria, aya ya (b) inafuta maneno "*Government Chemist*" na kuweka maneno "*Government Analyst*". Maneno hayo yanayobadilishwa bila ya kutolewa tafsiri au kutolewa ufafanuzi ni kwa nini Mkemia Mkuu wa Serikali ameondolewa, italeta maswali na mashaka kuhusu sababu za kumwondoa Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 23 ya Muswada inaongeza kifungu kipya cha 48A katika sheria. Kambi Rasmi ya Upinzani kama ambavyo imeonesha wasiwasi hapo awali kuhusu "*Government Analyst*" badala ya "*Government Chemist*" inapenda kueleza kuwa ni vyema Serikali na Bunge tukawa na umakini katika hili kwani jambo hili linahusu

maisha ya watu. Hii ni kutokana na sababu ni lazima mtu anayepima sampuli za watuhumiwa awe ni mtu wa kuaminika na mwenye kutenda haki kwa sababu matokeo ya vipimo vyake vinaweza kusababisha mtu kufungwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhoji, je, kuna mamlaka nyingine inayoweza kuaminika katika upimaji wa sampuli mbalimbali za kimaabara zaidi ya Mkemia Mkuu wa Serikali? Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu sababu zaidi zinazosababisha kuondolewa Mkemia Mkuu wa Serikali na kuwekwa huyo anayelitwa *Government Analyst*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa kila mwaka ifikapo tarehe 26 Juni, dunia huadhimisha siku ya kupinga biashara na matumizi haramu ya dawa za kulevya. Katika hili, Kambi ya Upinzani Bungeni imekuwa mstari wa mbele katika kuishauri Serikali na jamii kwa ujumla kuhusu matumizi ya madawa ya kulevya na athari zake kwa nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni aliyoitoa mwezi Aprili, 2017 wakati wa mjadala kwenye Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu tuliitaka Serikali kuwa na mbinu bora zaidi za kupambana na biashara hii haramu ambapo tulishauri mbinu hizo kuzingatia weledi na sheria za nchi, kuheshimu utu na haki za kila raia katika kupambana na sakata hili la dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka mapema mwaka huu harakati za kupambana na dawa za kulevya zilichukua sura mpya baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kuwataja hadharani watuhumiwa wa dawa za kulevya huku kila mmoja akilipokea kwa namna yake kutokana na Mkuu huyo wa Mkoa kuwataja watu bila kuwa na ushahidi wowote huku kitendo kile kikifanywa kwa ubabe, kebehi, dhihaka na uonevu mkubwa kwa kuwa utaratibu uliotumika haukuzingatia masharti kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukiukwaji huo mkubwa wa haki za binadamu na udhalilishaji uliofanyika

kwa watuhumiwa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya Kiongozi Mkuu huyo wa Mkoa. Ndani ya Bunge lako hili Wabunge walionesha hisia zao za kukerwa na jambo lile lililokosa staha ya uongozi na lililolenga kudhalilisha watu mbalimbali. Kambi Rasmi ya Upinzani iliiani na itaendelea kulaani vikali tabia hiyo kwani vita vya dawa za kulevya siyo vita ya mtu mmoja au vita binafsi bali ni jukumu la jamii nzima kuhakikisha inapinga kwa nguvu zote biashara na matumizi ya aina yoyote ya dawa za kulevya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesema kuwa lengo la Muswada huu pamoja na mambo mengine umejikita katika kuboresha ufanisi wa Mamlaka katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya. Pamoja na hilo Muswada huu una vipengele vyenye utata ambapo bila kuvichambua kwa undani na kwa makini vinaweza kuwa kichaka kikubwa cha ukiukwaji wa haki za raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani, katika Ibara ya 19 ya Muswada inatoa mamlaka kwa Maafisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kuzuia Dawa za Kulevya kutumia silaha za moto na vilipuzi (*firearms and ammunition*) katika mazingira ambayo wanadhani yanaweza kuhatarisha usalama wao. Ibara hiyo inamruhusu afisa huyu kufyatua risasi au kutumia silaha kwa mtu yeyote anayehisiwa/kushukiwa kutumia au kuuza madawa pale anapotaka kukimbia, anakimbia au kutaka kuleta hatari na amepewa tahadhari kuwa afisa anaweza kutumia silaha ya moto wakati wowote. Katika hali ya kawaida, Ibara hii ni hatari sana na ikitumiwa vibaya inaweza kuwa na madhara makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kuwa mwenye mamlaka ya kumkamata raia yeyote anayehisiwa au aliyetenda kosa kinyume na sheria ni askari aliyepewa mafunzo. Kitendo cha kuruhusu maafisa hawa ambao hajjaelezwa kwenye Muswada kama wanayo mafunzo ya kukamata au utaalumu wa kushughulikia wahalifu kama vile askari au maafisa wa usalama. Katika hali hii afisa anapopewa mamlaka makubwa ya kutumia silaha ni hatari sana kwa usalama wa raia hasa pale atakapotumia silaha

hizo kinyume na masharti ya kisheria. Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa kazi ya kupambana na dawa za kulevya ni ya hatari. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kuruhusu maafisa chini ya mamlaka hii kutumia silaha bila kueleza utaratibu wa mafunzo maalum yanayotambuliwa kwa mujibu wa sheria ni hatari zaidi. Mapendekezo haya yakiachwa kama yalivyo anaweza kutokea afisa yeyote ambaye hana weledi na kutumia fursa hiyo vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya sasa ya kisiasa ambapo kumekuwa na wimbi kubwa la mashambulizi kwa kutumia silaha, chuki za kisiasa na utaratibu mpya wa kutaja majina kwenye vyombo vya habari kwa hisia kuwa watu fulani wanaweza kuwa wanajihusha na dawa za kulevya ni dhahiri kuwa hali kama hii inaweza kabisa kupelekea baadhi ya maafisa ambao hawana weledi kutumia mwanya huo vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ripoti ya Umoja wa Mataifa iliyotolewa mwaka 2016 iliitaka nchi ya Uphilipino chini ya Rais Rodrigo Duterte kuacha kufanya mauji kwa watu wanaodhaniwa kutumia au kuuza dawa za kulevya kwa kuwa matukio hayo yalisababisha mauaji ya raia zaidi ya 700 ndani ya kipindi cha miezi mitatu pekee. Katika matukio hayo, wapo raia waliokumbwa na madhila hayo ilhali hawakuwahi kutumia wala kuuza dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa Ibara hii isipoangaliwa inaweza kuchochea mauaji endapo maafisa chini ya mamlaka hii hawatapewa mafunzo ya kutosha. Hivyo basi, ni vyema Serikali au sheria ikawa na msisitizo wa kuwabana na kutoa mafunzo yenye tija ili kutokuruhusu mwanya wowote wenye nia ovu kwa afisa ambaye atakosa weledi katika utekelezaji wake wa majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, ukisoma kifungu cha 5 ya sheria ambayo inahusu Wajumbe wa Baraza la Taifa la Kudhibiti Madawa ya Kulevya *(The National Drug Control Council)*, Baraza hilo linaundwa na wajumbe (Mawaziri) ambao baadhi yao wanasimamia Wizara ambazo ni za

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Muungano na wanaotoka Zanzibar. Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka kupatiwa ufafanuzi kuhusu matumizi ya maneno "Baraza la Taifa" kama yalivyotumika katika kifungu hicho cha sheria na uhusiano wake na Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 1 na Ibara ya 2(2) ambapo Katiba inasema kuwa Tanzania ni nchi moja na Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kupambana na madawa ya kulevya lina changamoto zaidi kuliko kupambana na majambazi. Mtazamo wa jumla wa sheria hii unatoa fursa ya kudhibiti madawa ya kulevya kwa upande wa Tanzania Bara wakati sheria imeunda Baraza la Taifa la Kupambana na Dawa za Kulevya. Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na namna utaratibu ulivyotumika katika maandalizi ya Muswada huu na hatua iliyofikiwa kuletwa Bungeni huku kukiwa na wasiwasi juu ya ushirikishwaji wa upande wa pili wa Muungano yaani Zanzibar, ambapo kuna tatizo kubwa la dawa za kulevya japokuwa jambo hili si jambo la Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuelewa ukubwa wa tatizo la mirungi ndani ya nchi yetu sambamba na changamoto kuwa katika nchi ya Kenya zao hilo ni halali kuotesha na kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, itakumbukwa kuwa dawa za kulevya yameharamishwa pia na Itifaki ya Ulinzi na Usalama ya Jumuiya Afrika Mashariki.

Pamoja na Ibara ya 12 ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kueleza kuwa kutakuwa na shughuli za pamoja katika kutekeleza masharti ya itifaki hiyo, ikiwa ni pamoja na shughuli za kuzuia usafirishaji wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi ya Kenya imehalalisha matumizi ya mirungi, nchi ya Kenya haitaweza kutekeleza masharti ya itifaki hiyo kwa sababu imehalalisha matumizi ya madawa hayo kama itaamuliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kupambana na madawa ya mirungi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. Nawashukuru sana nyote. (*Makofi*)

**MAONI YA MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
KATIKA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU MAREKEBISHO YA
MUSWADA WA SHERIA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA
DAWA ZA KULEVYA WA MWAKA 2017 (The Drug Control and
Enforcement (Amendment) Act, 2017) KAMA
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

(Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza kuwa madhumuni ya Muswada huu ni kuondoa upungufu ambao umebainishwa katika utekelezaji wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya ya mwaka 2015. Aidha Serikali imeelekeza kuwa lengo la marekebisho ni kupanua wigo na kuipa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya nguvu ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na malengo hayo Serikali imeeleza kuwa marekebisho ya Sheria hii yanalenga pia kushughulikia makosa mengine ya jinai kama vile utakatishaji fedha, kughushi na usafirishaji haramu wa watu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya ilipitishwa rasmi na Bunge tarehe 24 Machi, 2015 na kusainiwa na Mheshimiwa Rais tarehe 11 Mei, 2015. Malengo ya kutunga Sheria hiyo ilikuwa ni kutokana na kwamba sheria namba 9 ya mwaka 1995 haikuleta tija inayostahili kudhibiti biashara haramu ya madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake marekebisho yaliyowasilishwa katika Bunge lako tukufu ni ya kudhibiti kwa kuongeza adhabu na kuwa kali zaidi kuliko ilivyokuwa awali. Kuna usemi kwamba; *“the higher the risk the higher the return”*. Hii maana yake ni kwamba adhabu kubwa zinazopendekezwa katika Muswada huu zinaweza kupandisha thamani madawa ya kulevya na hivyo kuwa motisha kwa ambao wanaweza kujitoa kukabiliana na adhabu hizo.

Mheshimiwa Spika, Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona marekebisho haya yaliyoletwa na Serikali yanaweza yakawa njia ya kumtafuta mchawi badala ya kutibu tatizo la madawa ya kulevya. Hii ni kwa sababu Serikali inaonekana kupunguza kasi ya utoaji wa elimu ya kudhibiti madawa ya kulevya badala ya kutoa elimu kwa vijana na kutoa matibabu kwa walioathirika na matumizi ya madawa hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona pia kuwa mapendekezo ya marekebisho mengi yanayopendekezwa katika muswada huu yanalenga watumiaji wa kawaida wa madawa ya kulevya badala ya kushughulikia wazalishaji na wasafirishaji wakubwa wa madawa hayo.

2. MAPITIO YA MUSWADA

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba kutoa maoni kuhusu ibara za Muswada huu ambazo kwa mtazamo wetu tunaona kuwa yataleta usumbufu mkubwa kwa jamii kama yatapitishwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6 ya Muswada inayofanyia marekebisho kifungu cha 9 cha Sheria kwa kuongeza kifungu kidogo cha 7 ambacho kinatoa mamlaka kwa Mwakilishi wa Mamlaka kuwa Katibu wa Kamati. Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa kutokana na umuhimu wa kamati hiyo iwekwe wazi katika Sheria kuwa

Mwakilishi wa Mamlaka awe afisa mwenye wadhifa wa juu katika uongozi na utawala wa Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8 ya muswada inafanyia marekebisho kifungu cha 15 cha Sheria kwa kuongeza kifungu kipyua cha 3 ambacho kinaweka masharti ya aina na kiasi cha madawa ambayo mtu akikutwa na hatia ya kusafirisha madawa hayo atakuwa ametenda kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 ya muswada inaongeza kifungu kipyua cha 15A cha Sheria ambacho kinatoa adhabu ya kifungu cha miaka 30 jela kama mhusika atapatikana na makosa yanayotajwa katika kifungu kidogo cha 2.

Mheshimiwa Spika, makosa yaliyoainishwa katika ibara ya 8 na 9 yataleta mkanganyiko katika jamii na vyombo vinavyosimamia haki kwa sababu kiwango na aina ya madawa ambacho atakutwa nacho mtuhumiwa. Hii ni kutokana na viwango vinavyotajwa katika kifungu kidogo kipyua cha 15 (3) kuwa mtu atafanya kosa ikiwa atakutwa na bangi au mirungi inayozidi kilo hamsini, wakati kifungu kipyua cha 15A(2) (c) kinasema kama mtu atasafirisha bangi au mirungi chini ya kilo hamsini atakuwa ametenda kosa na adhabu yake ni kifungu cha miaka 30.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11 inafanyia marekebisho kifungu cha 27 cha Sheria ambacho kinahusu adhabu kwa makosa ambayo adhabu zake hazikutajwa katika sheria. Vifungu vya Sheria ambavyo vinapendekezwa kufutwa vilikuwa vinatoa ruhusa kwa Hakimu kupima kiwango kutokana na Sheria kutowekewa kiwango cha chini.

Mheshimiwa Spika, kwa mapendekezo ya Muswada huu na yakiridhiwa na Bunge, kiwango cha juu kimepandishwa na kiwango cha chini kimewekwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji msingi na sababu hasa za kupandisha kiwango cha adhabu toka milioni ishirini hadi milioni hamsini ili Waheshimiwa Wabunge na Bunge kwa ujumla waelewe malengo ya Serikali katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, Ibara 11 ikisomwa kwa pamoja na Ibara ya 13 ambayo inafanyia marekebisho kifungu cha 29 cha Sheria kuhusu makosa yasiyo na dhamana ya polisi, itaonekana kuwa marekebisho yanayopendekezwa yanafuta gramu mia mbili (200) za awali na kuzipunguza na kuweka gramu ishirini. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa marekebisho ya masharti haya yanaweza kutumika kwa hila na bila kuwa na nia njema kwa sababu kama mtu anaweza kuchukua silaha nzito za kivita na kumshambulia mtu mchana kweupe atashindwaje kumuwekea mtu yeyote kiasi hicho cha madawa kwa lengo la kutaka kumkomoa akose dhamana ya Polisi na pia ikiwezekana afungwe miaka thelathini?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa na mapendekezo ya Muswada huu ya kumwondoa Mkemia Mkuu wa Serikali (Government Chemist) katika Sheria na kumweka mtu mwingine (Government Analyst) ambaye hata hivyo haijaelezwa ni mtu wa namna gani katika kifungu cha ufafanuzi. Ibara ya 13 ya muswada inafanyia marekebisho katika kifungu 29 cha Sheria, aya ya (b) inafuta maneno **“Government Chemist”** na kuweka maneno **“Government Analyst”**. Maneno hayo yanayobadilishwa bila ya kutolewa tafsiri au kutolewa ufafanuzi ni kwanini Mkemia Mkuu wa Serikali ameondolewa, inaleta maswali na mashaka kuhusu sababu za kumwondoa Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 23 ya muswada inaongeza kifungu kipya cha 48A katika Sheria. Kambi Rasmi ya Upinzani kama ambavyo imeonesha wasiwasi hapo awali kuhusu **“Government Analyst”** badala ya **“Government Chemist”** inapenda kueleza kuwa ni vema Serikali na Bunge tukawa na umakini katika hili kwa jambo hili linahusu maisha ya watu. Hii ni kutokana na sababu ni lazima mtu anayepima sampuli za watuhumiwa awe ni mtu wa kuaminika na mwenye kutenda haki kwa sababu matokeo ya vipimo vyake vinaweza kupelekea mtu kufungwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhoji, je kuna mamlaka nyingine inayoweza kuaminika katika upimaji wa sampuli mbalimbali za

kimaabara zaidi ya Mkemia Mkuu wa Serikali? Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu sababu zaidi zilizopelekea kuondolewa Mkemia Mkuu wa Serikali na kuwekwa huyo anayeitwa "Government Analyst".

Mheshimiwa Spika, Ikumbukwe kuwa kila mwaka ifikapo tarehe 26 Juni dunia huadhimisha siku ya kupinga biashara na matumizi haramu ya dawa za kulevya. Katika hili, Kambi ya Upinzani Bungeni imekuwa mstari wa mbele katika kuishauri serikali na jamii kwa ujumla kuhusu matumizi ya madawa ya kulevya na athari zake katika nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Katika hotuba ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani aliyoitoa Mwezi April 2017 wakati wa mjadala kwenye Bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu tuliitaka serikali kuwa na mbinu bora zaidi za kupambana na biashara hii haramu ambapo tulishauri mbinu hizo kuzingatia weledi na sheria za nchi, kuheshimu utu na haki za kila raia katika kupambana na sakata hili la dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, tutakumbuka mapema mwaka huu harakati za kupambana na dawa za kulevya zilichukua sura mpya baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kuwataja hadharani watuhumiwa wa dawa za kulevya huku kila mmoja akilipokea kwa namna yake kutokana na Mkuu huyo wa Mkoa kuwataja watu bila kuwa na ushahidi wowote huku kitendo kile kikifanywa kwa ubabe, kebehi, dhihaka na uonevu mkubwa kwa kuwa utaratibu uliotumika haukuzingatia masharti kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukiukwaji huo mkubwa wa haki za binadamu na udhalilishaji uliofanyika kwa watuhumiwa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya kiongozi Mkuu huyo wa Mkoa. Ndani ya Bunge lako hili wabunge walionyesha hisia zao za kukerwa na jambo lile lililokosa staha ya uongozi na lililolenga kudhalilisha watu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ililaani na itaendelea kulaani vikali tabia hiyo kwani vita ya dawa za kulevya sio vita ya mtu mmoja au vita binafsi bali ni jukumu la jamii nzima kuhakikisha inapinga kwa nguvu zote biashara na matumizi ya aina yoyote ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesema kuwa lengo la Muswada huu pamoja na mambo mengine umejikita katika kuboresha ufanisi wa Mamlaka katika kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevya. Pamoja na hilo Muswada huu una vipengele vyenye utata ambapo bila kuvichambua kwa undani na kwa makini vinaweza kuwa kichaka kikubwa cha ukiukwaji wa haki za raia. Mathalani, katika Ibara ya 19 ya Muswada inatoa Mamlaka kwa Maafisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kuzuia Dawa za kulevya kutumia **silaha za moto na vilipuzi** (firearms and ammunition) katika mazingira ambayo wanadhani yanaweza kuhatarisha usalama wao.

Mheshimiwa Spika, Ibara hiyo inamruhusu Afisa huyu kufyatua risasi au kutumia silaha kwa mtu yeyote anayehisiwa/kushukiwa kutumia au kuuza madawa pale anapotaka kukimbia, anakimbia au kutaka kuleta hatari na amepewa tahadhari kuwa Afisa anaweza kutumia silaha ya moto wakati wowote. Katika hali ya kawaida Ibara hii ni hatari sana na ikitumiwa vibaya inaweza kuwa na madhara makubwa.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kuwa mwenye Mamlaka ya kumkamata raia yoyote anayehisiwa au aliyetenda kosa kinyume na Sheria ni askari aliyepewa mafunzo. Kitendo cha kuruhusu maafisa hawa ambao hajjaelezwa kwenye Muswada kama wanayo mafunzo ya kukamata au utaalumu wa kushughulika na wahalifu kama vile askari au maafisa wa usalama. Katika hali hii Afisa anapopewa mamlaka makubwa ya kutumia silaha ni hatari sana kwa usalama wa raia hasa pale atakapotumia silaha hizo kinyume na masharti ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa kazi ya kupambana na dawa za kulevya

ni kazi ya hatari. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kuruhusu Maafisa chini ya Mamlaka hii kutumia silaha bila kueleza utaratibu wa mafuzo maalum yanayotambuliwa kwa mujibu wa Sheria ni hatari zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo haya yakiachwa kama yalivyo anaweza kutokea Afisa yeyote ambaye hana weledi na kutumia fursa hiyo vibaya.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya sasa ya kisiasa ambapo kumekuwa na wimbi kubwa la mashambulizi kwa kutumia silaha, chuki za kisiasa, na utaratibu mpya wa kutaja majina kwenye vyombo vya habari kwa hisia kuwa watu fulani wanaweza kuwa wanajihusha na madawa ya kulevya ni dhahiri kuwa hali kama hii inaweza kabisa kupelekea baadhi ya Maofisa ambao hawana weledi kutumia mwanya huo vibaya.

Mheshimiwa Spika, katika ripoti ya Umoja wa Mataifa iliyotolewa mwaka 2016, iliitaka nchi ya Ufilipino chini ya Rais Rodrigo Duterte kuacha kufanya mauji kwa watu wanaodhaniwa kutumia au kuuza dawa za kulevya kwa kuwa matukio hayo yalisababisha mauaji ya raia zaidi ya 700 ndani ya kipindi cha miezi mitatu pekee. Katika matukio hayo wapo raia waliokumbwa na madhila hayo ilhali hawakuwahi kutumia wala kuuza dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Ni dhahiri kabisa Ibara hii isipoangaliwa inaweza kuchochea mauaji (Extra Judicial killings) endapo Maofisa chini ya Mamlaka hii hawatapewa mafunzo ya kutosha. Hivyo basi, ni vyema Sheria ikawa na msisitizo wa kuwabana na kutoa mafunzo yenye tija ili kutokuruhusu mwanya wowote wenye nia ovu kwa Afisa ambae atakosa weledi katika utekelezaji wake wa majukumu.

3. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, ukisoma kifungu cha 5 ya Sheria ambayo inahusu wajumbe wa Baraza la Taifa la kudhibiti

madawa ya kulevya (The National Drug Control Council), Baraza hilo linaundwa na wajumbe (Mawaziri) ambao baadhi yao wanasimamia Wizara ambazo ni za Muungano na wanaotoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka kupatiwa ufafanuzi kuhusu matumizi ya maneno "Baraza la Taifa" kama yalivyotumika katika kifungu hicho cha sheria, na uhusiano wake na Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 1 na Ibara ya 2(1) ambapo Katiba inasema kuwa Tanzania ni nchi moja na Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kupambana na madawa ya kulevya lina changamoto zaidi kuliko kupambana na majambazi. Mtazamo wa jumla wa sheria hii unatoa fursa ya kudhibiti madawa ya kulevya kwa upande wa Tanzania Bara wakati Sheria imeunda Baraza la Taifa la Kupambana na Dawa za Kulevya.

Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na namna utaratibu ulivyotumika katika maandalizi ya muswada huu na hatua iliyofikiwa kuletwa Bungeni huku kukiwa na wasiwasi juu ya ushirikishwaji wa Upande wa pili wa Muungano, yaani Zanzibar, ambapo kuna tatizo kubwa la madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuelewa ukubwa wa tatizo la Mirungi ndani ya nchi yetu sambamba na changamoto kuwa katika nchi ya Kenya zao hilo ni halali kuotesha na kutumia.

Mheshimiwa Spika, aidha itakumbukwa kuwa madawa ya kulevya yameharamishwa pia na Itifaki ya Ulinzi na Usalama ya Jumuiya Afrika Mashariki. Pamoja na ibara ya 12 ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kueleza kuwa kutakuwa na shughuli za pamoja katika kutekeleza masharti ya itifaki hiyo, ikiwa ni pamoja na kuwa na shughuli za pamoja kwa mujibu wa Itifaki ikiwa ni pamoja na shughuli za kuzuia usafirishaji wa madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi ya Kenya imehalalisha matumizi ya mirungi, nchi ya Kenya haitaweza kutekeleza masharti ya Itifaki hiyo kwa sababu imehalalisha matumizi ya madawa hayo kama itaamuliwa Jumuiya ya Afrika Mashariki wataamua kupambana na madawa ya mirungi.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni naomba kuwasilisha.

.....
MASOUD ABDALLA SALIM (Mb)
K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI OFISI YA WAZIRI MKUU
17 Novemba, 2017

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimepata majina hapa kutoka vyama vyenye uwakilishi Bungeni. Ninayo majina ya Chama cha Mapinduzi, Chama cha Demokrasia na Maendeleo na Chama cha Wananchi (*CUF*).

Sasa kwa kuzingatia muda tulionao na kila chama kilishauriwa kuleta mchangiaji mmoja lakini naona kuna vyama majina yanakuwa mengi zaidi, kwa hiyo muda tutaugawanya kati ya hayo majina yaliyoletwa hapa mbele.

Chama cha Wananchi *CUF* kuna majina matatu kwa hivyo kila mmoja atachangia dakika tano kwa sababu sasa hatutaki kuingia tena kwenye mjadala wa Kambi zinahusika vipi. Mheshimiwa Ally Saleh, atachangia dakika tano, Mheshimiwa Mussa Mbarouk, atachangia dakika tano na Mheshimiwa Riziki Lulida dakika tano. Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sheria hii imekuja wakati mzuri sana na *in fact* imechelewa kupita kiasi kwa sababu tumepitisha sheria hii mwaka 1995, tukafanya marekebisho mwaka 2015 mpaka

hivi sasa lakini bado tunakwenda katika hali ambayo mimi nisingefurahi kwamba inachelewa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni sheria ambayo ni lazima iakisi mtazamo wa dunia. Tatizo la dawa za kulevya lazima utizame katika picha ya dunia na ni kitu ambacho ni uchumi na ni maisha ya watu hao ambao wanahusika na *drugs*. Kwa hivyo, ili kupambana na *barons* wale wakubwa wa biashara hii ni lazima uwe na sheria ambayo ningetarajia ingekuwa *better* zaidi kuliko ambayo imekuja hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inakwenda zaidi kwenye adhabu kuliko taaluma. Kuna baadhi ya wenzetu sisi ambao tunashiriki katika Bunge la *SADC* wanakwenda kwenye *de-criminalization*, mtazamo ambao badala ya kutoa adhabu kwa mkosaji/mtumiaji unatafuta njia ya kumfunza, njia ya kumtoa katika utumiaji kuliko kumfunga maana ukimpeleka jela anakuwa sugu na pengine anapata maradhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wengine vilevile wamekuwa wakitazama zaidi katika suala la elimu na suala la utamaduni kwa sababu uki-*instill culture* ya watu kujijua, kujitambua kutoka ujana wao na utoto wao unatengeneza mazingira mazuri ya mtu kutotumia unga kabla hajautumia lakini hilo linakosekana. Ni kweli tunasikia hapa na pale kuna elimu zinatolewa lakini nafikiri eneo hili lingetiliwa zaidi mkazo lingetusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema pale mwanzo lazima uwe na *global approach*. Msemaji wa Kambi ya Upinzani amezungumzia juu ya utata uliopo kwa mfano baina ya sisi na Kenya kuhusu suala la mirungi. Kama tukichukua *joint effort* wao kwao mirungi ni halali, lakini pia *SADC* wanasema *effort to fight against drugs is hampered by lack of legal uniformity*. Kwa hiyo, hili pia Serikali ilitazame vipi tunafanya kazi na wenzetu *otherwise effort* yetu itakuwa haina nguvu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naona kuna pendekezo la kufanya suala hili la *drugs* kuchukua ushahidi kwa njia ya *online* au ya mitandao, lakini pia ningependa sheria hii itazame kipengele kidogo cha kutizama namna ya kupata *supply* ya *drugs* kupitia mitandao. Hivi sasa Tanzania si ajabu kupata *supply* ya *sex* kupitia kwenye mitandao. Tunaona makundi mbalimbali kwenye mitandao yanatangaza njoo utapata huduma hii, na sasa naona pengine tunaweza tikaelekea huko sasa ikawa mpaka si tu *sex*, lakini mpaka unga unaweza ukapata kupitia *online*, ningependa hili litazamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona hapa pembeni kuna pendekezo la kuifanya sheria hii iende mpaka Zanzibar; nafikiri hii si sahihi. Jana tu hapa tumetoka kuukataa muswada ambao umesema ufanye kazi Zanzibar wakati jambo hilo si la Muungano.

Kwa hiyo, pamoja na ukweli, na mimi ni muathirika wa matumizi ya unga kwa maana ya watoto wangu, watoto wa ndugu zangu wengi watatu/wanne wameingia hii, lakini bado sioni uhalali wa Kikatiba/wa kisheria jambo hili kulipeleka Zanzibar kwa sababu kule tuna taasisi yetu na mipango yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependekeza kama sheria itaweza kusema kuwepo na *joint commission* ambayo inaweza ikafanya kazi, ili ifanye kazi kwa pamoja, kwa sababu nakubaliana na hoja kwamba, huwezi kupigana na hiki kitu bila kuwa *inclusive* sote, lakini haina maana kwamba, ulazimishe sheria ambayo kitu ambacho si cha muungano ukipeleke kwenye mambo ya muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh hilo la mwisho nadhani uwaandikie hapo mbele watalipata.

Mheshimiwa Mussa Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Ruth Mollel ajiandae.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Mimi kwanza nishukuru kwa kupata nafasi hii, lakini vilevile niunge mkono asilimia 100 Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, hata hivyo na mimi nina ya kwangu machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la dawa za kulevya ni tatizo la kimataifa, lakini moja ya changamoto zinazojitokeza katika nchi yetu, bado ipo mianya mingi ambayo inasababisha dawa za kulevya zingizwe nchini. Kwa mfano katika viwanja vya ndege bado ni mwanya ambao unatumika mara nyingi sana kuingiza dawa za kulevya nchini mwetu. Jambo lingine pia katika viwanja vya ndege hivyo hivyo kuna mbinu mpya ambayo wasafirishaji wanaitumia sasa hivi ambayo ni ya kupitisha watu kama wagonjwa katika *wheel chairs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati mwingine inapofikia hatua hiyo hapo hapo inatolewa taarifa kwamba *lift* hazifanyi kazi, hapo ndio wanapopenya waingizaji wa dawa za kulevya na wakatamia mwanya huo kufanya biashara hiyo ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali katika viwanja vyetu vya ndege tuwe makini sana na tuwe macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa za kulevya ni biashara kubwa, kama alivyoseme mtangulizi wangu Mheshimiwa Mnadhimu Ally Saleh, kwamba hii biashara kubwa, imewahi kufanywa hata na baadhi ya Marais. Tuliona ugomvi kati ya Rais Manuel Antonio Noriega na Rais wa Marekani aliyemaliza muda wake kipindi cha nyuma bwana George Bush.

Sasa haya yalikuwa ni mapambano ya biashara, kwa hiyo na sisi tusije tukafikiri kwamba tunapozungumza biashara ya dawa za kulevya tunazungumzia kitu rahisi. Hili ni tatizo kubwa la kimataifa. Na jambo lolote ambalo linaingiza fedha binadamu anatafuta kila aina ya mbinu,

kila aina ya nyenzo kuhakikisha kwamba, biashara hiyo inafanyika. Kwa hiyo, mimi nashauri tu Serikali iwe makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulisema ni kwamba kuna mkanganyiko sasa katika nchi zetu za Afrika Mashariki. Ukienda Burundi, Rwanda, Kenya, Uganda na *Southern Sudan* mirungi ni kitu kinachotumika kama uraibu au kama ulevi wa kawaida, lakini Tanzania kwetu peke yake mirungi ndiyo haramu. Sasa hapa lazima Serikali tulifanyie kazi kwa kina suala hili kwa sababu leo nguvu kazi ya Taifa kwa maana ya vijana kwa mfano katika Jimbo langu la Tanga wengi wako magerezani, hawapewi dhamana. Na wakati mwingine kuna watu wanatiwa hasara ya umaskini, mimi ni tajiri nitemkabidhi dereva gari au kondakta, anapakiza bidhaa mimi sijui, lakini gari likikamatwa linataifishwa hali ya kuwa mimi sikuhusika katika biashara hiyo, kwa hiyo, hili nalo Serikali pia iliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo pia lazima tufanye utafiti wa kina. Haiwezekani katika gari dereva *turnboy* na *conductor* wote wakawa wanalijua hilo tatizo. Kwa sababu pana biashara ya magendo yawezekana akawa anajua mtu mmoja tu, kwa hiyo, wengine wanapata adhabu bila ya kuhusika katika biashara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulisema, kuna dawa kama *valium*. *Valium* ni dawa inayotumika katika kupata usingizi, lakini watumiaji wa dawa za kulevya, hasa wanapokosa dawa za kulevya wanatumia *valium*. Anakwenda hospitali anasema yeye anaumwa anapewa *valium* anaitumia kama dawa ya kulevya. Sasa Serikali napo hapa hili italishughulikia vipi suala hili la kutumia *valium* kama dawa za kulevya?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni katika *sober house*, Serikali bado haijajikita hasa katika kuwatibu wanaotumia dawa za kulevya. Katika *sober house* unakuta inaanziwa na mtu binafsi au mtu anayejisikia uchungu kuona nguvukazi ya Taifa inapotea.

Mimi naishauri Serikali ihakikishe kwamba, inazisaidia *sober house* kwa kuwapa vifaa kama chakula na nyenzo nyingine ambazo zinahitajika katika vituo hivi vya kuwafanya watu waache kutumia dawa za kulevya. Pamoja na hivyo pia, kuna dawa za aina nyingi ambazo zinatumika katika kuwatibu hawa watu wanaotumia dawa za kulevya, ziwe zinapatikana kiurahisi, ikibidi ziondolewe kodi, ili jamaa zetu, ndugu zetu waweze kutibiwa warudi katika hali zao za kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nalisema kuhusiana na masuala ya dawa za kulevya ni katika masuala ya wanafunzi. Mwaka jana tulipata taarifa hapa kwamba Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) pana wanafunzi wamekamatwa na misokoto ya bangi. Sasa inakuwaje wanapata fursa ya kuweza kufanya biashara ya misokoto ya bangi ndani ya Chuo Kikuu kama Dodoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mimi naiomba Serikali napo iwe macho...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbarouk muda wako umekwisha, lakini kwa taarifa tu Mheshimiwa Mbarouk, Mnadhimu aliyeleta jina lako hapo ni Mheshimiwa Maulid Mtulia, sasa sijui mna wanadhimu wangapi huko? Lakini hamna taabu.

Mheshimiwa Riziki Lulida, dakika tano.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nikushukuru vilevile kwa kunipatia nafasi hii. Mimi ni mdau na mkereketwa wa kuwasaidia vijana ambao wanatumia dawa za kulevya. Na nitakuwa mkweli daima kuwapongeza wale wote ambao wako kipaumbele kusimamia suala la dawa za kulevya. Yeyote ambaye hajaathirika katika familia yake hatakiwi kubeza kwa vile katika nyumba nyingi akina mama wengi wanasumbuliwa na vijana wo katika suala la

dawa za kulevya; hivyo nitawapongeza wote waliokuwa katika ukereketwaji huu, iwe Mkuu wa Mkoa, awe nani, mimi kwangu namfagilia kwa *big up*, kuwa aendelee kusimamia kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea tena kuhusu *airport*. Walikuja Wakurugenzi wa TAA (*Tanzania Airport Authority*), Tanzania tuna *airport* 58, lakini tisa tu ndizo zilizo chini ya Serikali zilizobakia zote ni njia za panya, kinachofanyika kule ndani hakijulikani. Sasa jilize kama tuna *airport* 49 mimi na wewe hatujui kinafanyika nini na *airport* nyingine ziko ndani ya visiwa vidogo vidogo kama Kisiwa cha Tanzhovu, Kilwa. Sasa unajiliza sehemu kama hizi Serikali hata Mbunge hata mtu yeyote haruhusiwi kwenda pale, ni mianya ambayo ni hatari kwa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na utaangalia wazi kuwa maeneo ambayo yameathirika ni kandokando ya bahari kuanzia Mtwara mpaka Lamu. Mombasa sasa hivi imeshakufa hata hoteli zote zimefungwa kwa ajili ya biashara ya dawa za kulevya imekuwa kubwa, hivyo Zanzibar, Dar es Salaam pamoja na Tanga nao wamekuwa waathirika wakubwa wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie sana hasa njia panya za baharini katika mikoa hii. Watu wanatumia majahazi kuingiza dawa za kulevya kwa kupitia bandari bubu. Watu wanapitia katika mitumbwi kuleta dawa za kulevya kuingiza nchini, tusimamie hilo, ni eneo ambalo watu wanatumia nafasi hiyo kuiangamiza nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi, *airport* ya Dar es Salaam *VIP* wanakuja watu wengi ambao sio *VIP*; wanakuja watu unashangaa *delegation* ina watu 50 mpaka 60. Je, tunakagua wale watu kuwa wote ni *VIP*? Na mizigo yao mingi inakuwa haikaguliwi na kama haikaguliwi wanafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maeneo ambayo ni ya kuangalia. Sisi tunakwenda nchi za nje hatuthaminiwi kama

VIP, lakini anakuja mtu mchovu tu ameipata alikoipata huko *passport* yake anakuja pale anathaminiwa na anapita pale na mizigo yake bila kukaguliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikupe ufafanuzi kuhusu suala la *uplift* ya *Dar es Salaam Airport*. Unaingia ndani ya *uplift*, mgonjwa mmoja ana watu wanne wote wamembebea mizigo, unajuliza mizigo hii ya nini? Mizigo inapita katika nia ya kawaida. Halafu unafika pale chini unaambiwa *lift* haifanyi kazi, anapitishwa katika njia ya kawaida, anachukuliwa na magari kama *ambulance* na kila kitu anaondoka na mizigo ile na watu wale wanaondoka katika maeneo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba maeneo ya *airport* ya Dar es Salaam, hasa eneo la *VIP* likaguliwe kwa makini sana. Na wale wanaokuja na *passport* zao waangaliwe hivi ni kweli wote wamekuja na *delegation* ile ni watu ambao mizigo yao haikaguliwi? Ni mianya ya hatari, ni mianya ambayo inawafanya Watanzania na vijana wetu kuangamia katika suala la dawa za kulevya bila kuwa na msaada wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja katika *sober house*. Vijana wanapelekwa pale wanapewa nafasi ya kuelimishwa, lakini baada ya pale anafanya nini? Hana kazi ya kutosha, hamjamtafutia shamba akalime, hamjamtafutia mazingira ambayo akitoka pale atafanya nini. Anakwenda kukaa mtaani akiwa hana kazi, hana shughuli ya kufanya, matokeo yake yule kijana atakuwa tayari anarudi tena kurudia yale yale, hapa tutakuwa bado hatujaifanyia mema sheria hii, ili iwasaidie hao vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sina mengi, nasema ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Ruth Mollé kwa dakika saba na nusu, Mheshimiwa Lucy Mlowe kwa dakika saba na nusu, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab dakika saba na nusu.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Moja kwa moja naunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maeneo machache. Kwanza nilipenda nipate ufafanuzi, katika sheria kwenye *clause* ya 14 kuhusu kiasi cha *precursor chemicals* pale kwenye *clause* ya 3; inasema *precursor chemicals or substance with drug related effect weighing more than 100 litres in liquid form or 100 kilograms in solid form*, lakini kwingine inasema *100 kilograms below*. Vilevile inapokuja kwenye *cannabis* na *khats* kuna mahali inasema, *more than 50 kilograms*, lakini ukienda kwenye 15A inasema *below*. Sasa ningependa kufahamu kama ni vitu viwili tofauti au ni mchanganyiko?

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama tunazungumzia *below* mimi nitakuwa na mashaka sana kwamba vijana wengi sana watakwenda jela. Na nilifikiri kwamba hili suala la *drugs* lingejikita sana, kama walivyozungumza wenzangu, kwenye elimu na *counselling* kusudi vijana wajitambue waweze kuepukana n dawa za kulevyu. Kwa hiyo, ningependa kupata ufafanuzi kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mimi naona adhabu kwa watu wanaokamatwa na *cannabis* na wanaokamatwa na mirungi ni kubwa sana ukiifananisha na *cocaine*. Mimi nilifikiri kwamba adhabu yake ingekuwa tofauti kidogo, kwa sababu *cocaine* athari yake ni kubwa zaidi kuliko *cannabis* na mirungi. Na tukiangalia kwa wenzetu Wakenya wao wamehalalisha, mimi sisemi tuhalalishe, wao wamehalalisha, lakini wao wanatumia mirungi tena kama *raw material* ya kutengeneza divai, wanatengeneza *yoghurt*, wanatengeneza na *juice*. Kwa hiyo, kuna umuhimu pia wa kutazama hivi vitu kwa mtazamo mpana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, limekuja suala ambalo alilifanua Mheshimiwa Waziri. Nimefurahi kwamba hii *council* ya *drugs* au hii taasisi isiwe ndio *soul* ambayo watu wakitaka kuleta dawa, *precursor substances* na kuleta dawa ambazo

mwishowe zinatengenezewa *cocaine* au dawa za kulevya, wao sio wapewe *authority* ya ku-*import* kwa sababu, kuna *TFDA*, tuna *MSD*. Kwa hiyo, nategemea kwamba, kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri inaelekea kwamba, labda hicho kipengele kitakuwa kimerekebishwa kwa sababu kitaleta mkanganyiko mkubwa sana na urasimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni kuhusu mabadiliko ya jina kutoka *Government Chemist* na kwenda *Government Analyst*. Kwa mtazamo wangu ninaposema *Government Chemist* yaani unaelewa kabisa unazungumzia mkemia na ninapozungumzia Mkemia Mkuu unajua kabisa Mkemia Mkuu ni nani, lakini tunaposema *Government Analyst* kwa kweli mimi naona hili neno *analyst* liko *vague*; *policy analyst*, *economic analyst*, *research analyst*, huyu *analyst* ni nani? Hilo suala moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ningependa kujua kama huyu *Government Analyst* jina hili linaoana na muundo wa watumishi wa wakemia kwa sababu, wakemia wana muundo wao. Unanza mdogo, unapanda mkemia, mkemia *senior* mpaka unakuwa *principal* mpaka unakuwa Mkemia Mkuu. Ningependa kujua kuna uhusiano gani kati ya kuwa *Government Analyst* na kuwa mkemia kwa mujibu wa muundo wa utumishi wa wakemia?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshazungumzia kuhusu hiyo *cannabis*. Mimi nafikiri naomba niishie hapo na ningependa kupata ufafanuzi kuhusu hayo. (*Makofi*)

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaunga mkono hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani, pili, nachukua nafasi hii kuishukuru Kamati pamoja na wadau mbalimbali ambao wamekuwa wakivalia njuga suala hili la dawa za kulevya, lakini papo hapo nimshukuru Mheshimiwa Waziri ambaye

aliyapokea mawazo yetu ya Kamati na kuyafanyia kazi, ikiwa mojawapo ni suala la viroba, Kamati ilipolizungumzia suala hili, tunashukuru lilikubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nina masuala machache ambayo naomba niongezee. Suala la kwanza ni suala la muswada huu pamoja na suala la Uteuzi wa Kamishna wa Tume ya Masuala ya kudhibiti dawa za kulevya kucheleweshwa kuteuliwa. Serikali imechelewesha kumteua Kamishna, lakini vilevile imechelewesha kuleta muswada hapa ndani, ingewahisha kuteuliwa huyu kamishna pamoja na kuingiza muswada hapa ndani kusingekuwa na tatizo la ukiukwaji wa haki za binadamu ambao ulikuwa umejitokeza hapa karibuni wa kamata kamata kule Dar es Salaam, niki-*refer*kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambaye ameingia madarakani na kuanza kukamata kamata watu hovyoo hovyoo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ni suala la matumizi ya silaha. Sisi kama Kamati tuliona kunaweza kukawa na tatizo la matumizi ya silaha wakati wa ukamataji kwa wanaotumia na wanaosafirisha dawa za kulevya. Tulipohoji na kujadili kwenye Kamati ikaonekana kwamba wakati wa kuwakamata hawa wanaokuwa wanauza dawa za kulevya au kuingiza dawa za kulevya huwa wanakuwa na silaha, kwa hiyo, hawa wanaodhibiti watu wa dawa za kulevya wanajitahidi kuwa na silaha ili wajihami.

Naomba niishauri Serikali hawa watu wanapotumia hizo silaha watumie inapobidi au kama kuna ulazima, lakini namna nyingine naona kuna hatari na inaweza ikawa ni kichaka, wanaweza wakatumia *loophole* hiyo kwamba, kuna watu wanatumia dawa za kulevya, kumbe sivyo, kumbe ni kichaka tu. Kwa hiyo, niishauri Serikali namna nyingine kuwa makini na maafisa hawa kupata mafunzo maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niongelee juu ya kemikali ambazo sasa hivi zinatumiwa badala ya dawa za kulevya. Baada ya kukatazwa dawa za kulevya watu sasa

wamebuni njia nyingine ya kutumia kemikali nyingine ili kutengeneza dawa za kulevya. Hivyo, naishauri Serikali kujaribu kudhibiti uingizwaji wa kemikali hizo holela na hasa wale wanaotumia njia za panya, kwa hivyo, Serikali iwe makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la utata unaoweza kujitokeza wakati wa ukamataji wa hawa wanaoingiza na wanaotumia dawa za kulevya. Kwa sababu wakati mwingine mtu anaamua tu ana chuki na hila anaamua kumbambikiza mtu kesi kwamba yeye anauza dawa za kulevya au anasafirisha dawa za kulevya kumbe sio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, ninaomba suala hili Serikali iliangalie, lisitumike kisiasa, kwamba kwa sababu tu ya chuki basi mtu fulani anaambiwa huyu anauza dawa za kulevya. Wafanye kwanza utafiti kabla ya kutoa hukumu au kumchukulia mtu hatua ili kuweza kubaini kama ni kweli huyu mtu anauza au anasafirisha dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nishukuru kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab tutamalizia na Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde ajiandae.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru sana kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Muswada huu ambao ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza sana Kamishna Jenerali Siang'a kwa sababu tangu ameteuliwa kwa muda mfupi sana ameonesha kweli ana nia ya kupambana na *barons* wa dawa za kulevya. Pili nashukuru kwa Muswada huu kuja ili kuangalia na kujaza yale mapengo ambayo yanaonekana kwamba yanaweza kuathiri hizi kesi za dawa za kulevya mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu ambavyo vimeongezwa, moja ya kifungu ambacho kimeongezwa kwa kweli ambacho kilikuwa ni tabu sana; hizi kesi ndogo ambazo zilikuwa zinajaza msongamano wa mahabusu kule magerezani sasa hivi utaona kwamba *at least* vimewekewa viwango na zile kesi ndogo ambazo zilikuwa ninangojea mahakama Kuu kuweza kusikilizwa basi zinasikilizwa na Mahakama za Hakimu Mkazi au Mahakama za Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiki ni kitu cha kupongeza sana kwa sababu kamati yangu ilipokwenda kutembelea kwenye magereza, kesi nyingi ambazo zilikuwa zinasubiri kusikilizwa zilikuwa ni kesi za mauaji na za dawa za kulevya. Kwa hiyo, muswada huu umekuja kwa wakati ambao ni mzuri sana na ninaamini kabisa kwamba utapunguza msongamano ambao umejaa kule magereza wakisubiri *High Court Sessions* ili kesi hizo ziweze kusikilizwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye vifungu. Kifungu cha 15 ambacho ni *para eight*, kifungu hiki kimeanisha makosa ambayo watuhumiwa wakionekana na hatia basi watakwenda magerezani maisha.

Sasa kifungu cha 15(1)(iii) ambacho kimetaja makosa ambayo watakwenda magerezani, utaona pale kwenye kifungu hicho ukianza mwanzo kwamba *narcotic drugs, psychotropic substances* ambazo zinazidi kiwango cha gramu 200 basi huyo mtu atakwenda kufungwa maisha. Pia kuna *precursor chemicals or substances* ambazo zitazidi lita 100 na yenyewe atakwenda kufungwa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu unakuja pale *cannabis* na *khats* ambacho wanasema kwamba ukikutwa na *cannabis* (mirungi) au bangi zaidi ya kilo 50 ni *trafficking* lakini unakwenda kufungwa maisha. Sasa imenipa wasiwasi kwamba huku tumeondoa kesi zile ndogo na inanipa wasiwasi kwamba tunapoingiza kifungu hiki maana kilo 50 za mirungi na bangi *trafficking* ni kiwango kidogo sana

ambacho watu wengi sana watakatwa na tutarudia makosa yale ya kupeleka watu gereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka wahusika waangalie kifungu hicho kwa makini kwa sababu kitarudisha tena msongamano na ile mantiki ya kupunguza msongamano na kuweka madaraka kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi itakuwa imepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, nilitaka hilo liangaliwe na liweze kuonekana kwamba ni kitu cha muhimu sana. hii ni kwa sababu ukiangalia kwenye 15A imeeleza kabisa kwamba *less than 50 kilograms* kwamba basi *RM's Court* zitaendelea kusikiliza hizo kesi. Kwa hiyo labda ingeendelea iangalie ifanyiwe marekebisha ya kifungu 15A kuweza ku-*accommodate cannabis* pamoja na *khats* kwa sababu kimejumlisha hizi *hard drugs* na hizi *drugs* nyingine za kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, *hard drugs* maana yake ni hizi *cocaine, heroin, mandrax* na kila kitu; sasa zile *effects* zake ni kubwa sana na pia bei zake ni kubwa sana ukilinganisha na mirungi na bangi, kwa hiyo ni vitu viwili tofauti ambavyo sasa vimekuwa *grouped* kwenye sehemu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninaona ni la muhimu sana ni kwenye para ya 22 kifungu cha 48(2) ambacho kimetoa madaraka *of course* kwenye rekodi ya *interrogation* au *interview, caution statement* kuchukuliwa na kuweza kukubalika ukiongezea uzito na hiyo *electronic equipment* ambayo itaongeza uzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa niliona kwamba kui-*separate* ile *alternative* ya *caution statement* kwa sababu *caution statement* inataratibu zake ambazo kama imetolewa kwa *inducement* au *threat* basi *trial within a trial* inabidi iingie na inaweza kuwa na *process* ndefu. Kwa hiyo, tutakapoweka *paragraph* nyingine tofauti ambayo itampa Kamishna Jenerali au yule afisa kuchukua maelezo kama ni *alternative* ili iweze kukubalika moja kwa moja mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, *para* nyingine ambayo nimeiona ina matatizo ni para ya 31 kifungu cha 53 ambacho kinampa uwezo *Commissioner General* kuweza ku-*forfeit any illegal properties* ambazo anazona kwamba labda zimepatikana kwa njia isiyo ya halali. Kwa hiyo, niliona kwamba *illegal properties* ambazo zimepatikana *through drugs* labda kuongeza na *abandoned* ambazo zimeweza kutupwa au wenyewe wamekimbia bila kuwa na wenyewe basi na yenyewe apewe madaraka aweze kuzi-*forfeit* kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni suala la mali ambazo zipo nje ambazo zinaonekana zimepatikana kwa njia ya *drugs*. Hili suala *of course* linatakiwa ku-*invoke registration* ya *mutual assistance* ambayo lakini hii inahitaji sana *bilateral agreements* ambazo itakuwa ni ngumu sana lakini nimeona kifungu kimoja ambacho kinaonyesha ushirikiano na *other law enforcing agencies*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri *Commissioner General* ajaribu kuingia kwenye *MOUs* na hizi *law enforcing agencies* ambazo *already* zina *contact* nje ili kama inapobidi kuweza kurudisha au kuzichukua hizo mali waweze kuwasiliana na wao ambao wana *contact* nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ni suala la huku kwenye *schedule* kuna mabadiliko mbalimbali ambayo yanaweza kuwa ni makosa tu sababu ya kazi nyingi, lakini nilitaka yaangaliwe kuanzia fomu ya kwanza, pili, tatu na ya nne. Isipokuwa hii fomu ya nne nilitaka kwa *seizer* wale watuhumiwa ambao wanameza madawa ya kulevya na kuyatoa basi eneo la kuonyesha kwamba kuna shahidi ambaye ameshuhudia kwamba ameona huyo mtuhumiwa akitoa hizo nani ili iweze kuongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Lucy Mayenga atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, halafu Mheshimiwa mtoa hoja ujiandae.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia hii nafasi. Vilevile ninaomba kwa nafasi ya pekee nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ambaye kwa kweli kwa kiwango kikubwa yeye ndiye aliyesababisha mpaka leo hii Tanzania kwenye vita hii tumeweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa msimamo mkubwa alionao dhidi ya vita hii. Vile vile kwa nafasi na upendeleo wa kipekee nimpongeze Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya, Kamishana Siang'a, ninampongeza sana. Ninampongeza sana kwa sababu anafanya kazi na amefanya kazi kubwa sana, ndani ya muda mfupi na katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamishna huyu ndiye yule ambaye alikataa rushwa ya shilingi milioni 800. Kwa kweli ni kitu ambacho kwanza ni nadra maana hata katika hali ya kawaida unaona kabisa kwamba kama ni mtu ambaye si mzalendo na hauna uzalendo wa dhati kutoka moyoni mwako, ni kitu ambacho ni kigumu sana, kwa hiyo ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninampongeza kwa sababu alifanya kazi hii katika mazingira magumu sana ya sheria; alifanya kazi hii katika mazingira ambayo sheria hii ilikuwa haitumiki Zanzibar, katika mazingira ya sheria ambayo yalikuwa hayaruhusu mamlaka hii kumiliki silaha, mazingira ambayo hata yeye mwenyewe kuweza kutaifisha na kufanya mambo mengine yote ili kuweza kukabiliana na hawa wauzaji wa dawa za kulevya ilikuwa haiwezekan lakini aliweza kupambana na hatimaye sasa hivi kwa kweli watu wanasema kwamba misuli imekaza lakini kwa hawa wauzaji wa dawa za kulevya imekaza zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie kwenye suala hili la dawa za kulevya kwa upande wa Zanzibar. Mimi nilikuwa

ninategemea kwamba leo Wazanzibari wote wangukuwa na kauli moja kwamba sheria hii wanaiunga mkono kwa asilimia 100 bila kusita. Nasema hivyo kwa sababu matatizo haya ya madawa ya kulevya athari zake ukiachilia mbali athari za kijamii kwa maana ya kwamba maradhi na nyingine lakini ina athari kubwa sana... *(Makofi)*

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. LUCY T. MAYENGA: ...kwenye masuala ya uchumi...

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy Mayenga kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mattar.

T A A R I F A

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. nimpe taarifa dada yangu Mheshimiwa ambaye alikuwa akizungumza hapa, sisi kama Wazanzibari Sheria hii, Tume hii na Muswada huu tumeuridhia, tumeukubali asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimueleze tumeshakubaliana, tumewahi kuzungumza si mara moja wala mara mbili kuwa suala hili tunamwambia Kamishna wa Dawa za Kulevya aweze kufanya kazi Zanzibar kwa kadri anavyoweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kama Wazanzibari tunataka, tunaupenda na tunajua kama tuna shida kubwa na matatizo tuliyonayo Zanzibar. Kwa hiyo tunamuomba sana na tunaiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iweze kufanya kazi kwa nguvu zote kwa kushirikiana na Tume ya Zanzibar... *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mattar, Mheshimiwa Lucy Mayenga unaipokea taarifa hiyo.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, yeye alikuwa ni sehemu ya Wazanzibari, lakini hasa nilikuwa nimem-*target* Mheshimiwa Ally Saleh kwa sababu naye pia ni Mzanzibari. Kwa hiyo, kwa wale ambao wanaunga mkono sheria hii tupo pamoja, lakini kwa wale ambao hawaungi mkono kwa sababu pia wewe unaweza ukawa ni mmojawapo, lakini kuna wenzenu pia hawauingi mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kusema mengi lakini ninachotaka kusemea ni kwamba hata kama tunaunga mkono sisi viongozi na sisi ambao ni Wabunge Wazanzibari tuliopo humu ndani, ninaomba sasa maana yake nilikuwa sitaki kusema lakini ninaomba kwenda mbele zaidi. Ninaomba tufanye kazi ya ziada kwa tume ya kudhibiti na kupamba na madawa ya kulevya Zanzibar. Imeunda zaidi ya miaka kumi, lakini mpaka sasa hivi haijakamata hata kilo tano, naishia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala haya ya madawa ya kulevya yana athari nyingi sana. Zipo nchi ambazo zimekuwa zikifadhiliwa kutokana na athari hizi za dawa za kulevya zimeingia kwenye matatizo makubwa sana kisiasa, kiuchumi na nyingine pia zimepinduliwa. Nchi kama Nicaragua, Panama, Mexico na kadhalika na wengi pia mnajua historia hizo, wapo katika hali ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo vita hii ninaomba wote tuwe na kauli moja kwa sababu vita hii inahusu kuanzia wale wadogo ambao ni watumiaji lakini hata na sisi pia wakubwa. Kwa sababu ambao wamekuwa wakikamatwa mara nyingi huko wanasemwa sana, lakini bado miongoni wetu kuna watu ambao baadhi yao wapo katika nafasi mbalimbali, si lazima wawe Wabunge ni watu ambao wapo katika nafasi kubwa lakini wamejiingiza kwenye biashara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba kupongeza sana sheria hii na kwa kweli ninaomba serikali kwenye utekelezaji wa sheria hii isimuangalie mtu usoni, awe mtoto wa mkubwa, awe mwenyewe ni mkubwa awe sijui ni nani, tuangalie na tuweze kuchukua hatua zinazostahili. Haiwezekani watu walikuwa wamefikia kiwango cha kuingiza katika nchi yetu mpaka *tons as if* ni unga wa mahindi, haiwezekani. Kwa hiyo, sheria hii ikate kotekote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeskiliza kuhusu taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu suala la kifungu cha dhamana kwamba ile kupunguza gramu. Ili mtu alewe kutokana na unga anatakiwa atumie 0.01 gramu ya unga ndipo analewa. Sheria iliyopita ilikuwa ni kwamba mtu akikamatwa na madawa ya kulevya haya ya viwandani, *heroin* au *cocaine* ikiwa ni chini ya gramu 200 anapata dhamana, sasa nini kilichokuwa kinafanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichokuwa kinafanyika ni kwamba wafanyabiashara walikuwa gramu 200 anazigawa kwa watu tofauti tofauti, kwa sababu anajua kwamba akikamatwa na gramu 200 au zaidi mtu mmoja itakuwa ni matatizo. Gramu 200 anaweza kutengeneza, gramu moja ya dawa za kulevya inatengeneza kete 100 kwa maana hiyo gramu 200 ni zaidi ya kete 20,000...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lucy Mayenga kwa mchango huo. Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kwanza kabisa kuwashukuru Wabunge wote ambao mmechangia katika muswada huu kwa namna ambavyo mmeguswa na ukubwa wa jambo hili na kuona umuhimu

wa sheria ambayo ipo mbele yetu hasa katika kukabiliana na changamoto hiyo kubwa ya dawa za kulevyaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa kwamba changamoto hii inagusa kundi kubwa sana hasa la vijana ambao ndio nguvukazi ya Taifa hili. Hivyo, kwa hiki ambacho kinafanyika hivi sasa, kwa maana ya sheria hii itasaidia sana katika kupambana na udhibiti na lengo la kuiondoa jamii yetu katika changamoto hii kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda moja kwa moja katika hoja ambazo zimekuwa *raised* na Waheshimiwa Wabunge hapa na nikianza na ya kwanza, Waheshimiwa Wabunge katika michango yao wamzungumza kuhusu matumizi ya baadhi ya maneno na moja wapo ilikuwa ni neno *control*, mapendekezo yalikuwa ni kulifuta neno *control*.

Mheshimiwa Naibu Spika, neno hili *control* ambalo kwa mujibu wa marekebisho haya tuliyonayo, neno hili limeongezwa kati ya maneno *drug* na *council* ili liendane na jina lenyewe ambalo ni tunasema ni Baraza la Kudhibiti Dawa za Kulevyaa (*National Drug Control Council*), ndiyo maana hii *control* haina namna kuiepuka, na lazima liwepo ili kwenda kukamilisha hasa jina lenyewe la Baraza la Kudhibiti Dawa za Kulevyaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine ambayo ilikuwa *raised* pia hapa ya masuala ya kuondoa neno *institution* na badala ya kusema tu taasisi, lakini taasisi hizi zitajwe kwenye sheria. Neno taasisi kama lilivyosemwa hapa kwenye sheria ukiliondoa na ukaanza kuzitaja moja moja, katika utekelezaji wa sheria italeta ugumu mkubwa sana, hii ni kwa sababu katika zile *techniques* za kwenda kutafsiri sheria iko rule moja ambayo inasema kwa lugha ya kilatini *expressio unius est exclusio alterius* maana yake ni kwamba *the express mention of one thing is the exclusion of the other*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizitamka leo zile taasisi pale *specifically*, ikija kutokea jambo limefanyika katika taasisi moja ambayo haijatajwa na sheria *then* maana yake pale

umeshajishindishwa mwenyewe sheria inajishinda yenyewe. Ndio maana tunaendelea kuona kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa neno *institution* liendeleo kubaki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Waheshimiwa Wabunge walichangia katika hoja ya kusema kwamba lazima tutoe elimu kwanza na badala yake tuibadilishe hii sheria isiwe ya adhabu sana lakini pia tufanye na masuala ya elimu. Ni dhahiri kwamba na ninyi Waheshimiwa Wabunge mnafahamu, mamlaka hii imefanya kazi kubwa sana kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali katika kutoa elimu na kuwafanya watanzania kuelewa madhara makubwa ya matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo si kweli tu kwamba tunafanya kazi ya kukamata tu lakini pia tunaelimisha umma wa Watanzania ili wafahamu madhara makubwa ya matumizi ya dawa za kulevya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia imezungumzwa hoja hapa ya kwamba kuna mianya ya kuingiza dawa za kulevya na sheria hii sasa iangalie namna bora ya kuweza kudhibiti. Ukiangalia katika marekebisho ambayo yamefanyika hapa, zamani katika namna ya kupambana na dawa za kulevya, kwa maana ya udhibiti wake tulikuwa tunaainisha njia kadhaa *especially* katika maeneo ya bahari, kwa maana ya majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika mapendekezo ambayo yanakuja hapa sasa tumefanya mabadiliko. Tumetumia maneno *conveyance* ambayo sasa *it's a broader term* ambayo ina-cover zaidi ya yale ambayo tulikuwa tukiyasoma pale awali, kwa maana ya masuala ya majini peke yake. Kwa hiyo, hivi sasa tunazungumzia pia katika viwanja vya ndege ambavyo vilisemwa hapa kama sehemu ya mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia imezungumzwa hapa hoja na Mheshimiwa Ruth Mollé, alitamani kufahamu na kupata ufafanuzi wa Serikali kuhusu matumizi ya maneno

Government Chemist na *analyst*. Kwa nini tumekwenda katika *Government Analyst*; tumekwenda huko kwa sababu tumefanya hivi ili yaendane na sheria nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ukae kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, nakusudia kuongeza muda kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2), sasa nitawahoji, kwa sababu Kanuni inataka niwahoji.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Muda umetajwa kwenye Kanuni Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunasoma Kanuni. Nimewatajia Kanuni ya 28(2), msipige kelele tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Waziri, malizia hoja yako.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ilikuwa ni katika kuonesha utofauti wa kwa nini tunaendelea kusema litumike neno *analyst*.

Mheshimiwa Naibu Spika, neno *analyst* ndilo neno ambalo linatumika kwenye baadhi ya sheria ambazo zinafanya azi pamoja na sheria hii. Moja kati ya sheria ambayo neno hili la *analyst* linatumika ni pamoja na *The Criminal Procedure Act*, lakini vilevile katika kifungu namba 13(1) cha Sheria ya *The Government Chemistry Laboratory Act* ya mwaka 2016, maneno yaliyotumika ni *analyst*.

Kwa hiyo, neno *analyst* ndilo neno sahihi hasa katika muktadha wa sheria hii, na ndiyo maana tuliona kwamba bado kuna umuhimu wa kuendelea kutumia neno *analyst* ili iendane na sheria nyinginezo ikiwemo hiyo *CPA* ambayo

nimeitaja, na Sheria ya *The Government Chemistry Laboratory Act* ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nakushukuru sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Mtoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwanza kabisa naomba nikushukuru wewe kwa kuongoza vizuri kikao hiki leo. Kikao hiki leo ni kikao cha kuunga mkono juhudi za mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania, kwa hiyo nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii, lakini kwa dhati ya moyo wangu niwashukuru wale wote ambao wametupa marekebisho na wameiunga mkono hoja hii, ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nitakwenda moja kwa moja kwenye hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na maoni ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulikia Masuala ya UKIMWI na inayoshughulikia pia masuala ya dawa za kulevya. Kamati ilitupa maoni mengi na iliomba Serikali ifanye marekebisho katika ibara mbalimbali. Naomba kulihakikishia Bunge lako kuwa tulichukua ushauri wa Kamati na tumeleta jedwali la marekebisho la Serikali, kwa hiyo tunaunga mkono maoni ya Kamati katika kufanya marekebisho ya Muswada wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitushauri kwamba kuna umuhimu wa kuongeza nguvu kama Serikali

katika kuhakikisha tunapambana na biashara hii haramu ya dawa za kulevya kwa upande wa pili wa Zanzibar. Naomba niliarifu Bunge lako tukufu kwamba tumeanza utaratibu huo vizuri; mimi mwenyewe nimeshafanya kikao cha kwanza na Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar katika kuhakikisha kwamba tunaongeza nguvu za pamoja kwenye mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, niliagiza Mamlaka yetu ikutane na Mamlaka ya Zanzibar ili itengeneze mpango mkakati ambao sasa utatumia nguvu za Bara na Visiwani kwa pamoja katika kuhakikisha kwamba jambo hili linafanyiwa kazi ipasavyo. Ninaomba kuliihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, na mimi kama Waziri mwenye dhamana nitafuatilia mkakati, huo na ninawahakikishia Wazanzibari kwamba tutafanya kazi sambamba, bega kwa bega mpaka tuhakikishe kwamba vita hii inatokomezwa sio Bara tu, hata upande wa pili wa Visiwani, kwa sababu lengo ni kuwaokoa watoto wetu wote wa pande zote mbili za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilisema kwamba hii sheria si sheria rafiki, Sheria hii inaweka adhabu kali na kwa kuweka adhabu kali itapandisha thamani ya biashara ya dawa za kulevya na hivyo basi hakutakuwa na manufaa makubwa kwa sheria hii katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niseme yafuatayo; kwanza, kama biashara hii itakuwa imepanda thamani kwa maana itakuwa ni biashara aghali, ina maana wale wafanyabiashara wanaojihusisha na dawa za kulevya wao ndio watakaolingia kwenye matatizo kwa sababu biashara itakuwa ni ghali kuliko ilivyo nyepesi kwa sasa, na kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumewaondoa Watanzania wengi sana katika kufanya biashara hii ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa jinsi sheria ilivyo, kama biashara itakuwa aghali ina maana hata wale wamiliki wa biashara itabidi wawe na bidhaa nyingi na wazinunue

kwa wingi ndipo waweze kufanya biashara hii. Sheria yetu sasa imeweka sasa masharti; kadiri utakavyokamatwa na mzigo mkubwa, ndivyo adhabu itakavyoendelea kuwa kubwa na itakushughulikia kweli kweli. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwa mabadiliko haya ya sheria itatusaidia sana kupunguza matumizi na biashara ya dawa za kulevya katika nchi yetu, lakini kwa kufanya hivi itaondoa upatikanaji wa dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania na hivyo tutaweza kuleta ustawi wa watoto wetu na ustawi wa uchumi wetu na wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kabisa matumizi ya dawa yanavyoongezeka ni kiashiria pia cha kuongezeka kwa tatizo la UKIMWI katika nchi yetu ya Tanzania, na hasa kwa wale wanaojidunga sindano za dawa za kulevya. Kwa hiyo naomba Waheshimiwa Wabunge tuungane kwa pamoja tupitische sheria hii leo tukapambane na dawa za kulevya na matumizi yake katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Upinzani wamesema hapa kwamba Sheria hii imejaa sana kusisitiza katika kuwahibiti wafanyabiashara wadogo wadogo badala ya kutoa tiba, lakini vile vile kutoa elimu. Naibu Waziri amejibu kwenye suala la elimu, na mimi naongezea kwamba kifungu cha 4(1)(e) kinaipa kazi kabisa Mamlaka yetu kutoa elimu kuhusu suala hili la dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye suala la tiba, ninaomba kwa dhati niipongeze Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini; kwa sababu kifungu cha sheria mama, kifungu cha 63, kimeagiza kabisa mamlaka ishughulikie pia suala la kuanzisha vituo vya tiba katika nchi yetu ya Tanzania vya kupunguza uraibu. Na ninaomba niliarifu Bunge lako Tukufu, toka mamlaka hii imeanza kufanya kazi tayari vituo hivi vya tiba vimeshaanza kuongezwa katika nchi yetu ya Tanzania, tunafungua kituo kingine hapa Dodoma kwa sababu hapa tatizo ni kubwa sana, na hizo ni juhudi za Mamlaka, na ninaomba kwa kweli tuwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunakwenda kufungua kituo kingine cha tiba kule Mwanza, kitakuwa ni kituo kikubwa na chenyewe kitatoa sana msaada wa tiba, tuwapongeze kweli mamlaka. Vile vile tutafungua kituo kingine cha tiba ya *methadone* kule Mbeya, na hivyo unaona kabisa kwamba tumekwenda kusambaa katika majiji makubwa, ukiacha vituo vitatu vikubwa ambavyo tunavyo mpaka sasa pale Dar es Salaam. Kwa hiyo, kama ni suala la tiba tunafanya. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, kutokupitishwa kwa sheria hii sababu isiwe ni tiba, tiba tunafanya na tunawahudumia vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema hii sheria ingegharamia sana kwenye suala hilo la tiba, naomba niwaarifu Waheshimiwa Wabunge yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio kwa mfano kwa mwaka 2016 kwenye tiba ya *methadone* ilikuwa ni kilo 120 kwa mwaka na kwa mwaka 2017 ilikuwa ni kilo 300 na kilo moja ya kuweza kutoa tiba kwa wagonjwa hawa inauzwa dola kwa chini kabisa ni dola 650 lakini kwa bei ya juu ni dola 1,500, kilo moja. Sasa kwa mwaka 2016 peke yake tumetumia takribani dola 180,000 na kwa mwaka 2017 tunakadiria kutumia dola takribani 450,000 kwa ajili ya kununua dawa hii na kutoa tiba kwa vijana wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni juhudi zimefanywa na malaka na sasa hivi mamlaka wameamua kununua dawa hii moja kwa moja kutoka India na tukifanikiwa kufanya hivyo tutapata dawa nyingi. Lengo ni kuongeza vituo vingi zaidi kwenye nchi nzima ya Tanzania na tiba iwakute vijana wengi na Watanzania wengi, tuweze kuondoa uraibu kwa Watanzania ambao wameshaathirika na dawa za kulevya. (Makofi)

Kwa hiyo, naomba niwapongeze sana tume kwa kazi hii nzuri ambayo wameendelea kuifanya na wanaifanya vizuri sana na hata Kamati imeshawahi kwenda kuangalia wanavyofanya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 29, Waheshimiwa Wabunge wanasema kwa nini tumekiweka; kifungu hicho cha 29 tunapendekeza kufanya marekebisho kwa lengo la kuongeza makosa yasiyostahili dhamana ambayo yatajumuishwa katika makosa ya kumiliki mitambo na kutengeneza dawa za kulevya, kufadhili biashara ya dawa za kulevya na kuwaingiza watoto kwenye biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule mwanzo makosa haya yalikuwa hayajaingizwa kisheria kama ni makosa ambayo hayastahili dhamana. Unaweza ukaenda ukakuta mtu ana mtambo wa kutengeneza dawa za kulevya kutokana na kemikali bashirifu, na anapopatwa hatia mahakamani kwa sababu sheria haijafunga kupata dhamana alikuwa anaashiwa mahakamani anapata dhamana na anaweza kwenda kucheza na kesi yake kwa namna moja ama nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, tumegundua mwanya huu umetumika vibaya sasa tunafunga dhamana kwa watu hawa wote. Kwa hiyo ukikutwa tu na kosa la kumiliki mitambo inayotengeneza dawa za kulevya hakuna dhamana mpaka kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukikutwa pia unawashirikisha watoto kwenye biashara ya matumizi ya dawa za kulevya, kosa hili halina dhamana. Kwa hiyo, tunataka tuwalinde watoto wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 4(2) kama nilivyosema, tunakirekebisha ili kuipa mamlaka nguvu ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya, si kushughulikia tu makosa ya dawa za kulevya bali tunataka pia mamlaka ishughulikie na makosa mengine yanayohusiana na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, mamlaka inapokwenda kufanya kazi zake labda za operesheni huko maeneo mbalimbali, inaweza ikafika mahali

ina taarifa kwamba pana dawa za kelevya, na hiyo *experience* wameshaipata, lakini wanapofika pale wanagundua kwamba pamoja na kuwa pale mahali pana dawa za kulevya, lakini inawezekana pana dhahabu *fake* ambazo zimewekwa hapo, maana wafanyabiashara wanaofanya biashara ya dawa za kulevya wanafanya pia na biashara nyingine haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukafika hapo ukawakuta pia wana pembe za ndovu ziko hapo, ukakuta na vitu vingine tu ambavyo vinamilikiwa kinyume cha sheria hata kama ni silaha na vitu vingine. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono, tunaipa mamlaka sasa nguvu, ikikuta hakuna dawa za kulevya lakini kuna pembe za ndovu watachukua hatua kwa kushirikiana na vyombo vinavyohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano wakati wanafanya operesheni zao, walifika mahali wakakuta dawa za kulevya zimetoroshwa lakini wale watu wanamiliki dhahabu feki ambayo walitaka kuiuza kwa siku hiyo hiyo mamlaka ilipokwenda hapo; na biashara nyingine tu za hovy, hata bidhaa ambazo ni mbovu ambazo hazina viwango. Kwa hiyo tumewapa mamlaka sasa watafanya kazi hiyo yote, wapeni hilo rungu wakafanye kazi, watatusaidia sana katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongelea pia katika kifungu cha 51(a) tunataka kumpa uwezo Kamishna Jenerali kushikilia akaunti za watuhumiwa kwenye benki mbalimbali. Unapomkamata mtuhumiwa lakini hujamuwekea utaratibu wa Kamishna wa kuweza kuzuia fedha ya mtuhumiwa kwa muda fulani wakati anafanya upelelezi, tulichogundua ni kwamba watuhumiwa wengi wamekuwa wakihamisha zile fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine. Na wanapozihamisha, wanazitakatisha fedha zile kwa matumizi mengine. Kwa hiyo sheria inakwenda kubana mianya hiyo yote, na sasa kwa kweli tunataka tuwe na nidhamu ya kutosha katika nchi yetu ya Tanzania, na hasa kwenye suala zima hili la biashara ya dawa za kulevya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeulizwa hapa kwa nini mnawapa mamlaka makubwa sana mamlaka hii mpaka wanafikia hatua ya kumiliki silaha. Mimi naomba Waheshimiwa Wabunge kwanza tukumbuke sheria mama ya mwaka 2015 ilipokuwa inatungwa iliweka kazi za mamlaka katika kifungu cha saba cha sheria mama, lakini ika-*define* pia kazi za Kamishna Jenerali wa Mamlaka hii ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapokwenda kwenye shughuli za mapambano dhidi ya dawa za kulevya mahali popote, hebu wote tujjulize tu; hawa wanaofanya biashara ya dawa za kulevya wanajikinga na silaha kubwa, wakati mwingine usiku mnapata taarifa na mnataka mkafanye *operation* na uvamizi mahali, mnakwenda kukutana na mtu mwenye silaha kubwa, lakini kwa sababu mamlaka haina mamlaka ya kisheria kumiliki silaha, wakati mwingine watumishi wa mamlaka wamekuwa wakijitosa kwenda bila kuwa na silaha hata moja na kuhatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoweka kifungu hiki sasa tunataka mamlaka izeze kumiliki silaha zake na itakapokuwa inakwenda kwenye mapambano iende ikiwa imejitosheleza Waheshimiwa Wabunge na wala lengo sio kwamba mamlaka itatumia silaha hizi vibaya, hapana, sheria inawaruhusu makampuni ya ulinzi kumiliki silaha na kulinda kwa kutumia silaha, kwa nini tusiruhusu chombo kikubwa kama hiki na chenyewe kikawa kinamiliki silaha kiende kikatusaidie katika mapambano haya dhidi ya dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, naomba mtuunge mkono, mapambano haya ni makubwa yanahitaji weledi, lakini yanahitaji kujitoa na usalama wa kutosha kwa watumishi ambao wanafanya kazi hiyo kwenye mamlaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeelezwa hapa ni kwa nini sasa Sheria yetu sisi inapingana na mikataba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Msemaji wa Kambi ya Upinzani amesema

ukienda kule Kenya mirungi inaruhusiwa ukija huku kwetu hairuhusiwi. Nataka tu niwape uzoefu wa nchi za Afrika Mashariki. Nchi ambayo inaruhusu matumizi ya mirungi nadhani ni moja tu, ni Kenya, Uganda hawaruhusu na nchi nyingine kadhaa ikiwemo Tanzania hawaruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi niwaulize Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa Kenya wanaruhusu mirungi, ambayo sisi tunajua ni aina ya dawa za kulevya, itumike kwao isiwe ni kigezo na sisi Tanzania turuhusu wakati tunajua inaweza kuwaathiri watoto wetu kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, sisi tutaendelea na utaratibu wetu, tutaendelea kushauriana na nchi za jirani waone umuhimu wa kuwakinga vijana wote wa Afrika Mashariki waondokane na janga hili kubwa la dawa za kulevya. Serikali zetu zitaendelea kuongea, lakini kwetu bado tunaamini kwamba jambo hili haliwezekani na tutaendelea kulisimamia kama jambo ambalo haliwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imeulizwa hapa, pamoja na kudhibiti aina hizo zote za dawa za kulevya, lakini zipo kemikali na dawa nyingine zinaweza zikawa zinatumiwa kama dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania. Sheria hii inampa sasa mamlaka Waziri mwenye dhamana kuendelea kuorodesha majina ya dawa na kemikali zozote zile ambazo tunaona kwamba zinaweza kutumika kama dawa za kulevya nchini na zenyewe zikawekwa katika jedwali na zikaelezwa kama ni dawa ambazo hazitatakiwa kutumika bila utaratibu katika nchi yetu ya Tanzania zikiwa chini ya jedwali ambalo linaorodhesha kemikali ama dawa ambazo zinaeleweka kama ni dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Lucy Mayenga, ametupa ushauri mzuri pia naye, na kwa kweli ametueleza hapa kwa kina ni kwa kiasi gani tunatakiwa kupambana kwa nguvu zote, na amewapongeza sana mamlaka kwa kazi nzuri wanayoifanya, na mimi nakushukuru sana Mheshimiwa Lucy, na

tunayachukua yote uliyoyasema kama ni kumbukumbu sahihi ya kuyafanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dada yangu Lucia Mlowe amesema tumechelewa kuleta sheria hii. Naomba nimwambie hatujachelewa, imepitishwa mwaka 2015 na mamlaka imeundwa hivi karibuni tu; lakini umeona mamlaka ilivyoanza kufanya kazi na baada ya kugundua kwamba yako maeneo ambayo si rafiki kwa mamlaka kufanya kazi leo tumeleta kufanya marekebisho na ninaamini baada ya marekebisho haya kazi itakuwa nzuri zaidi Mheshimiwa Lucia tutakuja mpaka kule Njombe na unajua tatizo la Njombe lilivyo; tutakuja kushirikiana na ninyi huko ili tuweze kusaidiana. Kwa sababu UKIMWI unaenda sambamba sana na matumizi ya dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameeleza suala la *RC* wa Dar es Salaam kujishughulisha na ukamataji. Waheshimiwa Wabunge naomba niwaambie kwamba jamani vita hii ya dawa za kulevya ni ya kila Mtanzania, kila Mtanzania afanye kazi hii. Tusioneane wivu wala tusipambane wakati tunajenga nyumba moja kwa kutumia fito zinazofanana. Cha msingi kila anayefanya kazi hii aheshimu sheria inayotuongoza katika kupambana na matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania wote, kazi ya kupambana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania ni ya Watanzania wote; haibagui wala haichagui nani afanye nani asifanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Adadi na nadhani kuna vifungu ambavyo tumeelewana na vifungu vingine tunafikiri tutaviacha kama vilivyo, lakini umezungumza sana sana kifungu cha (15) na una hofu ukubwa wa mzigo na hasa katika matumizi ya biashara ya bangi na mirungi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ninaomba tu niwaambie jambo moja kwamba hawa wafanyabiashara walipoona kwamba sheria haiwabani

kuwa na kiasi kidogo kidogo cha dawa walichoamua kufanya mtu analima shamba la bangi labda magunia 1000, lakini anajua ilimawe salama asikamatwe anagawa yale magunia 1000 katika viwango vidogo vidogo na anaviweka kwa watu mbalimbali. Kwa hiyo, hiyo sasa ilikuwa inatoa hamasa ya mtu kuwa na mmiliki wa dawa za kulevywa nyingi lakini anazigawa katika mafungu madogo madogo, akikamatwa ana dhamana lakini sheria inayomkamata haina makali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tumesema kamata mtu huyo zaidi ya hizo kilogram tulizosema tunafunga huko maisha. Kwa hiyo kila mtu aone kwamba matumizi na biashara ya dawa za kulevywa katika nchi yetu ya Tanzania hatuna mchezo nayo na sheria tumeiweka kuwa kali na sheria hii kwakweli tunataka ishughulike na kila mtu anayetaka kuharibu maisha ya kizazi cha Watanzania uchumi wa nchi yetu na mafanikio na mwelekeo wa maadili katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yaliyoulizwa ni mengi, kwa hiyo mengine tutaendelea kuyajibu kwa maandishi lakini nimalizie kwa kusema tunawaomba sana, sana, sana Waheshimiwa Wabunge mpitische Sheria hii leo muwape mamlaka ya kudhibiti ya kudhibiti dawa za kulevywa katika nchi yetu ya Tanzania wafanye kazi ya kuokoa kizazi cha Tanzania leo na kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa toa hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja Ilitolewa lamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono; Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na utaratibu ulio mbele yetu; Katibu.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:

**Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti
na Kupambana na Dawa za Kulevya wa Mwaka 2017
(The Drug Control and Enforcement (Amendment)
Bill, 2017)**

Ibara ya 1

Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

MWENYEKITI: Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta mabadiliko kwenye kifungu hiki cha 8(3). Makosa ambayo yameorodheshwa hapa kwa majili ya *trafficking* ambayo ni *narcotics drugs psychotropic substances, precursor chemicals*; na wametaja kwamba *narcotics* ambazo zitakuwa *more than two hundred grams* ni unafungwa maisha. *Precursor chemicals* zinazozidi lita 100 unafungwa maisha; *cannabis na khat* (mirungi na bangi) ambayo inazidi kilo 50 unafungwa maisha, *trafficking*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba kwamba makosa haya yamechanganywa, yaani *hard drugs* zimechanganywa na haya makosa mengine ya mirungi na bangi. Sasa tutakapoamua kumfunga huyu mtu wa ambaye ana-*traffic* bangi na milungi kilo 50 zaidi maisha naona ni adhabu kali sana. Kwa hiyo, nilikuwa nikifikiria kwamba ni vizuri tuangalie vinginevyo ile *purpose* ya kuja za watu magerezani itarudi vilevile kama ambavyo tunataka kupunguza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja.

WAZIRI WA NCHI, WAZIRI YA MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba sana Mheshimiwa Adadi atukubalie hiki kifungu kama kilivyo kibaki kama kilivyo sababu ni zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati mamlaka ilivyoanza kufanya kazi zake rasmi, jambo moja

tuliloligundua lilikuwa ni kwamba hawa wafanyabiashara wanaolima mirungi, wanaolima bangi; na mmeona tuna *operation* kubwa za uteketezaji wa bangi katika nchi yetu ya Tanzania; kwa sababu sheria ilikuwa haina makali kwa viwango vya umiliki wa bangi na mirungi; kwa hiyo wao walichokuwa wanakifanya wanaweza wakazalisha kwa wingi lakini wanagawa kwa mafungu madomado na kuwagawia vijana wengi zaidi wamiliki na waendeleo kufanya biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kufanya hivyo tatizo lilikuwa halijatibika, na mamlaka imegundua kwamba hawakuwa na uoga wowote. Kwanza sheria ilikuwa hata wakitiwa hatiani dhamana ilikuwa wazi kwa sababu pia ya kumiliki kiasi kidogo kidogo. Sasa tunasema tuwafuate kwenye kiasi hicho hicho kidogo kidogo na tuweke sheria kali na tukiweka sheria kali itawakomesha wataogopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vinginevyo tusipofanya hivi mapambano haya hayataisha kwenye nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo nimuombe sana Mheshimiwa Adadi aone kwamba tulipoamua kuja kufanya haya marekebisha ni kwa sababu ya *experience* ambayo mamlaka imeipata wakati wa kufanya kazi toka imeanza kufanya kazi. Nimuombe sana Mheshimiwa Adadi alidhie kifungu kibaki kama kilivyo.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Adadi ukae kidogo, Waheshimiwa Wabunge kwa kutumia Kanuni ya 28(6) tukiisoma pamoja na fasili ya (15) nakusudia kuongeza muda, japokua fasili ya (6) naweza nisiwahoji; lakini fasili ya (15) ili tuweze kumaliza shughuli zote zilizo mbele yetu kwa mujibu wa ratiba nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaokubaliana na hoja hii ili tumalize shaughuli zilizo mbele yetu.

(Hoja lilitolewa lamuliwe)
(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Walioafiki wameshinda, kwa hivyo tutaendelea Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye nyongeza ya vifungu ambavyo vimeongezwa kuna kifungu cha 15A ambacho kinasema kwamba *grams* au kilo ambazo hazizidi kilo 50 basi wale watu watafungwa miaka 30. Sasa nilikuwa nasema kwamba kama mamlaka na Serikali imeona kwamba miaka 30 haitoshi na wakaamua kuwafunga hawa watu miaka maisha; kilo 50 za mirungi *trafficking* kilo 50 za bangi; wasiwasi wangu ni kwamba jela zitajaa. Kama Serikali inaona kwamba, kwamba ni sawa sawa basi. Sitaki kutoa hoja ijadiliwe, lakini nataka kuiomba Serikali ihakikishe kwamba itakapona imefanya makosa basi ilete haraka huu muswada tubadilishe. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri hajatoa hoja kujadiliwa; lakini labda tusaidie ili tuwe na uwelewa wa pamoja humu ndani. Kwa sababu huyu mwenye 50 si anaweza kuwa nazo 1,000 akagawanyisha kwa watu ili wamshikie? Hafu kila mmoja atakuwa nazo 50 Ama huo uwezekana haupo, ili tuwe tumeenda vizuri hapa. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwanza kwa upande mwingine mmoja, kwamba tunapotunga hii sheria, labda nikirudi kwenye utungaji wa sheria tunakusudia kufanya nini; pamoja na kurundika watu wengi kwenye Magereza lakini tuangalie pia *effect* ya matumizi ya sheria katika kuokoa Watanzania wengi kwenye nchi yetu ambao wangeathirika na matumizi ya dawa, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili tunataka ku-*achieve* kitu gani tena, tunachotaka ku-*achieve* kitu kingine cha pili ni kuwafanya Watanzania wengi waogope kujiingiza kwenye biashara hii ya matumizi ya dawa za kulevya. Kwa hiyo, nikirudi kwenye hoja ya msingi hapa; ukiangalia kwenye

sheria *practice* ambayo tuliigundua kwenye sheria ambayo ilitungwa mwaka 2015, tulipogundua kuna mapungufu hayo tukaja kuiweka hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya msingi ilikuwa haijielezi vizuri ilikuwa haijaweka msingi wa kujielekeza vizuri. Lakini sheria hii sasa inaweka msingi wa kujieleza vizuri, *more than 50 kilograms* kwa hiyo inakuwa zaidi ya hizo *50 kilograms* ziwe 50, ziwe 100,000 ziwe ngapi; hao ndio sasa tutapambana nao; kwa sababu unaweza ukamkuta huyo sasa ana magunia 100,000 ana magunia 1000 ana magunia 10; kwa hiyo sasa yeye atakapokutwa *more than* hiyo, lakini wale *less than* hiyo hao hatuna shida nao. Kwa hiyo, *more than* hii 50 hao lazima twende nao sambamba na hao ndio tutakula nao sahani moja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa nitawahoji kwa sababu Mheshimiwa Balozi hajatoa hoja kama ijadiliwe.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11

Ibara ya 12

Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22

MWENYEKITI: Kifungu cha Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

MHE.BALOZI ADADI M. RAJABU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki nimeomba kifanyiwe marekebisho kutokana na umuhimu wa kifungu hiki. Kifungu hichi kinahusiana hasa na *recording* wakati *interviewer* wakati wa *interrogation* wakati maafisa hawa watakuwa wanafanya kazi hiyo. Lakini kifungu hiki kinaeleza kwamba baada ya *caution statement*, *caution statement* inaandikwa umemuonya mtuhumiwa anaandika baadaye *recording* inachukuliwa, *my argument* ni kwamba hii iishie pale ambapo inasema *in addition to*. Baada ya kuweka *in addition to* tuanzishe kifungu kingine kidogo ambacho kitatoa mamlaka uwezo, ambapo kinasema *in and alternative* yaani:-

"...the recording of interrogation in accordance with the provision of sub-paragraph (xi) shall d be admissible as an alternative to a written questions statement..."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii tutaipa uwezo nguvu kwamba ile *recording* ambayo imechuliwa kama

kutakuwa na *contradiction* kama ile *caution statement* haitakuwa *accurate* basi wapelelezi wataruhusiwa kutumia kifungu hicho ambacho kutakua *recorded* kiweze kukubalika Mahakamani moja kwa moja *this is my argument*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Balozi Adadi, na kama wote tunavyomfahamu ana uzoefu mkubwa sana kwenye masuala ya kupambana na uhalifu. Mimi nilikuwa naomba kupendekeza kwamba mapendekezo ya Serikali kama yalivyo pale tuyaache na sababu zake ni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuna mazingira ambayo ni vigumu kumpata huyu mtu akaandika pia maelezo, tunachotaka kufanya haya maelezo *either in caution statement* (maelezo yale ya onyo) na haya maelezo ya kurekodiwa *either* kwa video au kwa sauti yawe na hadhi sawa. Sasa kwa maana kwamba tusimpe muda mwanya muhalifu kukwepa. Sasa kwa mapendekezo ya Mheshimiwa Adadi ni kana kwamba sasa haya ya *recording* ambayo inafanya chini *sub paragraph 9* yanakuwa ni *secondary* yaani yanakuwa kama unayahafifisha yanakuwa yamekosa fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili la pili tunalikubaliile ya pili hile kwamba sasa kwasababu pale juu kuna *alternative*, pale ambapo sasa hukuchukua yale maelezo ya onyo basi ukachua haya ya *recording* yawe *admissible* kama *alternative to the written statement*. Kwa hiyo *to that extent* nilikuwa naomba kumshauri Mheshimiwa Adadi Rajab akubaliane na mapendekezo haya ya Serikali lakini tunayakubali haya mengine isipokuwa tu ile *propose* ya kwanza ya kuondoa yale maneno lakini haya mengine yote tunayakubali. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kwa hiyo, Serikali ili ajue nini cha kuzungumza hapa, (a) ndiyo ambayo mnaomba aitoe, lakini (b) mnakubaliana nayo. Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

MHE.BALOZI ADADI M. RAJABU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyomuelewa Mwanasheria Mkuu ni kwamba *recording such ya interrogation* ambayo itafanyika basi wataweka *provision* ambayo *recording* hiyo itakubalika moja kwa moja *without the written caution statement*. Kama ni hivyo sina matatizo nayo.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Ile *propose* ya pili ile...

MWENYEKITI: Hebu weka vizuri Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali rudia maelezo yake.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa itakuwa kwamba:-

"... the recording of an interrogation taken in accordance with the provision of sub-paragraph eleven shall be admissible in court as an alternative to written caution statement..."

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tena tunafanya *renumbering* ile (c).

MWENYEKITI: Sawa, sasa tusaidie Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, hapa maneno yanasema *"shall be admissible"* kuna uwezekano wa kuwa *admissible elsewhere than in court*? Kwa sababu kama tukiweka *in court* maana yake *elsewhere* hayatakuwa *admissible* kama wanataka kuyatumia, lakini yatakuwa tu *admissible in court*. Sasa ipi ni bora? kuwa na hii *admissible ya general* ama tuwe *specific* na hiyo ya mahakama?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Kwa kawaida haya tunayoyazungumza saasa ni mahakamani, lakini kama kuna *forum* nyongine yoyote ile ambayo inai-*quasi judicial* basi yanaweza kuwa *admissible*

MWENYEKITI: Kwa hiyo, ni bora ibaki hivi basi *“shall be admissible anywhere where admissibility is needed.”*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Sawa

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nadhani tumeelewa yale aliyokuwa ameleta Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu kwenye kifungu cha 22(a) upande wa Serikali na yeye wamekubaliana kuiondoa lakini (b) na (c) imekubalika hapa, kwa hivyo sasa nitawahoji. Hii namba 3 ndiyo inahusu *renumbering*, namba (c) samahani.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 23

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ruth Mollel.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nimependekeza badala ya kuwa na neno *“Government Analyst”* tuwe na *“Government Chemist”* tu-replace hiyo *analyst* na *chemist*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Antony Peter Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya neno *‘analyst’* kama nilivyosema pale awali badala ya *‘chemist’* ni kwasababu neno hili la *analyst* linatumika na sheria zingine ambazo zinafanya kazi kwa pamoja na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamka pale sheria kama ya *The Criminal Procedure Act* inatamka neno *‘Government Analyst’* kwa kazi ambayo pia imeainishwa katika sheria hii, kwa hivyo ili kuifanya tafsiri yake iwe rahisi ndiyo maana tuliona kwamba badala ya kutumia neno *Government Chemist* ibaki kuwa *Government Analyst* ili iendane na Sheria zingine ambazo zinafanya kazi pamoja na sheria hii.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kujua, tunapozungumzia hawa *analyst* wengine ambao unasema wanafanya kazi pamoja na sheria hii ni pia watakuwa wanashughulika na kupima hizi *drugs* na *precursor drugs* au wanakuwa wanapima na vitu vingine? Nasema hivi kwa sababu binadamu ana hulka ya kuonea, binadamu kama hana hofu ya Mungu anaweza akafanya jambo ambalo siyo sawa kama yule mtu hatujam-*define* sawasawa ajulikane kwamba kweli huyu anayepima hizi *drugs* na *precursor drugs* ni kweli ni mtu ambaye anayetambuliwa na Serikali na siyo nje ya hapo.

MWENYEKITI: Serikali mmeulizwa swali hapo, nani anajibu? Mheshimiwa mtoa hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge asiwe na hofu kwa sababu ukienda kwenye Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni kwamba hizi *laboratory* zote, kwa mujibu wa kifungu cha 13 ni lazima ziwe *registered* na zinawekewa masharti na mtua anayezi-*oversee* ni Mkemia huyo Mkuu wa Serikali kwahiyo yale masharti yote yanayowekwa na mfumo wote wa utaratibu na anayewatambua ni Mkemia huyo Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo hizo *check and balances* zipo. Kwa sababu hiiyo ndiyo maana na sisi lazima tutunge Sheria ambayo inaendana na Maabara nyingine zinazofanyakazi kwa kuzingatia Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali na *regulations* ambazo zimewekwa na Mkemia Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, hilo halina tatizo tatalifanya tu vizuri.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

Ibara ya 25

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ruth Mollel

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo rekebisho lilishafanyika na Seriakli, ahsante.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 27

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 28

Ibara ya 29

Ibara ya 30

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 31

MWENYEKITI: Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki niliona kirekebishwe kumuongezea madaraka zaidi *Commissioner General* kwa zile mali ambazo zinaonekana zimepatikana kwa njia ya *drugs*, sasa pale kuna sehemu ambayo imesema:-

"...subject to sub-section four where the commissioner general receives a report pass one to section 51 sub-section 7 and he satisfied the reasonable ground to believe that the property is being illegally acquired..."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilitaka kuongeza "or abandoned" kwa sababu kuna wakati ambapo hawa watuhumiwa wanakimbia, wanaacha mali zao au wakati

ambapo imeonekana mali zimeonekana pale na hajulikani mwenyewe yuko wapi sasa ni kumuongezea uwezo *Commissioner General* ili aweze kuzitaifisha na kuzifanya mali za Serikali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikiliza Mheshimiwa Adadi, nadhani ana hoja ya msingi. Kwa kweli ana hoja ya msingi na kama ana hoja ya msingi Serikali tunakubaliana na marekebisho hayo ambayo pia yameletwa kwenye jedwali lake la marekebisho.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri tusaidie kabla sijahoji kifungu hiki kwa sababu yakiongezeka haya maneno "*or abandoned*" hiyo sehemu ambayo inapandekewa, maana yake itasomwa hivi; "*That the property has been illegally acquired or illegally abandoned*" hebu muiangalie hiyo tutaendelea kuhoji vingine.

Kwa hiyo, muiangalie ikae wapi ili iwe inasomeka vizuri, kiangalieni vizuri hicho kifungu kwa kukisoma na hayo maneno yaliyopandekewa halafu muone yakae wapi kwa sababu ukiweka tu neno "*or*" hapo linasomeka na hilo neno lililotangulia hapo kwa sababu ni "*acquired or abandoned*" sasa lazima usome na neno "*illegally*" sasa unataka kusema "*illegally abandoned*" pia kwa hiyo angalieni tuliweke wapi wakati tukiendelea kuhoji vifungu vingine.

Waheshimiwa Wabunge tutarudi kwenye kifungu cha 31.

Ibara ya 32

Ibara ya 33

Ibara ya 34

Ibara ya 35

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Jedwali la 1

Jedwali la 2

(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Jedwali la 3

MWENYEKITI: Mheshimiwa Balozi, Jedwali la tatu.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jedwali la Tatu wameingiza nano la Kiswahili "cha" badala ya kuweka "of". Hiyo hiyo inakwenda na jedwali la nne pia nafikiri ni *error* ndogo ambazo zirekebishwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hayo majedwali nafikiri ilikuwa ni *typing error* tunakubalaina kwamba lile neno la "cha" limekaa mahali ambapo siyo mahali pake.

(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

MWENYEKITI: Sawa. Waheshimiwa Wabunge basi tutarejea kwenye kifungu cha 31.

Ibara ya 31

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Balozi taarifa gani unataka kutupa sasa hivi kwa sababu hakuna mtu anayezungumza unayetaka kumpa taarifa kwa sababu kama ninayezungumza ni mimi sipewi taarifa, lakini zungumza labda itatusaidia kwenye kuboresha.

T A A R I F A

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *page* ya pili kwenye marekebisho yangu kwenye jedwali hilo hilo lakini *form* ya nne nilipendekeza kwamba kwa sababu ni suala la *observation* wakati watuhumiwa wale wanapotoa zile dawa basi pawepo na shahidi. Kwa hiyo, ndiyo niliweka hayo mapendekezo kwenye hiyo *form number four*.

MWENYEKITI: Serikali mapendekezo (h) na (d)?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu ukiongeza *name of witnesses* na *signatures* zao haziondoi msingi wa *form* yenyewe jinsi inavyokaa ila inaongeza uhalali wa *form* yenyewe nadhani hatuna shida.

MWENYEKITI: Sawa, kwa hiyo sasa kwa sababu tulihoji pamoja na marekebisho ya Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab kwa hiyo, yataingia hapo. Mko tayari kifungu cha 31? Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyogusia katika eneo hili, tunaona umuhimu wa matumizi ya maneno ambayo Mheshimiwa Mbunge amewasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo yakisomeka kama vile ambavyo imewasilishwa inaweza ikaleta tafsiri tofauti kidogo, vinginevyo vyake inawezekana pia bado tukatumia maneno yale yale lakini kupeleka ujumbe ule ule ambao badala ya kusema kwamba; *“That property has been illegally acquired or abandoned”* tuanze na neno kwanza *“abandoned”* halafu ndyo ifuatie *“illegally acquired”* ili iweze kutengeneza muktadha wa madhumuni hasa ya hiki kifungu *otherwise* likitangulia neno *“abandoned”* kule mbele na huku limeanza *“illegally acquired”* inaweza ikaleta tafsiri tofauti kidogo.

Hilo ndilo ambalo hasa tumeliona hapa na kama Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kapendekeza maneno haya na lengo ni kufanya iingie kwenye kifungu hiki, tuone namna ya *replacement* tu ya haya maneno.

MWENYEKITI: Upande wa Serikali bado kuna shida kiodgo hapo; *Administrator General* ndiye anayeshughulika na *abandoned properties*, sasa huyu hapa ana *properties* ambazo ni mahususi kwenye eneo lake la *drugs*. Sasa ukimpa kama unavyopendekeza ni kana kwamba yaani ni wakati gani utajua ardhi ama mali hii imekuwa *abandoned* ikihusishwa na *drugs* ama iko *abandoned* ile ambayo ni mtu mwingine anahusika nayo kwa sababu *Administrator General* ndiyo anayeshughulika na *abandoned properties in the country, unless the law has changed. (Makofi)*

Hebu tusaidieni hapo ili kama linaleta tabu sasa hivi ni afadhali likienda hivi halafu mkaliangelie mlete hayo marekebisho ili kuweka mazingira yote kwa pamoja, lakini mkiweka namna mnavyoweka hapa haikai vizuri kwa sababu yule *Administrator General* ndiyo anayeshughulika na *abandoned properties* sasa hizi lazima uzihusishe na *drugs* ndiyo ashughulike huyo ambae anashughulika nah ii Sheria.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Administrator General* anaweza kuwa anashughulika na *abandoned property* katika *civil*, kwa mukhtadha wa kawaida tu. Kwa mfano; kuna *abandoned land*, hiyo ni ya *Commissioner of Land*. Chini ya kifungu cha 51 cha Sheria ya Ardhi, *abandoned land* ikikaa pale kwa muda fulani inakuwa *forfeited*, inaipa fursa Serikali kuchukua tena hii ardhi kuwa ya Serikali, lakini katika *criminal justice* kwenye *CPA* pale pia kuna ku-*deal* na *abandoned property. (Makofi)*

Sasa katika muktadha huu na ndiyo umesema huku, ukisoma Sheria yenyewe hii inasema Sheria ile ya *CPA* ile itatumika sambamba na h ii lakini ili kufanya huyu bwana

asiwe akikuta tu mali anabeba yaani sasa hii ni *property abandoned* anajifanya ni yakwake ndiyo mana tulikuwa tunafikiri *proposal* yetu kama alivyoiweka Waziri ilikuwa ni sahihi kwamba ashughulike na hayo ambayo yalikuwa *illegally abandoned*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana, tunaomba tukipendekeza kwamba *proposal* ya Mheshimiwa Waziri kama ilivyokuwa imewekwa pale na kama ilivyowekwa na Mheshimiwa Balozi Adadi tuipokee jinsi ilivyo, lakini kama ulivyosema ulikuwa umefikiri kwamba labda tungeweza kuandalia kama kutakuwa na shida huko mbele tulete marekebisho, lakini kwa kweli hata sisi alivyosema kwenye hii Mheshimiwa Adadi tuliona kwamba ametusaidia sana kwa sababu huu unaweza ukawa mwanya, akiona anapelelezw tu analiacha hapo anakimbia kwao huko Musoma, halafu linakaa tu hapo maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunakushukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa bangi iko nyingi Iringa kuliko Musoma.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chenge.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru wote wawili, AG na Mheshimiwa Adadi. Kwa nini tusiseme hivi, ibaki kama ilivyo "*has been illegally acquired or, being tainted property, is abandoned.*"

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chenge hebu rudia hicho ulichosoma.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Yanabaki "*has being illegally acquired or,...*" sasa weka comma maana tunaelewa *what is tainted property* kwenye muswada huu kwahiyo ndiyo nasema baada ya comma unasema "*being tainted property*". Unaweza kutumia "*present is abandoned or has been abandoned.*"